

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Saba – Tarehe 15 Juni, 2005

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge Kikao cha Saba cha Mkutano wa Ishirini kinaanza. Kabla hatujaanza nieleze ratiba ya leo kwamba baada ya kipindi cha maswali, watapewa nafasi Waheshimiwa Manaibu Mawaziri wahitimishe hoja ya Bajeti.

Halafu atapewa nafasi Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Mipango na Ubinafsishaji naye ahitimishe. Baada ya hapo tutasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni ambapo atapewa nafasi Mheshimiwa Waziri wa Fedha, halafu tutaingia kwenye shughuli za kupiga kura ya kuitisha Bajeti. Kikao kinaanza, Katibu endelea na ajenda inayofuata.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 60

Bendera ya Taifa

MHE. GRACE S. KIWELU (k.n.y. MHE. PHILLEMON NDESAMBURO) aliuliza:-

Kwa kuwa wakati nchi ikipigania Uhuru wake, Watanzania wote Weusi, Wahindi na Wazungu walijumuika wote katika harakati hizo:-

Je, rangi za Bendera ya Taifa zinaashiria nini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba wakati wa harakati za kupigania uhuru wa nchi yetu Watanzania wa rangi zote walitoa mchango wao katika kufanikisha azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Bendera ya Taifa ina rangi nne, rangi hizo ni kijani inayoashiria ardhii ya nchi yetu, rangi ya dhahabu inayowakilisha utajiri na madini, rangi nyeusi inawakilisha watu wa nchi yetu walio wengi yaani Watanzania na rangi ya bluu inawakilisha Bandari inayounganisha pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Na. 61

Huduma ya Akinamama – Hospitali ya Wilaya Ludewa

MHE. STANLEY H. KOLIMBA aliuliza:-

Kwa kuwa tangu kuanzishwa/kuzinduliwa kwa hospitali ya Wilaya ya Ludewa mwaka 1980 haijapata jengo maalum la kuhudumia wazazi wanaojifungua *maternity wing*, na kwa kuwa idadi ya akinamama wanaojifungua sasa imeongezeka na kusababisha msongamano kwa wagonjwa wengine wa kike:

- (a) Je, ni lini Serikali itaondoa kasoro hiyo kwa kujenga *Maternity Wing*?
- (b) Kwa kuwa kulingana na hadhi inayostahili kupewa hospitali hiyo. Je, ni majengo mangapi hayajengwa katika hospitali hiyo hadi sasa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanley Haule Kolimba, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa hospitali ya Wilaya ya Ludewa ilizinduliwa mwaka 1980. Tokea wakati huo imekuwa ikitoa huduma zote za afya ya uzazi na mtoto zikiwa ni pamoja na zile za kliniki ya watoto na wajawazito, huduma za kujifungua, chanjo pamoja na zile za uzazi wa mpango. Vile vile ni kweli kwamba jengo lililotengwa ni dogo na linahitaji kupanuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 ilitenga jumla ya shilingi milioni 4 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wazazi. Fedha hizi zilitumika kufanya usanifu wa ujenzi wa msingi wa jengo hilo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Halmashauri imetenga tena kiasi cha shilingi bilioni 4 kwa ajili ya kuendeleza kazi hiyo ya ujenzi wa wodi ya wazazi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mwongozo wa Wizara ya Afya, majengo ambayo bado yanahitajika katika Hospitali ya Wilaya ya Ludewa ni pamoja na yafuatayo:-

- Jengo la Maabara;
- Jengo la kuhifadhia maiti lenye jokofu lenye uwezo wa kuhifadhi angalau maiti wanne;
- Jengo la wodi ya wazazi na jengo la huduma za kliniki ya Afya ya Uzazi na Mtoto;
- Jengo la Utawala kwa ajili ya Ofisi za timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya za Wilaya na Menejimenti ya Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wingi wa majengo haya na uhaba wa fedha, Halmashauri itajenga majengo haya kwa awamu kadri itakavyokuwa inapata uwezo wa kifedha.

MHE. STANLEY H. KOLIMBA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa imebainika kuwa kuna majengo kadhaa ambayo hayajajengwa hadi hivi sasa katika kipindi cha miaka 25 iliyopita. Je, Serikali inaweza kuahidi kwamba sasa itakuwa na mpango kabambe na mkakati mzuri wa kujenga majengo hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nia kwa kweli ya Serikali ni nzuri sana tunatamani majengo yale yote ikiwezekana yamalizike ndani ya kipindi kifupi kadri inavyowezekana, lakini tatizo letu kubwa ni ufinyu wa bajeti. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Stanley Kolimba kwamba kadri Halmashauri hiyo itakavyokuwa inaweka suala hili katika bajeti kupitia Mkoa sisi kiofisi tutajitahidi sana kuunga mkono ili kuwezesha kuharakisha ujenzi wa majengo hayo yote.

Na. 62

Usimamiaji wa Maendeleo katika Ngazi ya Kijiji – Tarafa

MHE. MUSA A. LUPATU aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika azma yake ya kuwapa wananchi madaraka ya kusimamia shughuli za maendeleo yao katika ngazi ya Kijiji, Kata na Tarafa imeanzisha ajira za Wataalam na Watendaji mbalimbali katika Kijiji, Kata na Tarafa:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kujenga ofisi zinazostahili katika ngazi hizo ili wataalam na watendaji katika ngazi hizo wapate sehemu ya kufanya kazi zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI
ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musa Lupatu, Mbunge wa wa Korogwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kukubaliana na maoni ya Mheshimiwa Mbunge, kuhusu Serikali kuwapa wananchi madaraka ya shughuli za maendeleo yao katika ngazi ya Kijiji, Kata na Tarafa. Dhana hii ya kupeleka madaraka kwa wananchi chimbuko lake hasa ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 hususan Ibara ya 146. Tunaamini madaraka haya ni ya kuleta tija na kwamba hayabgui wala hayana mipaka ili mradi hayavunji sheria. Mfano kama Kata au Kijiji kinahitaji kujenga Zahani hakuna anayewazuia maadam wanafuata na kuzingatia taratibu zilizowekwa katika masuala ya ujenzi kama vile ramani, na mahitaji halisi kupitishwa kwenye vikao husika na kadhalika. Utaratibu huu ndiyo unafuatwa katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe tayari inatekeleza kazi hiyo kwa kushirikiana na wananchi kati ya vijiji 134 vilivyopo kwenye Halmashauri hiyo, Vijiji 43 vina Ofisi za Vijiji ambazo zilijengwa kwa nguvu za wananchi. Kwa mfano, Vijiji vya Changelikwa, Kwamadolwa, Kwameta, Chekelei, Kwasunga na Magamba na Kwalukonge kwa kutaja vichache. Vilevile katika ngazi ya Kata kuna Ofisi 8 kati ya Kata 20 ambazo zimejengwa na nguvu za wananchi na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe kupitia mradi uliokuwa unaitwa *Village Management Training Programme (VMTP)*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 na hasa kifungu 113(b) kila Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kufanya jambo lolote linalohusiana na huduma katika Mamlaka yake ilimradi liko chini ya Sheria katika eneo lake. Kwa hiyo, kimsingi ni jukumu la wananchi wa maeneo husika na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe kujenga ofisi hizo ili kuimarisha utendaji. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kuzidi kuwashamasisha na kuwashirikisha wananchi kujenga ofisi zinazostahili katika ngazi mbalimbali zitakazotumiwa na Wataalam na Watendaji mbalimbali ili kuleta ufanisi na tija.

MHE. MUSA A. LUPATU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya ufasaha. Kwa kuwa Mpango wa MMEM umefanikisha sana ujenzi wa shule za misingi; na kwa kuwa MMEM imekuwa kichocheo. Je, Serikali haioni kwamba ingekuwa jambo la busara kuchangia kama ilivyofanya kwenye MMEM katika Halmashauri za Wilaya ili fedha hizo ziweze kuwa kichocheo kwa ajili ya wananchi kujenga ofisi hizo za Vijiji na Kata? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI

ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, mimi naelewa nia nzuri sana ya Mhesimiwa Musa Lupatu ya kutaka kuwa na ofisi nzuri katika Vijiji na Kata zetu na ingelipendeza vilevile kama Serikali ingekuwa na uwezo tungeweza kutafuta kila mbinu kuchangia jambo hili. Lakini kwa kweli kupanga ni kuchagua fedha yenyewe ya MMEM ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Kwa hiyo, hatutarajii kwamba tunaweza kuwa na uwezo zaidi wa kuweza kusaidia kuchangia katika ujenzi wa ofisi hizi. Lakini jambo tunalosisitiza hapa ni kwamba Halmashauri ikipanga vizuri na kama wananchi wakihamasishwa vizuri ofisi hizi zinaweza kujengwa kutohana na uwezo wa wananchi kwa sababu katika sehemu nyingi imefanyika hivyo. Kwa hiyo, mimi namwomba Mheshimiwa Musa Lupatu tusaidiane tu katika jambo hili kwa sababu liko ndani ya uwezo wa Halmashauri zetu wenyewe.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niulize swali moja ndogo la nyongeza. Kwa kuwa siku zote Serikali imekuwa ikihimiza wananchi wajitolee na ndiyo Serikali inaingia, Serikali inasema anza wewe na yenyewe itamaliza. Kama alivyojibu katika swali la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Halmashauri ya Korogwe imejitahidi sana kujenga ofisi hizi lakini zimekwama. Serikali haioni kuna umuhimu wa kuamua hao wananchi ambao wamefikia katikati ili waweze kuzikamilisha hizo ofisi kwa sababu Serikali ikiwa na ofisi nzuri ndivyo ambavyo huduma zitakuwa nzuri. Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kusaidia katika hilo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI

ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme kwamba Halmashauri yetu ya Wilaya ya Korogwe imekwishaanza kutekeleza jukumu hili na kama pengine katika kuwahamasisha wamewahamasisha bila kuzingatia hali halisi ya uwezo wa wananchi katika kukamilisha ofisi hizo ni jambo ambalo wakikaa katika Halmashauri wanaweza wakazungumza wakaona ni zippi zinaweza zikasaidiwa na Halmashauri yenu na zippi zinaweza zikasubiri zisianze kujengwa tena mpaka mtakapokuwa mmekamilisha zilizokuwepo tayari.

Na. 63

Barabara - Makao Makuu Wilaya Iramba – Misigiri - Kiomboi - Bomani

MHE. LEONARD M. SHANGO aliuliza:-

Kwa kuwa muda mrefu sana barabara inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Iramba kutoka Kijiji cha Misigiri kilichopo barabara kuu ya Dodoma – Mwanza na Kiomboi Bomani yenyе urefu wa kilometra 21 hajawahi kufanyiwa matengenezo au kuwekwa kwenye mpango wa matengenezo rasmi na Wakala wa Barabara Mkoa (*TANROADS*) ila tu kwa matengenezo ya dharura ya kufukia fukia sehemu korofu yanayojitokeza mwaka hadi mwaka:-

- (a) Je, Serikali inatoa sababu gani za msingi za kutoitengeneza barabara hiyo na kutokuona umuhimu wa kuhudumia kimawasiliano Makao Makuu ya Wilaya?
- (b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka mipango mizuri ya kuitengeneza barabara hiyo sasa kwani hali yake ni mbaya sana na inapitika kwa shida sana wakati wote?
- (c) Serikali kwa kuona umuhimu wa kiungo cha barabara hiyo yaani Misigiri – Kiomboi Bomani haiwezi kuunganisha mara moja na matengenezo yanayoendelea sasa ya barabara kutoka Kijiji cha Kizega – Ndago – Singida yenye umbali wa takriban kilometra 110 ili kuboresha mawasiliano kati ya Mkoa na Wilaya ya Iramba?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Mlumba Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Barabara ya Kiomboi –Misigiri yenye urefu wa Kilometra 21, ni barabara ya Mkoa inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Singida. Barabara hii imekuwa ikipata matengenezo ya kawaida ambayo hayakuwa yanakidhi hali halisi ya uharibifu. Ili kuboresha hali ya barabara hii, Serikali iliingiza barabara hii katika programu ya ukarabati wa barabara za Mkoa chini ya Mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) katika mpango wa kupunguza umaskini. Barabara zingine ambazo zinahusika na mpango huu kwa Mkoa wa Singida ni pamoja na Sepuka - Ndago; Ndago - Kizaga; Ilongero – Gumanga; Igugumo – Nduguti; Ilongero - Ngamu; Kititimo – Kinyamshindo na Singida - Sepuka zenyе jumla ya kilometra 267. Naomba nitoe taarifa kuwa Mkandarasi *CETIC* toka China alishaanza kazi tangu Januari 2004 na anatarajiwa kukamilisha kazi hii ifikapo Julai, 2005 kwa gharama ya shilingi milioni 4,695.43. Hivi sasa Mkandarasi amekamilisha matengenezo makubwa katika barabara ya Singida – Sepuka, Sepuka – Ndago na Ndago - Kizaga na kwa sasa anaendelea na matengenezo katika barabara ya Misigiri – Kiomboi tangu tarehe 10 Mei, 2005.

MHE. LEONARD M. SHANGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Iramba Magharibi namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri apokea shukrani za wananchi wa Iramba Magharibi kwa Serikali kukubali kuanza kutengeneza sasa barabara hii na matengenezo yameanza na yanaendelea vizuri sana. Sasa swali je, Serikali itakubali ombi la wananchi la kutengeneza barabara ya kutoka Kiomboi madukani mpaka kwenye lango la hospitali ya Wilaya ya Kiomboi kwa sababu barabara hii urefu wake ni takriban chini ya kilometra 1, lakini ni muhimu sana kwa huduma za hospitali? Kwa hiyo, ombi hili naomba kama Serikali inaweza kukubali. Ahsante. (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, shukrani Serikali imezipokea mara mbili. Barabara ya kutoka Kiomboi madukani hadi lango la hospitali ya Kiomboi nitawasiliana na *Regional Manager* tuone tunawezaje kusaidia. (*Makofî*)

Na. 64

Barabara ya Nangurukuru – Liwale na Liwale Nachingwea

MHE. HASSAN C. KIGWALILO aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Nangurukuru hadi Liwale na Liwale – Nachingwea ni kichocheo kikubwa kwa maendeleo ya wananchi wa Liwale; na kwa kuwa Serikali imeonyesha dhamira ya kuboresha barabara hiyo kwa kukarabati sehemu korofî lakini hasa sasa Liwale haifikiki kirahisi kwa kutumia barabara hiyo hasa wakati wa masika:-

- (a) Je, juhudî za Serikali za kuboresha barabara hiyo ya kati ya Nangurukuru kwenda Kimambi hadi Liwale na kutoka Liwale- Nachingwea zimefikia wapi na ni lini itamalizika ili kuwaondolea wananchi wa Liwale kero hiyo?
- (b) Je, Mradi wa barabara wa dola za Kimarekani U\$ 600,000/700,000/= unaofadhiliwa na *OPEC* chini ya *HIPC* uliolenga kutengeneza sehemu korofî zenye umbali wa kilometa 20 – 30 kuanzia Liwale Mjini kupitia Kijiji cha Mikunya katika barabara iendayo Nachingwea utaanza lini?
- (c) Je, Serikali inachukua tahadhari gani ili kupata Makandarasi wenye sifa nzuri na waaminifu ambao hawatakjamisha juhudî za Serikali za kuboresha barabara nchini kote hasa zile ziendazo pembezoni mwa nchi kama vile Wilaya ya Liwale?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Nangurukuru - Liwale yenyé urefu wa kilometa 231 na ile ya Liwale hadi Nachingwea yenyé urefu wa kilometa 136 ni barabara ya Mkoa zenye tabaka la udongo na charangwe. Barabara hizi zinahudumiwa na Wizara yangu kuptit Wakala wa Barabara (*TANROADS*).

Kwa kutambua umuhimu wa barabara hiso, Wizara yangu imekuwa ikizifanyia matengenezo mbalimbali ili kuhakikisha zinapitika wakati wote wa mwaka. Matengenezo ambayo yamekwishafanyika kwenye barabara hiso na gharama zake ni kama ifuatavyo:-

(i) Barabara ya Nangurukuru – Liwale kuptitia Vijiji vya Njinjo, Kimambi, Zinga, Kichonda ni kama ifuatavyo:-

- Mwaka 2002/2003 - matengenezo ya sehemu korofi kilometra 25 kwa gharama ya shilingi milioni 250.
- Mwaka 2003/2004 - matengenezo ya sehemu korofi kilometra 15.4 kwa gharama ya shilingi milioni 167.7.
- Mwaka 2003/2004 - ukarabati wa madaraja ya Njinjo na Zinga Kibaoni kwa gharama ya shilingi milioni 42.
- Mwaka 2004/2005 – Ukarabati wa madaraja ya Kilongo na Kimambi kwa gharama ya shilingi milioni 51. Aidha, barabara hii iliendelea kufanyiwa matengenezo ya kawaida katika urefu wake wote na kuifanya ipitike kwa muda wote wa mwaka.

Barabara ya Nachingwea – Liwale:-

- Mwaka 2000/2001 - matengenezo ya sehemu korofi kilometra 12 kwa gharama ya shilingi milioni 85.0.
- Mwaka 2001/2002– matengenezo ya sehemu korofi kilometra 10 kwa gharama ya shilingi milioni 108.
- Mwaka 2003/2004 - matengenezo ya daraja la Kibutuka kwa gharama ya shilingi milioni 30. Aidha, barabara hii ni kati ya barabara zitakazokarabatiwa kwa kiwango cha changarawe katika mpango maalum wa kukarabati barabara za Mkoa wa Lindi zenyenye jumla ya urefu wa kilometra 200 chini ya ufadhili wa *OPEC* na Serikali ya Tanzania.

(b) Mradi wa barabara unaofadhiliwa na *OPEC* chini ya *HIPC* unalenga kuimarisha sehemu ya kuanzia Liwale Mjini hadi Mikunya yenye urefu wa kilometra 30. Mhandisi Mshauri amekwishakamilisha maandalizi ya nyaraka za zabuni. Zabuni zinategemea kuitishwa mwishoni mwa mwezi Juni mwaka huu 2005. Aidha, Mkandarasi anatarajiwa kuanza kazi rasmi mwezi Agosti, 2005.

(c) Wizara yangu inachukua tahadhari kuhakikisha kazi za barabara zinafanyika kwa kiwango kinachofaa na kukamilika kwa muda uliopangwa.

Kwa kuzingatia hayo, Wizara ya Ujenzi kuptitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) itafanya manunuzi kulingana na Sheria Mpya ya Manunuzi (*Public Procurement Act – 2004*). Katika kufanya manunuzi hayo matangazo ya zabuni yatawekwa kwenye magazeti yanayosomwa kote nchini ili kuhakikisha kwamba Wakandarasi wengi na wenye sifa zinazotakiwa wanapata taarifa ya zabuni. Aidha,

uchambuzi wa kitaalam unafanywa kwa makini ili kuwapata Makandarasi wanaofaa kwa kwa kazi hizo.

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu hayo mazuri nina maswali mawili madogo ya nyongeza na ningependa kupata majibu yake pia.

(a) Kwa vile fedha amesema zimeshatengwa kwa ajili ya kilometra 30 toka Mjini Liwale Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutupa *time frame* ya kusema kazi hiyo itakamilika lini?

(b) Mheshimiwa Naibu Waziri anaelewa kwamba katika kipindi kilichopita barabara ya Nangurukuru hadi Liwale ilikuwa haipitiki wakati wa masika wakati amesema ilikuwa imekarabatiwa kwa kipindi chote cha mwaka iweze kupitika. Anaelewa kwamba ilikuwa haipitiki?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kutoa *time frame* ya utengenezaji wa barabara ni lazima iwe tayari imekwishapatiwa *tender* na Mkandarasi ndiye atakayetoa *time frame* kwamba barabara hii itanza kuanzia tarehe hii mpaka tarehe hii na tarehe hii nitafanya hiki na tarehe hii nitafanya hiki. Baada ya kupata Mkandarasi tunaweza kumpa Mheshimiwa Mbunge *time frame* ya utengenezaji wa barabara, kwa sasa hivi hatuvezi.

Kuhusu (b) ninaelewa Mheshimiwa Mbunge anahangaika sana na barabara hii amekuja mara nyingi na hata wakati wa masika amekuja na yeye ni shahidi kwamba kufika kwake pale ni kwamba barabara hii inapitika. Lakini vilevile ni shahidi kwamba wakati anakuja ofisini kwangu tulwasiliana na *Regional Manager* aifungue barabara hiyo ninamshukuru sana anajitahidi sana na yeye anaelewa kwamba tumejitahidi kiasi cha kutosha. (*Makofi*)

SPIKA: Swal la msingi linahusu Nangurukuru – Liwale. Sasa nani anajua kule!

MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Nangurukuru hadi Liwale ni muhimu sana kwa kusafirishia korosho, ufuta kama ile barabara ya Mtwara - Tandahimba na Masasi. Je, kwa nini barabara hizi muhimu zisitengenezwe kwa kiwango cha lami kabisa kuna tatizo gani, zitengenezwa kwa kiwango cha lami jambo hili liishe kuzungumzwa hapa Bungeni? (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa barabara ya Mtwara-Tandahimba hadi Masasi ni muhimu sana kwa kusafirishaji wa korosho na vilevile abiria na usafiri wa kawaida. Lakini tatizo kubwa ambalo Serikali inashindwa kutengeneza barabara za lami katika sehemu hii na zingine ni ufinyu wa bajeti ambayo na nyie Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi hapa, hatuna uwezo wa kufanya hivyo.

Uboreshaji wa Elimu Nchini

MHE. MARIA D. WATONDOHA aliuliza:-

Kwa kuwa elimu haina mwisho; na kwa kuwa Serikali imepania kuboresha elimu nchini:-

(a) Je, tangu mwezi Julai, 2003 hadi Desemba, 2004 ni walimu wangapi wameweza kujiendeleza toka Daraja la C kwenda A; na A kwenda *Diploma* na *Diploma* kwenda Shahada; na ni wangapi wamerudi darasani kufundisha?

(b) Kwa kuwa elimu ya msingi humjengea msingi bora wa masomo mwanafunzi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na walimu bora wenye ujuzi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO
(k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, walimu waliojiendeleza katika kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokana na jumla ya walimu 52,754 wa Daraja B/C walimu 26,382 sawa na asilimia 50 wamo katika mafunzo maalum ya kuendelezwa kuwa Daraja A ambayo yalianza mwezi Agosti, 2003 na yatamatilizika mwezi Mei 2006.

(ii) Walimu 229 waliokuwa wa Daraja A wamehitimu kujiendeleza kuwa na Stashahada; na

(iii) Walimu 266 waliokuwa na Stashahada wamehitimu kujiendeleza kuwa na Shahada.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kwanza kabisa ya Mwalimu ni elimu anayoipata akiwa shulen ianapopata elimu ya msingi na sekondari. Kuanzia mwaka huu mtaala mpyaunaotekeleza taarifa iitwayo: “*The Tanzania Education System for the 21st Century*”, umeanza kutumika Kidato cha kwanza kwa lengo la kuinua ubora wa elimu ili iendane na malengo tuliyojiwekea katika Dira ya Maendeleo Tanzania 2025. Katika mafunzo ya Ualimu zinachukuliwa hatua zifuatazo:-

(i) Kuboresha mitaala ya Ualimu ambapo mwongozo wa matumizi ya Njia na Mbinu Shirikishi katika kujifunza na kufundishia umekamilika. Hadi Desemba 2004, jumla ya wawezeshaji 2,610 wamepatiwa mafunzo katika matumizi ya njia hizi.

(ii) Kuboresha mafunzo ya Ualimu kazini na tarajali yenyе kuzingati Njia na Mbinu Shirikishi. Jumla ya walimu 7,070 mwaka 2002, walimu 14,836 mwaka 2003 na walimu 10,833 mwaka 2004 wamepatiwa mafunzo hayo.

(iii) Jumla ya vitabu 23,000 vya Elimu ya Ualimu vimenunuliwa kati ya Julai 2002 na Machi 2005 kwa lengo la kuboresha mafunzo ya taaluma na utaalumu katika Vyuo vya Ualimu.

(iv) Kuendeleza wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu ili kupata wakufunzi wenye ujuzi wa kuandaa walimu bora, ambapo jumla ya wakufunzi 270 wamepatiwa mafunzo katika Mitaala, Ufundishaji, Utafiti na Malezi; na wakufunzi 250 wanaendelea na masomo ya Shahada ya Chuo Kikuu Huria Tanzania.

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali yafuatayo:-

(a) Takwimu zinaonyesha kwamba kuna walimu wengi ambao wameweza kujiendeza kutoka ngazi mbalimbali ili wapate taaluma na vilevile tegemeo la walimu ni kupata maslahi. Je, walimu hao waliotoka daraja la C kwenda A wameongezewa mishahara kwa kadri walivyoongeza elimu na wale wa *diploma* na kuendelea?

(b) Pamoja na maelezo mazuri ya mbinu zote zinazotumika kwa ajili ya kuongeza ujuzi wa walimu waweze kuwa walimu wazuri. Je, Serikali imeweza kuangalia kwamba walimu hao ambao wanaishi vijiji wanahitaji motisha ili ujuzi huo waweze kuutafsiri unahitaji kuijandaa usiku na kuna utaratibu gani wa kuwawezesha walimu hao wawe na mazingira mazuri ya nyumba za kuishi ili waweze kuandaa masomo yao vizuri na ujuzi wao wautumie inavyotakiwa? Ahsante. (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mwalimu anapanda daraja kutoka daraja moja kwenda nyingine ni lazima na maslahi yake nayo yabadilike kwa sababu mishahara ya Walimu inakwenda na madaraja yao.

Kwa hivyo hili suala lake la kwanza ni kwamba wale Walimu ambao wamefanikiwa kupanda daraja baada ya kujiendeza kutoka C kwenda B, B kwenda A, A kwenda Stashahada, sio tu wamepandishwa mishahara lakini na wale ambao wamestahili kutoka Shule ya Msingi kwenda Sekondari wamefanyiwa hivyo.

Kuhusu motisha ya mazingira mazuri ya nyumba za Walimu Serikali inaliangalia hilo kwa makini ndiyo maana katika mwaka wa 2004 tumejenga nyumba 1,633. Mwaka

huu 2005 tunategemea kuwa na nyumba 2214. Mwaka 2006 tunategemea kuwa na nyumba 3,890. Mwaka 2007 tunategemea kuwa na nyumba 6,337. Mwaka 2008 tunategemea kuwa na nyumba 5,910 na awamu ya kwanza wa mpango wa MMES utakapokamilika mwaka 2009 tunategemea kuongeza nyumba nyingine 3,268. (*Makofî*)

Katika utaratibu huu bila ya shaka Wizara ya Elimu na Serikali kwa ujumla inajitahidi kutengeneza mazingira mazuri ili Walimu waweze kuandaa masomo yao vizuri.

MHE. BENITO M. MALANGALILA: Mheshimiwa Spika, katika jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali ina mpango wa kutoa mafunzo ya utaalamu kwa ajili ya Walimu katika Shule za Msingi. Na kwa kadri ninavyoolewa mimi utaalamu kwa vijana wetu wa Shule ya Msingi watakaomiliza masomo na kurudi huko Vijijini ni katika masuala ya kilimo na ufundi.

Sasa Serikali inaweza kutoa sababu za msingi kabisa ambazo zinaifanya Serikali ifute mitaala ya ufundi na kilimo katika Shule za Msingi na Sekondari?

SPIKA: Hilo ni swali jipya kabisa liletwe kwa njia zake za kawaida. (*Makofî*)

Na. 66

Usimamizi wa Masafa Katika Mawasiliano

MHE. JANET B. KAHAMA (k.n.y. MHE. PHILIP A. MAGANI) aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inayo Mamlaka inayosimamia pamoja na masuala mengine ya mawasiliano mgawanyo wa masafa ya kuitisha mtandao wa mawasiliano, ili kuhakikisha kuwa matumizi ya masafa hayo hayaingiliani:-

(a) Je, Mamlaka imeweka utaratibu gani ulio wazi wa kuhakikisha kuwa kila mtumiaji anatumia masafa alivyopewa bila kuingilia masafa ya wengine?

(b) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa na Mamlaka dhidi ya wale wanaoingilia au kupora masafa ya wengine?

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philip Alfred Magani, Mbunge wa Ruangwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ili kuhakikisha matumizi ya rasilimali ya masafa ni sahihi bila ya kuwa na maingiliano, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania inao Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Masafa (*National Frequency Plan*). Mpango huu unazingatia Sera ya Taifa ya Mawasiliano (*National Telecommunication Policy*), Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*National ICT Policy*) na Mpango wa Mgawanyo wa Masafa

Kimataifa ambao husimamiwa na Umoja wa Simu Duniani yaani (*The International Telecummunication Union-ITU*) nchi zote wanachama tumekubaliana kutekeleza mpango huo.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu wa Taifa wa Masafa, pia unazingatia makubaliano juu ya matumizi ya masafa baina ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*) na pia baina ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*). Jukumu la Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) ni kusimamia, matumizi sahihi ya rasilimali ya masafa.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu wa Taifa wa Masafa, unahakikisha kwamba masafa hayana maingiliano. Mamlaka imeyagawa masafa katika wigo mbalimbali (*frequency bands*) kulingana na huduma zinazokusudiwa kutolewe (*type of service*). Wakati mwengine wigo huzingatia aina ya teknolojia inayokusudiwa kutumiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ruangwa tumefuatilia sana maendeleo ya Wilaya ya Ruangwa kwa upande wa mawasiliano. Kwa Ruangwa *TTCL* wamegawiwa masafa ya *7 megawatts* na simu za mkononi wamegawiwa masafa ya *900 megawatts*. *TTCL* ina mpango wa kuunganisha Ruangwa kwa njia ya kisasa *digital microwave* na kuwezeshe kutoa huduma za simu za mkononi na za msingi. *CELTEL* tayari wamejenga mnara hapo Ruangwa.

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge walishangilia kwa kupiga makofi mara alipoingia Bungeni Waziri Mkuu Mhe. Frederick Sumaye*)

SPIKA: Kabla hatujaendelea Waheshimiwa Wabunge niliwatangazia mapema wiki iliyopita kutokuwepo Bungeni kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa natambua kwamba amerejea Bungeni na nashukuru kwamba mnatambua kuwapo kwake kwa makofi. (*Makofi*)

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningombwa kutaka kujua mpaka sasa hivi ni watu wangapi wamekwishachukuliwa hatua yoyote?

Pili, je Serikali sasa haioni kuwa kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa watu waweze kuwafichua wale wanaoingilia masafa ya wenzao. Ahsante sana? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano ikipata taarifa ya kuingiliana kwa masafa basi hutumia chombo maalum ambacho kinaitwa *frequency inspector monitoring equipment* kuchunguza huo muingiliano. Baada ya kuthibitisha taarifa za namna hiyo basi anayeingilia masafa huadhibiwa kufuatana na mkondo wa sheria. Si tatizo la kawaida sana, kwa hiyo hatuna takwimu sasa hivi zinazoonyesha ni wangapi wameingilia. Lakini limo katika uwezo wetu kuweza kuwatambua halijatupatia matatizo mpaka sasa. Kuhusu elimu *TCRA* inatumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na matangazo kwenye vyombo vyao habari,

semina, warsha na njia nyingine kuhusu mgawanyo wa masafa na muingiliano wa masafa. (*Makofî*)

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa inafahamika kwamba *frequency* haziingiliani katika masuala ya mawasiliano na Wilaya nyingi mpaka sasa hivi zinahitaji mawasiliano lakini kutokana na gharama kubwa za kuweka minara ya mawasiliano inawia vigumu kwa Kampuni hizi kutekeleza jambo hilo. Je, Serikali imefikia wapi suala zima la kuchangia mnara mmoja kwa Makampuni yanayotaka kupeleka mawasiliano katika Wilaya hizo. Ahsante sana?

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli Kampuni za Simu zingetumia mnara mmoja kwa maana ya kugawanya eneo la kutumia basi ingekuwa afadhali kwa sababu fedha zinazotumika kujenga minara mingine zingeweza kwenda mahali pengine. Tuliacha kwa makusudi hilo lisifanyike kwa sababu tulikuwa tunataka wawekezaji waje kwa wingi. Lakini baada ya sasa minara kuenea tunachosisitiza ni kwamba Kampuni zinapokuja au zinapotaka kwenda kwenye maeneo mbalimbali ya nchi kwa kweli tunawasisitizia watumie minara kwa pamoja. Na hili huwa sasa wanalifanya. Kwa mfano *VODACOM* na *ZANTEL* kwa upande wa Unguja na Pemba wanatumia minara kwa pamoja. Kwa mfano *CELTEL* na *TTCL* wanatumia minara kwa pamoja. *ZANTEL* wanapokuja Bara kuanzia tarehe 7 Julai, 2005 wameamua kwamba badala ya kujenga minara yao watazungumza na wenye minara hizi Kampuni nyingine ili waweze wakatumia minara hiyo. (*Makofî*)

MHE. KHAMIS AWESU ABOUD: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize suala la nyongeza. Kwa kuwa wapo wateja waliopoteza *line* zao za simu katika *line* mbalimbali. Lakini kwa bahati nzuri ukienda katika Wizara unawenza ukapewa *line* ile ile. Je, hawako watu zaidi ya mmoja waliopewa *line* hiyo hiyo?

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, si kawaida kutoa namba ile ile kwa watu zaidi ya mmoja. Ikitokea hivyo ni kwa sababu yule aliyekuwa na namba ile awali haitumii tena.

MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nchini India simu za mkononi wanatoza shilingi 20 kwa dakika moja. Na hivi karibuni kuna Kampuni inataka kuanzisha simu za mkononi ili itoze kati ya shilingi 20 mpaka 30 kwa dakika moja na mimi nimefika katika Wizara hii kuomba masafa na Wizara ikasema kwamba haina masafa kwa sasa hivi.

Je, kwa vile *TRITEL* ilijiondoa katika kutoa huduma hizi na kwa vile mawimbi yake yapo je, Serikali itakuwa tayari kuipa Kampuni hii iweze kutoa huduma kwa shilingi kati ya 20 mpaka 30 kwa dakika moja badala ya shilingi 300 kwa dakika moja? (*Makofî*)

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naamini kuhusu India teknolojia ambayo inazungumzia si GSM isipokuwa ni inayoitwa *SDMA*. Ukichukulia ukubwa wa India na wingi wa watu kwa hiyo inaeleweka kwa nini bei za India ni rahisi zaidi kuliko bei za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masafa ya *TRITEL* ningependa kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba hivi sasa *TCRA* imekuja na mpango mpya wa kutoa leseni ambao leseni hutolewa kwa huduma zaidi kuliko kufuatana na teknolojia. Kwa hiyo mwenye kutaka leseni inabidi aombe kufuatana na huduma anayotaka kutoa.

Kwa hiyo, baada ya kuwa na mpango huu mpya basi kwa kweli huwezi ukasema kuna masafa yametengwa kwa ajili ya *TRITEL* ambayo yako wazi kwa ajili ya Kampuni ambayo Mheshimiwa Mgaywa anaiwakilisha. Lakini namwomba afike *TCRA* ili aweze akawasiliana nao kuhusu kuelezwu huu mpango mpya ambao ni mpango wa ufanisi ambao utaleta maendeleo makubwa ya mawasiliano nchini tunamkaribisha. (*Makofi*)

Na. 67

Uwanja wa Ndege Mwanza

MHE. JACOB D. SHIBILITI (K.n.y. MHE. STEPHEN M. KAZI) aliuliza:-

Kwa nini, mpaka sasa Uwanja wa Ndege Mwanza haujapewa hadhi ya Kimataifa kama ilivyoahidiwa wakati Serikali ilipojibu swali langu Na. 112 hapo tarehe 22 Aprili, 2004?

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo niliyotoa awali wakati nikijibu swali namba 126; katika kikao cha Bunge cha Aprili, 2004 napenda nifafanue kwamba kulingana na tafsiri ya Shirika la Mataifa la Usalama wa Anga (*ICAO*) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa ni kiwanja ambacho kinahudumia ndege kutoka nje ya nchi yaani (*Airport With International flights*). Kiwanja chenye hadhi hiyo kinapaswa kutoa huduma za uhamiaji na forodha na kwa tafsiri nyingine inaweza kuwa ni kile kinachoitwa (*entry exit airport*). Kwa maana ya tafsiri hiyo pana Mwanza ni Kiwanja cha Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kiwanja hutangazwa rasmi kuwa cha Kimataifa pale ambapo kinasajiliwa na (*ICAO*). Kimsingi hakuna tatizo kwa kukisajili na (*ICAO*) Kiwanja cha Mwanza kuwa cha Kimataifa.

Hata hivyo, nchi inaposajili kiwanja kuwa cha Kimataifa inapasa kutumiza masharti ya kuweka viwango, vifaa na huduma ambazo zinakidhi viwango vinavyotakiwa na (*ICAO*) yaani (*standards and recommended practices*) na kuwa kwenye orodha ya kukaguliwa mara kwa mara na (*ICAO*). Ulaguzi wa (*ICAO*) ni kuhakikisha kuwa viwango vya Kimataifa vilivyowekwa kuhusiana na usalama na huduma yaani (*safety and security facilitation*) vinafikiwa na kuendelezwa. Maana ya kutofikiwa kwa viwango hivyo wakati wa ulaguzi ni kwa (*ICAO*) watatangaza kasoro yaani (*deficiency*) zilizopo na kunyima utoaji wa leseni au cheti kinachoitwa (*Airport Certification*) ambacho ni lazima kwa viwanja vya ngazi hiyo. Kulingana na utaratibu wa sasa wa (*ICAO*) ulioanza Novemba, 2004 vifaa ambavyo inalazimika viwepo ni pamoja na mtandao wa kuwezesha ndege kutua kwa kutumia mitambo maalum (*instrument landing system*), mitambo ya kupimia umbali (*distance measuring equipment*), jengo la abiria linalokidhi viwango vya huduma. Umuhimu wa kuwepo kwake utategemea wingi wa ndege zinazotua na kuruka kutoka kiwanja hicho.

Mheshimiwa Spika, kutangaza rasmi kuwa kiwanja kuwa cha Kimataifa kunakifanya kiwanja kuwa kiwanja mbadala yaani *alternate airport* kwa saa 24 kwa ndege zinazotumia viwanja vya Kimataifa vilivyosajiliwa na (*ICAO*) vilivyo jirani. Kwa Mwanza viwanja hivi ni pamoja na Jomo Kenyatta International Airport Entebbe na Kigali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kutokana na soko huru la usafiri wa anga linalotokana na mikataba baina ya nchi na nchi yaan *BASA* Makampuni ya Ndege ya nje yako huru kutumia viwanja vyetu vyenye hadhi ya *entry exit* kikiwepo kiwanja cha Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imekuwa na mpango wa kukiendeleza Kiwanja cha Ndege cha Mwanza hatimaye kukiangaza rasmi na (*ICAO*) kuwa cha Kimataifa. Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kina njia ya kurukia na kutua yenye kiwango cha Kimataifa inayoweza kutua ndege kubwa ya aina ya *Boeing 747*. Njia hii ya kurukia na kutua ndege (*runway*) yenye urefu wa mita 3,300 ilikarabatiwa na kuongezwa kufikia kiwango hicho mwaka 1998/1999 kwa gharama ya shilingi bilioni 4.5 ni moja ya njia za ndege bora zaidi katika Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa iliyobakia ni kukiendeleza kiwanja cha Mwanza kwa kujenga maegesho na viungio yaani (*apron na tax ways*) pamoja na jengo la abiria la kukidhi kiwango hicho. Juhudi zinafanywa kupata fedha kwa ajili ya kukiimarisha na kuongeza Miundombinu pamoja na kujenga jengo jipya la abiria litakalokuwa na uwezo wa kuhudumia abiria wapatao laki tano (500,000) kwa mwaka. Mazungumzo na washirika mbalimbali yanaendelea ikiwa ni pamoja na Mashirika ya Fedha nchi rafiki na sekta binafsi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu niliyoitaja pamoja na mitandao mingine inayotakiwa Mwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kazi na Waheshimiwa Wabunge kutoka Kanda ya ziwa wamefuatilia kwa karibu sana suala hili muhimu la kuendeleza Kiwanja cha

Ndege cha Mwanza. Tunawashukuru. Serikali inawahakikishia itafanya kila linalowezekana kukiboresha kiwanja hicho ambacho ni muhimu kwa Tanzania, Afrika Mashariki na Afrika ya Kati. (*Makofi*)

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe amekiri kwamba jengo la abiria haliridhishi na maegesho pia hayapo. Je, ni lini hasa watatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria ili angalau kiwanja hiki cha Mwanza kiwe cha Kimataifa kwa kweli?

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, usanifu wa jengo la abiria, jengo la mizigo na jengo la matengenezo ya ndege yaani anga kwa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza tayari umefanyika. Umefanywa katika mwaka 2002/2003 kwa jumla ya shilingi takriban 200 milioni.

Kwa hiyo, hiyo kazi ya usanifu tayari imeshafanyika. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi tunafanya kila njia kutafuta wawekezaji ili tuweze kwa pamoja tujenge jengo lenye hadhi ya Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kwa sifa nilizozitolewa kwa maana ya *runaway* yake na vile vile Mwanza sasa ni jiji.

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya kutoa ahadi naomba nisitoe ahadi. Tunatoa ahadi ambazo tuna hakika tutazitekeleza katika kipindi cha muda mfupi na mara nyingi sisi wengine tunatoa ahadi baada ya kutekeleza.

Lakini naweza kumhakikishia Mheshimiwa Shibiliti kwamba tuna uhakika kwamba mwaka kesho tunaweza tukawa tumepata fedha za kutosha sio kutoka bajeti ya Serikali isipokuwa baada ya kuzungumza na vyombo vya fedha vya nje. Mawasiliano yako katika hali nzuri sana na sipendi kutoboa siri za mazungumzo hayo kwa sasa. (*Makofi*)

Na. 68

Mnyama Aitwaye Kakakuona

MHE. JUMANNE H. NGULI aliuliza:-

Kwa kuwa, mnyama ajulikanaye kama Kakakuona huonekana kwa nadra sana, na anapoonekana huashiria neema au balaa ya namna fulani kufuatia dalili alizoonyesha wakati huo kama vile shibe au njaa, ukame au mvua nyingi:-

(a) Je, kuna utafiti wowote uliofanyika kuthibitisha uwezo wa mnyama huyo wa kutambua neema au balaa inayokuja baadaye?

(b) Kwa kuwa, mnyama huyo huonekana kwa nadra sana. Je, ni jamii ya wanyama wachache wanaotishiwa kupotea duniani?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Nguli, Mbunge wa Singida Mjini, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Kuna aina saba za Kakakuona ulimwenguni, nne (4) kati ya hizo zinapatikana Afrika na tatu (3) Bara la Asia. Kati ya nne (4) zinazopatikana Afrika, ni aina moja tu inayopatikana Tanzania (*Cape Pangolin*). Nyinginezo tatu (3) zinapatikana Afrika Magharibi.

Miili ya wanyama hawa ina magamba magumu (*scales*) ambayo huwasaidia kujikinga na maadui kwa kujiviringisha kama mpira na kuficha kichwa na sehemu laini za mwili. Wanyama hawa hujificha kwenye mashimo saa za mchana na kutoka kutafuta chakula wakati wa usiku.

Chakula cha wanyama hawa ni siafu na mchwa na wana maumbile maalum yanayowawezesha kupata chakula hicho. Maumbile hayo ni pamoja na (i) ulimi mwembamba mrefu kwa ajili ya kushikia siafu na mchwa walioko chini ya ardhi, kwa mfano kutoka kwenye vichuguu, na (ii) kucha ndefu kwa ajili ya kuchimbia mashimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swal la Mheshimiwa Nguli, Mbunge wa Singida Mjini, lenye sehemu (a), (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na taarifa zilizopo, hakuna utafiti wa kisayansi uliowahi kufanywa kuhusu mnyama huyu mahali popote duniani, ikiwemo Tanzania, kuthibitisha madai ya kuwa Kakakuona ana uwezo wa kutambua neema au balaa itakayokuja siku za usoni. Mbali ya Kakakuona, wapo wanyama wengine ambao mara nyingi wanahuishwa na imani kama hizo kwa mfano Bundi, ambaye makabila mengi yanamhusisha na balaa (*Bird of bad omen*).

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanyama hawa imepungua kwa kiasi kikubwa kwenye sehemu nyingi ambapo wanapatikana kutokana na kuwindwa kwa ajili ya kitoweo, dawa na imani za kishirikina. *Cape Pangolin*, Kakakuona anayepatikana hapa Tanzania yuko kwenye orodha ya wanyama walio kwenye hatari ya kutuweka duniani (*Near-threatened Species*) ya IUCN-CITES Red List ya 2000. Hata hivyo, mtandao wa hifadhi (*Protected Areas Network*) Tanzania unatoa mwanga kwa mnyama huyu kuendelea kuwepo nchini bila hatari ya kutuweka.

MHE. JUMANNE H. NGULI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal la nyongeza.

Kwanza naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameshayatoa. Pamoja na majibu mazuri hayo naomba kuuliza suala moja au mawili ya nyongeza.

Je, kwa sababu utafiti wowote haujafanyika juu ya mnyama huyu anayeashiria aidha balaa au lolote lile ambalo linaweza likatokea na kwa sababu mnyama huyu sasa hivi anapatikana kwa taabu sana katika maeneo machache ya Tanzania ikiwepo na maeneo ya Singida. Je, Serikali iko tayari kufanya utafiti juu ya huyu mnyama hasa kujua kama uwezekano upo wa kutambua matatizo au neema ya masuala hayo?

Pili, je, kwa kuwa mnyama huyu hupatikana pamoja na Singida katika kufanya utafiti huo. Je, Serikali inaweza ikaufanya utafiti huo Singida hasa katika hifadhi ya pori la Mgori ambayo mnyama huyo anapatikana? (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, mara nyingi sana unapofanya utafiti unataka kujua kitu fulani na kitu hicho kiwe muhimu kwa kweli kwa jamii na Taifa kwa ujumla wake. Kama nilivyosema kwamba mnyama huyu kama vile bundi ni mnyama ambaye anahusishwa na mambo mara nyiningine ya kishirikina lakini ni mambo ambayo siyo ya kisayansi. Kwa kweli kwa hivi sasa Serikali haitakuwa tayari kufanya utafiti wa suala hilo, lakini pia nielezee kwamba mtandao wa Tanzania na ndiyo maana nikasema kwamba kwa upande wa Tanzania mnyama huyo hayupo katika hatari ya kutoweka. Mtandao wa maeneo ya hifadhi kwa Tanzania yaani *protected areas* ni kama asilimia 25. Kwa hivyo wanyama hao kwa kweli kwa Tanzania hawako katika hatari ya kutuweka.

Na. 69

Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Mese

MHE. AGGREY D. J. MWANRI aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu wananchi wa Kijiji cha Mese Jimboni Siha wameshirikiana na *TANAPA* kuititia *KINAPA* katika kuhifadhi msitu wa asili uliopo katika Kijiji hicho na kuzuia uharibifu wa adha yoyote ile usifanyike katika msitu huo:-

Je, Wizara ya Maliasili na Utalii ina mpango gani wa kusaidia wananchi wa Kijiji hicho kuvuta umeme kutoka Kijiji cha jirani cha Ngaronyi ambacho kina umeme ili wananchi wasije wakashawishika kuvamia msitu huo wa asili kwa ajili ya Nishati?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, napenda kwanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) lina utaratibu wa ushirikiano wa Vijiji viliyvo jirani na Hifadhi unaofanyika kwa kufuata mpango wake wa

Ujirani Mwema. Chini ya utaratibu huu, kwa kutambua mchango wa wananchi wa Vijiji vilivyo jirani na Hifadhi katika kuhifadhi na kuzilinda Hifadhi hizo, *TANAPA* huchangia katika miradi ya maendeleo ya Vijiji hivyo kama vile ujenzi wa shule, zahanati, barabara na mengineyo ambayo Vijiji vinaipa kipaumbele kwa kuzingatia uwezo wa *TANAPA* na Vijiji husika wa kugharamia miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuitia kwa Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha niwashukuru wananchi wa Kijiji cha Mese kwa mchango wao katika uhifadhi wa sehemu ya Msitu wa Hifadhi wa Mlima Kilimanjaro iliyo jirani nacho. Nawaomba kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge waendelee na moyo huo.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Mese kina ushirikiano wa muda mrefu wa Ujirani Mwema na *KINAPA*. Chini ya ushirikiano huu, Kijiji hiki kilisaidiwa na *TANAPA* na Halmashauri ya Wilaya ya Hai kujenga daraja katika Mto Kisaisa ili kurahisisha mawasiliano.

Daraja hilo liligharimu shilingi 7,872,075/= na kufunguliwa Desemba 2003 lina urefu wa kukata mto wa mita 5 na upande wa mita 4. Mchango wa *TANAPA* katika ujenzi wa daraja hilo ulikuwa shilingi 7,087,575/= na Kijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Hai waliochangia shilingi 784,500=

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la Wizara ya Maliasili na Utalii kuwasaidia wananchi wa Kijiji cha Mese kuvuta umeme kutoka Kijiji cha Ngaronyi linaweza kufanyika chini ya utaratibu wa ujirani mwema uliopo kwa kuzingatia:-

Kipaumbele wananchi wanachoupa mradi huo;

Gharama za mradi; na

Uwezo wa *TANAPA*, Halmashauri ya Wilaya ya Hai na wanakijiji wa Mese wa kuchangia katika utekelezaji wa mradi.

MHE. AGGREY D.J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, kumshukuru sana sana Mheshimiwa Zakia Meghji kwa msaada mkubwa ambao tumekuwa tunapatiwa. (*Makofî*)

Sisi wananchi wa Jimbo la Siha tuko tayari kufuata maelekezo aliyoyatoa hapa na ningependa kujua kwamba kwa vile nilishazungumza na wananchi wa kijiji cha Mese na nilishazungumza pia na Wizara na imeonyesha wote kwa pamoja tuko tayari kuchangia katika jambo hili la kuingiza umeme pale. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba tukutane mapema kabla ya mwezi Oktoba ili tuweze kuona nini kinachowezza kufanyika? (*Kicheko/Makofî*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, sawa kabisa tutatakutana kwa mazungumzo. (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamemalizika. Sasa ni matangazo ya vikao. Kwanza ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake ananiomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 15/6/2005 kitafanyika kikao cha Kamati saa tano asubuhi katika chumba Na.231, jengo la utawala.

Vikao vya Wabunge katika vyama vyao vya siasa, *Chief Whip* wa Kambi ya Upinzani ananiomba niwatangazie Wabunge wa Kambi hiyo ya Upinzani kwamba kutakuwa na kikao leo, alisema saa saba lakini kwa maelezo yangu ya mapema tutaahirisha Bunge kabla ya saa saba kwa hiyo niseme mara baada ya kuahirisha Bunge katika Ofisi za Upinzani, jengo la utawala. (*Makofi*)

Chief Whip wa Kambi ya Chama Tawala, naye anawatangazia Wabunge wa CCM wakutane humu ndani mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge asubuhi hii. (*Makofi*)

Tangazo la mwisho, nakumbusha ujio wa mgeni wa Waziri wa Uingereza, Lord David Traceman ambaye atakuja kutuhutubia leo majira ya tisa na nusu mpaka saa kumi na nusu katika mazingira ya semina. Baada ya hapo, tutaendelea na Bunge kama kawaida. (*Makofi*)

Mwisho wa matangazo, Katibu endelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2004, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2005/2006 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006)

(*Majadiliano yanaendelea*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono kwa 100% bajeti hii.

Bajeti hii ni tegemezi kutokana na nguvu ya wahisani. Hivyo huenda miundo mbinu kama vile barabara hazitatengenezwa kikamilifu. Bajeti haina mwelekeo kwa Kanda ya Magharibi kama vile barabara, umeme huko Mkoani Kigoma. Miradi midogo midogo haina maana yoyote kwa sasa. Reli bado ni muhimu kwa nchi hii na pengine inaweza kuzalisha mali ya kutosha kuliko hata barabara.

Wanafunzi wa Chuo Kikuu au Vyuo vikuu wanazidi kusahaulika. Hii ni kwa sababu bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu inaonyesha kuwa ni wanafunzi 11,000 kati ya 28,000 watakaochaguliwa na kwamba uwezo wa Serikali ni 11,000 tu. Hata nusu ya 28,000 hakuna.

Tatizo hili ni muhimu kutatuliwa ili wanafunzi wengi waweze kujiunga na elimu ya chuo kikuu. Pesa iongezwe haraka sana ili wanafunzi hao wenye sifa waende *University*.

(i) Hao ni watoto wengi na ambao wazazi wao ni maskini wasiposoma ni kuuwa Taifa.

(ii) Umeme, barabara ya kwenda Kigoma hautapatikana na Serikali ya Tanzania inaonekana kushindwa kwa hilo.

(iii) *VAT* ya mazao iliondolewa tangu bajeti ya mwaka 2004. Ninaomba wakulima wa zao la kahawa Mkoani Kigoma warudishiwe pesa zao. Ahsante.

MHE. LEPHY B. GEMBE: Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe pongezi kwa Mawaziri wote wawili, kwa kazi nzuri waliozofanya katika kipindi chao wakiwa wanaongoza Wizara zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ndiyo mojawapo ya nguzo kuu ya kuleta maendeleo, naamini kuwa Serikali katika kipindi hiki imefanya mambo makubwa ambayo kwayo yametokana na mipango mizuri, vile vile ugawaji mzuri wa fedha na kuzisimamia fedha hizo kufanya kazi zilizolengwa kufanywa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumezungumza mengi kwenye Kamati, ningombaa Wizara zizingatie yale yote ambayo Kamati ya Fedha na Uchumi tumeshauri, hasa mambo haya yafuatayo. Yale yote ambayo yameelekezwa katika sera za mapato.

Kuimarisha Idara ya Walipa Kodi wakubwa. Kuuza hisa kwa Watanzania wenyewe. Ufutiliaji na usimamizi wa fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kuwashukuru Mawaziri na Watendaji wao wote kwa kazi nzuri, ni imani yangu kuwa wakiendelea na mwenendo huu – nguvu mpya, ari mpya na kasi kubwa tutafanikiwa kufikia malengo yetu ya kuwaondoa wananchi wetu katika hali duni ya maisha walijonayo na kuwafikisha katika hali ya maisha bora zaidi. Ahsante.

MHE. FATMA SAID ALI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mramba, Manaibu wawili na Makatibu Wakuu wawili wa Wizara ya Fedha. Naunga mkono hoja hii.

Katika mgao wa fedha wa Bajeti hii asilimia zaidi ya 50 ya Bajeti imetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa MKUKUTA. Je, kwa nini bajeti hii haijaongeza asilimia kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar badala ya 4.5 ya miaka ya nyuma? Kwani Zanzibar inahitaji misaada ya fedha zaidi kwani umaskini umezidi kuliko Tanzania Bara, tumeangalia takwimu.

Pia bajeti hii imetenga fedha kwa ajili ya uamuzi wa kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo. Naipongeza Serikali kwa hili. Swali langu jee, Serilai itawasaidiaje wanafunzi walioko *Secondary school* huko Zanzibar ili idadi iongezeke kuingia vyuo vya juu. Zanzibar haina mpango wa MMES na ndio maana hata kufaulu kwa kidato cha sita kuna tofauti kubwa baina ya Bara na Visiwani.

Lumumba Secondary School iliyopo Jimbo la Mlandege, haina vifaa vya *Laboratory*, hata *fence* haina. Vipi tutaweza kufanya vizuri mitihani ili kufaulu na kusaaidia kunyanya uchumi wa Zanzibar?

Naomba fedha zitakazopelekwa Halmashauri za Wilaya zote kwa ajili ya Watendaji kusimamia MKUKUTA. Naomba maandalizi yatayokuwepo yasisahau kabisa kuwaandaa watendaji wanawake kwani naamini watakuwa watendaji wazuri kutokana kwamba wanaelewa vizuri – umaskini vijijini.

Tunapongeza programu za *TASAF* ili kusaidia kuondosha umaskini. Naomba *TASAF II* itimize mihadi yake ya kujenga soko la Makadara na Shule ya Gulioni kama ilivyoahidi. Ile beki ya Wanawake ipo kwenye hatua gani? Wanawake tumechoka na mikopo midogo midogo ya *SIDO*, mfuko wa wanawake, *pride* na kadhalika. Wanawake tunataka tushiriki zaidi kwenye uchumi.

MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti.

Naomba Serikali itoe msamaha wa kodi ya *VAT* kwa spea za meli na vifaa vinginevyo.

Msamaha huu utasaidia sana kurahisisha usafiri katika maziwa na bahari ya Hindi. SMT kutenga asilimia 4.5 ya msaada kwa SMZ.

Napendekeza Serikali ifikirie kuweka kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 4.5 kwa sababu kiwango hiki kimepitwa na wakati. Muungano SMT, ishirikiane kwa ukamilifu na SMZ katika kuangalia njia za kukuza uchumi wa Zanzibar hasa kwa sababu Tanzania inakusudia kuelekea katika ushirikiano wa Afrika ya Mashariki. Ili kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unaboreka.

Naomba pia viwango vya kodi kibiashara kwa Zanzibar ni vyema viangaliwe.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya kuondoa kodi kwa mishahara ya kima cha chini, lakini bado mishahara

yenewe ni midogo. Ingesaidia zaidi kama pamoja na kuondoshwa kodi na hiyo mishahara ingepandishwa kufikia elfu themanini kwa mwezi.

Makusanyo ni makubwa lakini bado usumbufu upo bandari ya Dar es Salaam. Gari ikipitishwa Mombasa baadae Holili huchukua siku tano tu. Lakini Dar es Salaam ni zaidi ya wiki tatu Hali hi inaashiria kuwa upo mpango mbaya pale bandarini Dar es Salaam ama ni mazingira ya rushwa au kiburi cha watendaji. Kurekebisha hili linawezekana bora lifanywe na usumbufu uondoke. Doa moja jeusi huharibu shuka nzima nyeupe!!

Bei za mafuta bado hazina udhibiti mzuri ni vyema uangalifu mkubwa ukawekwa ili kupunguza usumbufu kwa watumiaji hasa wa vijiji.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji bado inaonekana hapana uwazi wa kutosha katika suala zima la uwekezaji na hata ufuatiliaji wenewe *royalty* ndogo. Wananchi hawafaidiki na miradi iliyowekezwa kwa kiwango kikubwa. Hasara hii ni yetu sote na inatumiza.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niwapongeze Mawaziri wote wawili, Manaibu wake, Makatibu Wakuu na Watumishi chini ya Wizara na Mashirika yake kwa bajeti nzuri yenye mwelekeo wa kuntuonda kwenye lindi la umaskini. Nimpongeze kwa dhati Rais wetu Benjamin William Mkapa kwa heshima aliyotujengea Watanzania katika sura ya Afrika na dunia nzima kwa kufufua uchumi na kusababisha nchi yetu kufutiwa madeni yote. Hongera sana. Hakuna kitu ambacho hata baba wa Taifa amefurahia kokote kule aliko kama kufutiwa madeni. Naunga hoja kwa asilimia zote mia moja.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuondoa umaskini, njia mojawapo ni kuandaa mazingira ya kuondoa umaskini. Mkulima mahali popote alipo, anahitaji, barabara, masoko, pembejeo na utaalamu. Hatuwezi kupunguza umaskini Mkoani Rukwa barabara ya kutoka Tunduma – hadi Sumbawanga na kutoka Sumbawanga hadi Kasesya (mpaka na Zambia) na kutoka Sumbawanga hadi Kasanga – Ziwa Tanganyika linalopakana na nchi za Rwanda, Burundi na *DRC* bila ya kuziwekea lami barabara hizi. Sasa ni zaidi ya miaka 20 tunalizingumzia suala hili. Je, nini mpango thabiti ya Serikali kuhusiana na suala hili? Namwomba Mheshimiwa Waziri awaeleze wananchi wa Rukwa kwa nini wameendelea kuzalisha chakula kingi bila ya kupewa motisha hiyo?

Mheshimiwa Spika, masoko ya Mkoa wetu yako nchi jirani. Lazima miundo mbinu hiyo ipewe kipaumbele!!

Mheshimiwa Spika, mapema mwaka huu niliwasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu kulundikana kwa mahindi katika maghala ya *SGR* na kwamba yanatakiwa yasafirishwe nje ya mkoa. Alinijulisha kuwa fedha za kuhamisha mazao hayo zimekwisha tengwa. Lakini leo ni mwezi wa sita sijaona hata tani moja ikisombwa au kuondolewa toka maghala ya *SGR* wakati msimu nao unakaribia wa mavuno mapya. Je,

Waziri ataaeleza nini kuhusu hali hii wakati mikoa yote ya kati ina upungufu mkubwa wa chakula mwaka huu!!

Mheshimiwa Spika, suala la upatikanaji wa pembejeo za uhakika, ni silaha kubwa ya maendeleo ya kilimo. Bado kazi kubwa ya kuzileta mbolea lkwa wakati muafaka hazijazaa matunda. Je, Serikali kwa nini inachelewesha kuwapatia fedha waagizaji wa pembejeo hizo (*TFC*) ili wawe wanawahi msimu wenyewe wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana niliomba nipatiwe *guarantee* ya Serilai ili niingize mbolea kwa bei chini ya shs.10,000 kwa mfuko wa *UREA* kutoka nje. Lakini masharti yakawa magumu kupatiwa *guarantee* hiyo!! Je Mheshimiwa Waziri atanielezea vigezo vipi vinatumika kwa mtu kupata *guarantee* hiyo ya Serikali na bemki ili nasi tuiombe kama wengine walivyo fanikiwa!!

Mheshimiwa Spika, hivi Tanzania imefanikiwa kwa kiasi gani malengo ya Milenia 2005 na hatua zipi zitumike hasa baada ya kusamehewa madeni yetu yote kama ilivyotangazwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, moja ya matarajio, malengo na mategemeo ya MKUKUTA ni kuongeza usawa wa mikoa katika ukuaji wa uchumi. Je, hatua zipi za makusudi zimeandaliwa ili kuhakikisha tofauti hizi zinapungua katika kipindi hiki cha awamu ya nne ya uongozi wetu. Nini wajibu wa mikoa husika na nini wajibu wa Serikali Kuu ili kila upande upate majukumu yake!!

Mheshimiwa Spika, mkizingatia hotuba ya msemaji mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na hoja alizozitoa kwa Wizara hizi. Naelewa hoja zake zote zina majibu kamilifu pamoja na kwamba nyingine zinaendelea kuchunguzwa na kuchukuliwa hatua pale inapobidi. Lakini ningeshauri Mheshimiwa Waziri asichakue jukumu la kuanza kujibu moja hadi nyingine kwa sababu Wizara zinazohusika zitabebe mzigo wa kuzijibu vizuri na kwa undani zaidi wakati hoja za Wizara zao zitakapohijiwa.

Mheshimiwa Spika, hu ni ushauri wangu ili tusifumue majadiliano wakati usio muafaka. Naunga hoja mkono.

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Spika, awali yote napenda kuwapongeza kwa moyo wa dhati Waheshimiwa Mawaziri, Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha na Dr. Abdallah O. Kigoda, Waziri wa Mipango na Ubinafishajji, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara na Wataalam wote kwa kuandaa hotuba ya bajeti ya Wizara zao. Hotuba za bajeti zimetoea dira, muelekeo na mikakati ya kuendeleza, kulinda na kutetea mafanikio na mapinduzi ya uchumi endelevu yaliyopatikana chini ya Serikali ya CCM kwa kipindi cha miaka kumi.

Baada ya pongezi zangu napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Fedha za MKUKUTA zitatoa mafanikio na *impact* kubwa, iwapo mpango Kata utahimizwa kama kitovu na chachu cha kukomboa wananchi. Naomba Wizara ya Mipango iandae mikakati ya kuanzishwa kwa mpango kata. Naunga mkono hoja.

MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti kwa asilimia kwa mia na ipite bila kupingwa.

Hata hivyo, nina maeneo yafuatayo ya kuchangia:-

Nimefurahi kutoza mvinyo kodi ya asilimia 25 ili kulinda viwanda vyetu vinavyoibuka hasa kile cha Hombolo ambacho Mheshimiwa Rais wetu atakifungua tarehe 26 Julai, 2005.

Suala la kutoza kodi mafuta ya dizeli, naomba lifikiriwe tena. Punguzo la kodi ya dizeli lingesaidia sana kuzifanya ada za kukodisha kulimia mashamba iwe ahueni. Aidha gharama za uchukuzi wa mazao toka mashambani iwe ahueni. Kwa sasa gharama za matumizi ya matrekta na *ma-bus*, na malori hazina unafuu.

Tengo la kuendeleza *Irrigation* nchini bado hazitoshi. Nchini zipo Ha 29 milioni zinazofaa kwa *irrigation*, lakini hadi leo hii tumetenga na kutumia Ha 27,000 tu ambacho kieneo ni kidogo mno, angalau tungekuwa tumefikia milioni moja hivi. Kufikia eneo hilo kikwazo ni fedha/*budget*. Je upo uwezekano kuliangalia hilo pia?

Hire Tractor Service, huduma za matrekta ya kukodisha mikoani ingelisa sana kuongeza eneo linalolimwa na hasa kuwavutia vijana kijijini kwenye kilimo. Pendekeso ni kuwa na mfuko wa pembejeo uongezewe uwezo ili bei za matrekta ipunguzwe kwa asilimia hamsini (50%). Au uanzishwe mfuko maalum kutokana na *budget* yenewe kama ilivyo kwa Wizara ya Ujenzi. Pawe na tengo maalum la kilimo. Kuwepo kwa matrekta kwa wingi na vifaa vyake pamoja na zana zingine zikipunguzwa bei itasaidia kuwavutia vijana kujajiri kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote za Wizara zote mbili kwa asilimia kwa mia!

MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, mia kwa mia. Bajeti ya 2005/2006 itasaidia sana kuongeza kasi ya kukuza uchumi na kupambana na umaskini.

Aidha, napongeza kwa kuondoa *VAT* kwenye *spare* za gari moshi na vifaa vinginevyo. Uamzi huu ni vizuri uboreshwe kwa kuondoa *VAT* kwenye *spare* za meli na vifaa vinginevyo. Ikumbukwe kwamba huduma za meli zinaungana na za gari moshi. Mizigo inayoshuka kwenye meli hupakiwa kwenye gari moshi na inayopakuliwa kwenye meli hupakiwa kwenye gari moshi.

Vile vile watumiaji wa meli ni wananchi wa kipato cha chini. Kwa kuwa tumezunguza kodi kwenye mafuta ya ndege, si vibaya kupunguza kodi zinazohusiana na usafiri wa majini.

Takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba Shirika la Meli za Maziwa linatumia fedha nyingi kununua *spare* na *VAT* inakuwa mzigoto mkubwa kwa shirika hilo. Aidha, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwa nini *TRA* hairejeshi fedha za *VAT* ambazo wakulima wa kahawa hulipa katika vifungashio, magunia, gharama za kukoboa na kusafirisha na utunzaji wa kahawa kwenye maghala. Ikumbukwe kwamba Serikali ya Bunge tulishakubali kutoendelea kukata *VAT* kwenye zao la kahawa.

MHE. OMAR S. KWAANGW’: Mheshimiwa Spika, tafadhalii rejea mchango wangu kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara ya kuunganisha Mkoa wa Manyara (Babati –Kiteto/Simanjiro) kwamba hajapewa umuhimu unaostahili kwenye bajeti hii na kwamba kwa staili ya utengaji wa fedha kwa barabara hii ni kuufanya Mkoa wa mpya wa Manyara uonekane hauna maana kwani kwa ssa tayari wapo watu wanaoanza kusema kuwa ni heri Mkoa huo uvunjwe na Wilaya za Kiteto/Simanjiro zirudi Arusha. Hii ni kampeni mbaya sana kwa ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Katika matumizi ya kawaida – deni la Taifa limetengewa Shilingi milioni 528,144 na kwa dhana ya msamaha uliotangazwa rasmi sasa, ipo nafasi ya kuusaidia Mkoa huo kwa eneo hilo. *RCC* ya Manyara iliomba shilingi biliioni 9 kwa ajili ya barabara hiyo. Hata hivyo tulisema Serikali ikiamua kuufanya mradi huu kuwa maalum na ikatenga walau bilioni 4 mwaka huu basi mawasiliano yangefunguka. Nashauri sasa nafasi ya kufutiwa madeni itumike. Mwisho bado azma yangu ya kutounga mkono kikamilifu bajeti hii ipo pale pale na kama nilivyoomba tuwasiliane ili kuona nitasaidiwa vipi. Kazi njema.

MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR: Mheshimiwa Spika, na mimi naungana na wenzangu kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango. Lakini kabla sijaanza kuchangia kwanza sina budi na mimi kutoa mkono wa rambi rambi kutokana na vifo vilivyotokea vya marehemu Wabunge walifariki hivi karibuni. Waheshimiwa wenyewe ni marehemu Hassan Diria na Marehemu Abu Kiwanga. Mungu aziweke roho za marehemu hawa mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo sasa naanza kuchangia hotuba hizi kwa kutoa pongezi kwa Mawaziri hawa. Hotuba hizi za bajeti hazina kasoro isipokuwa zinataka utekelezaji tu.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii kutokana na kutenga asilimia 4.5 ya misaada ya bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa Serikali ya Mapinduzi nayo mambo yake yatakwenda vizuri maana pesa hizi zimepatikana wakati muafaka. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itatatua matatizo yake kama ilivyopanga na shughuli za maendeleo zitakwenda kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa wagonjwa walioathirika kwa UKIMWI Serikali imewakumbuyka kwa kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa madawa ya kusaidia kurefusha maisha kwa waathirika hao. Vile vile fedha hizo hizo zitatumika kwa ununuzi wa madawa ya malaria na kifua kikuu.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii ya 2005/2006 pia Serikali imetenga fedha za malipo ya mafao ya waliokuwa watumishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kitendo kizuri kwa kuwakumbuka wazee wetu hawa. Lakini ikumbukwe kuwa tokea wastaifu waache kazi ni muda mrefu sana. Thamani ya fedha yetu imebadilika sana tokea wakati walipostaaifu. Sasa jambo hili lingeangaliwa lisije likaleta mzozo mwingine. Maana Serikali imelifanya jambo hili kwa nia nzuri. Lakini likaja kuwa kinyume chake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala hili hili la fedha, wastaifu walioichukua pensheni yao kwa mkupuo. Katika bajeti ya 2004/2005 Serikali ilikubali kuwalipa wastaifu. Lakini pametokea tatzilo la kutowalipoa kwa wakati. Usumbuu umekuwa mkubwa. Suala hili Serikali ingeliangalia na kulipatia ufumbuzi wa kulitattua.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la faraja sana kwa Serikali kutenga zaidi ya asilimia 50 ya bajeti ya mwaka 2005/2006 kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele kwa MKUKUTA kwa kutekelezwa na kila Wizara.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kila Wizara kutekeleza na huduma hii ya MKUKUTA kuwfafikishia walengwa ambao vijijini ndiko waliko wengi maana vijijini ndiko kunako umaskini wa kila aina.

Mheshimiwa Spika, na mimi naunga mkono hoja za Wizara zote mbili mia kwa mia.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze mchango kwa kumpongeza Mheshimiwa Benjamine William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein – Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri waliofanya ya kusimamia maendeleo katika nchi wakishirikiana askari wao wa miavuli katika kuwaletea maendeleo Watanzania. Aidha, nichukue nafasi kuwapongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa kuteuliwa kwao na Chama Cha Mapinduzi kuwa wagombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hizi mbili walioshiriki kuandaa mpango wa bajeti hizi kwa kazi nzuri na kuridhisha waliofanya.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwani bajeti hii ina mjali mananchi wa kawaida ambaye ndiye mlengwa wa mipango mbalimbali ya Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwanza kwa kuipongeza *TRA* kwa kazi nzuri ya ukusanyaji mapato ambayo yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka na kuiwezesha Serikali yetu kutekeleza mipango yake mbalimbali iliyojiwekea kwa ajili ya kuwashudumia wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, vile vile niipongeze Serikali kwa kuboresha elimu ya msingi kupidia mpango wake wa MMEM, sasa tuna hamia kwenye mpango wa MMES kwa ajili ya kuboresha elimu ya sekondari, naiomba Serikali isimamie vizuri mpango huu kama ilivyosimamia mpango wa MMEM kwa kuhakikisha nguvu za wananchi zinaungwa mkono ikiwa ni pamoja na matumizi ya fedha kuwekwa wazi kwa wananchi ili kuondokana na mianya ya ulaji wa fedha hizo ili kufikia azma ya Serikali ya kuwa na shule ya sekondari kila Kata.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Serikali kwa kuunda Tume ya Kuhakiki Madai mbalimbali ya walimu, ikiwemo mishahara, posho za safari, matibabu, uhamisho na kadhalika jambo ambalo limekuwa ukombozi kwa walimu wa shule za msingi inasikitisha kwamba zoezi hili halikuwashirikisha vilivyo walimu wa shule za sekondari na vyuo, kazi ambayo haijaleta matunda mazuri kwao, naomba Serikali itafute muda wa ziada kuhakikisha kwamba madeni ya walimu wa sekondari na vyuo yamehakikiwa upya kwa kuwashirikisha wahusika. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewaongezea walimu ari ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji, naishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ambacho ni ukombozi kwa wakulima, kwani mvua za siku hizi hazitabiriki. Vile vile, naipongeza Serikali kwa kusaidia na kutoa fedha, kwa ajili ya kujengea mabwawa ambayo yamesaidia sana kunyweshea mifugo. Matumizi ya nyumbani na kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji mfano:-

Wilaya ya Manyoni, Tarafa ya Kilimatinde, Kintinku, Konko na kadhalika. Wilaya ya Singida vijiji tarafa ya Sepuka, Kata ya Mgungiza na kadhalika bila kusahau mabwawa ya Iramba Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Singida, una mabonde mengi yanayo kusanya maji, ikiwemo na mito, naiomba Serikali ikumbuke kutoa fedha kwa ajili ya Mkoa wa Singida kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hasa Tarafa ya Shelui.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida unalima pamba, alizeti, ufuta, dengu, vitunguu na kadhalika. Lakini mazao hayo hayana soko tunaiomba Serikali ihakikishe inawatafutia soko wakulima ili wafaidike na mazao pia ili waongeze ari ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara, naiponeza Serikali kwamba barabara kuu zote zinazopita mkoani Singida zina wafadhili na zinajengwa kwa kiwango cha lami. Lakini mkandarasi wa barabara ya Manyoni – Singida (*SIETCO*) ana sua sua. Naomba Serikali ilitazame upya, kama ameshindwa kazi hiyo basi apewe mtu mwingine (Mkandarasi mwingine).

Mheshimiwa Spika, mwisho niishukuru sana Serikali kwa kukubali kuibadilisha Halmashauri ya Mji wa Singida na kuwa Halmashauri ya Manispaa kuanzia tarehe 1 Julai, 2005. Naiomba Serikali iwahamasishe wawekezaji waje kuwekeza biashara mbalimbali kwani vivutio vingi viro mfano:- Ardhi, misitu, maziwa, wanyama na mawe yaliopandana kwa madaha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia 100% mia moja.

MHE. SHAMIM P. KHAN: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wenzangu kwa kazi nzuri wanaofanya katika suala zima la kuandoa umaskini, hongereni.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuwapongeza watendaji wote akiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na kadhalika. Haja ni matokeo ya *team work*. *Budget* hii ni nzuri na mtambuka kwani imewagusa wote bila ya kujali tajiri na wasiyo tajiri. Kupunguza utegemezi hadi kufikia 41% *is not a joke*. *Gender budgeting* nadhani tulifanya uamuvi wa busara kwamba tunatazama miradi yote kwa kuwa *gender lens*. Bado idadi ya wanawake katika maeneo mengi ni ndogo sana. Kuna haja ya kuongeza nafasi za wanawake.

Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba bado wanawake tunahitajika kusoma lakini pia ni kweli kwamba kati ya hao tuliyosoma tuwe tunatazamwa mfano *RC* wawili hatutoshi kabisa. Hii haina maana kwamba hawapo wanawake ambao wanaweza kushika nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Elimu kwa kuhakikisha kwamba takwimu zilizotolewa ni *disaggregated* kwani mahitaji ya wanawake na wanaume au mvulana na msichana ni tofauti katika baadhi ya maeneo. Wizara ya Afya inajitahidi. Wizara zilizobaki zifanye hivyo, maana *international fora* huwa wanadai takwimu hizo (Me na Ke).

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake, Ninashukuru uamuvi wa kuanzisha Benki hiyo imetolewa na kwamba Wizara ya Fedha ikishirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Ushirika na Masoko zimepewa jukumu hilo. Nashauri suala hili lipewe *priority* katika Serikali ya awamu ya nne ili wanawake nao waweze kufaidika kimatendo na si kinadharia. Pamoja na hilo, kuna haja ya kuanzisha *Community Banks* katika maeneo yetu. Sisi wa Morogoro tuna-*finalize* mchakato wa kuanzisha *Morogoro community bank* ingawaje tumechelewa, lakini nia ipo na mchango unaendelea kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili bila ya kutetereka. Hongereni kwa kuendelea kutimiza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambayo ni dira yetu.

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza watoa hoja kwa pamoja, Waheshimiwa Mawaziri Basili Mramba na Dr. Abdallah Kigoda kwa kuleta mapendekezo ya kina na yenye mwelekeo wa kukuza

uchumi na kuondoa umaskini nchini Tanzania. Nawapongea pia Manaibu Waziri Mheshimiwa Dr. Festus Limbu na Abdisalaam Khatibu, pamoja na watendaji waandamizi hususan Ndugu Grey Mgonja, Katibu Mkuu Mwandamizi na Ndugu Pheniel Lyimo katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki bila kuchoka kufanikisha maandalizi haya ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naona nidhahiri kabisa Bajeti hii ni mwendelezo wa Bajeti za 2001/2002, 2003/2004, 2004/2005. Ni matumaini yangu kwamba awamu ya nne ya Serikali itakayoingia madarakani ifikapo Novemba, 2005, itaenzi na kukubali kuwa mafanikio yanayoanza kujitokeza katika kukuza uchumi wetu ni matokeo ya ubunifu, udhubutu, umakini na nidhamu ya hali ya juu katika utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tatu. Kilichofanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni historia ya mafanikio.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yatageuka kuwa sumu ya maendeleo endelevu pindi tutakapo bweteka na mafanikio hayo. Sharti sasa mikakati iandaliwe siyo tu kwa kulinda mafanikio lakini pia kukubali kujitathimini upya, kwa kuzingatia kuwa kila mara kuna namna bora zaidi ya kutenda mambo yetu. Kabla sijaanza kuchangia hoja kwa lengo la kuboresha napenda kusema naunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji umeleta tija kwa mtizamo mfupi, lakini kwa mwelekeo wa muda mrefu unaweza ukawa ni tatizo. Kwa mfano iliyokuwa Benki ya Taifa (*NBC*) ili kuwa ni Benki ambayo haikuwa na matawi nje ya mipaka ya Tanzania, ndio kwa sababu ilikufa kifo cha asili. Sina uhakika, kama *NBC 1997 Limited* inaweza kufungua matawi nje ya Tanzania, kama Kenya, Uganda, Zambia na Afrika Kusini na hata Uingereza. Katika ulimwengu huu wa utandawazi nchi itakufa kiuchumi ikiwa kama hutuwekeza nje ya mipaka yetu. Nashauri sheria zetu zifanyiwe marekebisho ili Makampuni yanayowekeza hapa kwetu pamoja na Mashirika yetu ya umma hususan Shirika la Nyumba la Taifa kupanua shughuli zake nje ya mipaka yetu. Ninaamini kama Mashirika yetu yangekuwa yamewekeza nje ya mipaka yetu, leo tungekuwa tunavuna.

Mheshimiwa Spika, mipango yetu sharti izingatie usalama na ulinzi wa nchi yetu, sharti tukubali kuwa usalama wa nchi ni uchumi. Mipango ya uwekezaji hasa Miundo mbinu ya mawasiliano budi izingatie nafasi yetu kijiografia. Tanzania itanufaika zaidi kwa kujenga mahusiano ya kiuchumi na kijamii na Jamhuri ya Kongo (*DRC*) kuliko Kenya na Uganda. Kwa mtizamo huo kujenga reli na barabara ya lami kuunganisha bandari ya Kasanga ziwa Tanganyika na Tunduma (Reli ya *Tazara*) nchi itanufaika zaidi kuliko kujenga reli kutoka Manyoni hadi Singida. Reli ya Manyoni Singida ni uwekezaji wa kisiasa ambao hautakuwa na manufaa ya kiuchumi. Miradi ya aina hii inatakiwa isiwe sehemu ya vipaumbele katika mipango ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato umeonyesha mafanikio makubwa, lakini hali hiyo bado haitoshelezi kwa sababu mipaka ya nchi yetu ni uchi (*porous*) ni jambo la ajabu kuona kuwa mpaka wetu na Msumbiji hakuna vituo vyta ushuru na Forodha (*TRA*) kituo ambacho unaweza kusema kipo karibu na mpaka Kilambo Mtwara

Vijijini ambacho ujenzi wake unaanza – biashara inavyofanyika kwenye mpaka huo wenyе zaidi ya urefu wa kilomita 800 ni kubwa lakini Serikali bado haijagundua. Nashauri Serikali inaangalia kwa undani ukusanyaji wa mapato kwa kuanzisha vituo vya TRA mipakani. Hakuna anayefahamu thamani ya mazao ya misitu ya asili yanayovunwa na kutumiwa hapa nchini na kusafirisha nje, lakini mapato yanayoingizwa kwenye mfuko wa Serikali yanaashiria jinsi eneo hilo lilivyo na ulegevu mkubwa siyo tu kukusanya mapato hata katika kusimamia matumizi endelevu ya maliasili ya misitu. Hali inayojionyesha katika nchi hii ni sawa sawa na kutoboa mtumbwi ukiwa baharini kwa lengo la kupata kuni ili upike chakula cha siku moja. Hatima yake ni kuliangamiza taifa.

Mheshimiwa Spika, hewa ya *oxygen* ni misitu, maji ya uhakika yanatokana na misitu, chakula ni mazao ya kilimo ni maji, umeme ni maji, kwa hiyo uchumi wetu wote ni maji ambayo yanatokana na misitu. Mheshimiwa Waziri nawaomba mchukulie udhibiti wa Makusanyo ya sekta ya misitu kuwa njia ya kunusuru ulimwengu.

MHE. MARGERETH J. BWANA: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mawaziri wote Waziri wa Fedha na Waziri na Mipango na Ubinafsishaji, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na wataalam mbalimbali kwa maandalizi mazuri ya *budget* hii. Ninapenda kutamka wazi kuwa ninaiunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Katika kuchangia hoja hii ninapenda kuchangia katika hotuba hii kwa lengo la kuboresha katika maeneo yafuatayo; kwanza suala la wastaifu wa Afrika Mashariki. Katika kufuatilia hotuba hiyo imeandikwa kuwa Serikali itawalipa wastaifu hao kwa thamani ya dola ya mwaka 1977 wakati huo dola ilikuwa na thamani. Lakini kitendo cha Serikali kuwalipa mwaka 2005 kwa thamani ya dola ya mwaka 1977 ni kuwaonea wastaifu hao. Tunaomba kwa vile Serikali ndiyo nyinyi mliochelewesha malipo hayo, basi muwalipe kwa thamani ya sensa nini na siyo ya mwaka 1977. Fedha hizo hazitawasaidia wastaifu hao. Kwa hiyo, Serikali mnawajibika kulipa riba wastaifu hao.

Pili, wastaifu waliolipwa kwa mkupuo tumekuwa tukipata matatizo kwa wastaifu waliolipwa kwa mkupuo, walipofika kuorodheshwa katika hazina ndogo za huko mikooani walielezwa kuwa watalipwa kwa awamu. Mbona suala hili limeteklezwa tofauti na tulivyo kubaliana humu Bungeni? Kwa nini wastaifu hao wa mkupuo wasilipwe kwa pamoa badala ya kuwaweka kwa makundi kama inavyofanyika hivi sasa? tatizo ni nini? Ninaomba nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Spika, Tatu, suala la mizani ya kupimia magunia ya mazao ya wakulima. Wakulima wetu wa Mikoa ya Rukwa, Iringa, Mbeya na Ruvuma ni wakulima wazuri sana wa mazao ya chakula na biashara. Wakulima wetu wamekuwa wakiiza mazao kwa kipimo cha macho, wakati wafanyabiashara wanauzwa mazao yao kwa kilo kwa kipimo cha mizani. Hivyo ili kuwasaidia wakulima katika mpango huu wa MKUKUTA ninaomba Serikali iondoe ushuru katika mizani ya wakulima ili bei yake iweze kuwa nafuu kuwawezesha wakulima Vijijini kununua mizani kwa bei nafuu ili waitumie kupimia magunia yao wanapowauzia wafanyabiashara. Kwa sababu mizani hiyo inauzwa kwa Shilingi 400,000 ambayo kwa mkulima wa kawaida hawezu kumudu

kununua mzani huo. Hivyo Serikali inaomba ione uwezekano wa kuondoa ushuru katika mizani hiyo ili kutoa nafuu kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, nyumba za *NHC – TEMEKE*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwauzia nyumba hizo wale wananchi wanaokaa katika nyumba hizo tangu mwaka 1961. Ziko katika hali mbaya, sana Mitaa ni michafu, barabara hazitunzwi, iko katika hali mbaya sana, kwa nini wananchi wanaoishi katika nyumba hizo, Serikali ikawasaidia kwa kuwauzia kama inavyofanya kwa nyumba zingine? Naomba nipatiwe majibu kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, tano mafao ya madiwani, tunaomba Serikali iandae Vizuri mafao ya madiwani watakapomaliza muda wao na wapewe mapema na wasicheleweshwe. Nini mipango katika utekelezaji wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nipatiwe majibu ya hoja hizi na ninaunga mkono hoja.

MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii ili niweze kuchangia katika hoja zilizo mbele yetu. Awali ya yote napenda kutoa rambirambi kwa jamaa na wananchi wa Kilombero kwa kufiwa na mpendwa wao, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mwenyenzi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, amani. Nawapongeza Ndugu Kikwete, Shein na Karume, kwa uteuzi wao katika Chama cha Mapinduzi.

Katika kuchangia nawapongeza Mawaziri wote kwa mipango na Bajeti Nzuri, jambo ambalo ni kawaida kwa Serikali ya CCM. Napongeza pia Serikali kwa kutenga pesa kwa wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Malipo yao yamalizike mapema maana wamengojea kwa muda mrefu.

Nampongeza pia Rais Benjamini W. Mkapa, kwa kutuongoza vizuri hadi madeni yetu ya Nchi za Nje kusamehewa. Tuendelee basi na kutumia pesa hizi kwa uhadilifu na kiutawala bora.

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudzi za Serikali katika kuendeleza miundombinu, hususani, ujenzi wa Barabara. Rai yangu ni kwamba tuwasimamie makandarasi kwa karibu ili barabara zijengwe mapema. Vile vile barabara ya Dodoma-Manyoni-Itingi-Kigwa-Tabora-Kigoma ijengwe kwa kiwango cha lami mapema iwezekanavyo. Wananchi wa Tabora wanapenda Mkoa wao ufunguke kwa barabara. Daraja la Malangalasi lijengwe mapema na lipewe jina la Rais Awamu ya Nne ambaye, *Inshallah*, atakuwa Ndugu Jakaya Mrisho Kikwete. Tunashukuru Serikali kwa ubinafsishaji wa *Tabotex* maana hivi karibuni wananchi wengi wataajiriwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja za Wizara zote mbili tajwa kwa asilimia mia.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: napenda kukupongeza kwa jitihada ninazofanyika kukusanya mapato. Wananchi wa Jimbo la Busanda wanashukuru jitihada hizi ila wanashangaa, pamoja na makusanyo hayo ni kwa nini hawapati matokeo, kwa mfano;

Kuna mradi wa maji wa Nyakagomba-Chigunga hadi Katoro, mradi huo ulianza mwaka 1996 hadi leo haujaisha. Kuna tatizo gani wakati kuna pesa. Maji yanatolewa ziwani ni karibu na maeneo hayo.

Vijiji au miji midogo ya Nyahazwa, Bukoli, Rwanas, Backif, Katoro ni maarufu kwa uchimbaji wa dhahabu na wamejenga shule kila kata. Nauliza ni lini watapelekewa umeme kutoka Katora au Geita kwani mnawasaidia kuzalisha dhahabu zaidi na wanafunzi wataweza kujifunza masomo ya komyuta. Umeme katika maeneo haya utaimarisha MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina utaratibu gani kumsaidia mkulima ambaye mazao yake hushuka bei bila kujali gharama alizotumia katika pembejeo. Kwa mfano mwaka huu pamba bei ni Tsh. 150 kwa kilo ambayo inamkatisha tamaa mkulima, au Serikali inashauri pamba isilimwe tena Serikali itasaidiaje? Tunapenda kufahamu jengo la Benki Kuu linatarajia kuwa kitu gani kwani upanuzi siyo wa kawaida, na mpaka litakapokwisha linatarajia kugharimu kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, ushauri, *TRA*, *Long Room* pana usumbufu sana kiasi cha kusababisha wateja wengi kukimbilia Bandari ya Mombasa. Wizara ya Nishati na Madini hasa Eneo la MADINI Bado haijafanyiwa kazi ipasavyo. *TRA* haina wajuzi wa kufuatilia wala kukagua biashara ya madini, na hata Wizara yenyewe ya Nishati na Madini ina suasua haina uwezo.

TRA haina uwezo wa kudhibiti mitambo inayoingia wala kutathimini thamani ya mitambo. Inahitajika nguvu ya ziada katika eneo hili wawekezaji, madini ni wajanja, hususan mkataba isipokuwa makini au kuandaliwa kwa makini.

Mikataba yetu ya madini ni kama vile ilipigwa *photocopy* hivyo ilifanana kwa migodi yote na kama vile inazalisha sawa. Wanasheria wetu waelezwe kwa makini. Ahsante.

MHE. MARGARET A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Basil Mramba, Manaibu Mawaziri Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kuandaa Bajeti nzuri yenyewe matumaini ya maendeleo ya Watanzania walio wengi.

Pia natoa rambi rambi kwa wananchi, familia ya Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga kwa kuondokewa na mpendwa uwakilishi wao na Mungu ailaze pema Roho yake peponi.

Mheshimiwa Spika, mchango wako utakuwa katika maeneo yafuatayo:-

Naomba nielimishwe ni vigezo gani vinavyotumika kufikia *Ceilings* za Wizara na Taasisi zake mbalimbali. Nataka kufahamishwa suala hilo kwa vile mgawanyo wa fedha za Bajeti wa kila Wizara naona zinatofautiana sana pamoja na kwamba majukumu ya kila Wizara ni muhimu na mazito. Nikichukulia Wizara chache kama mfano, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ambayo inahusika na wazee, walemavu, wajane migogoro ya kifamilia na kazini, watoto watukutu, michezo na kadhalika sehemu hizo zote ni nyeti kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, lakini inashangaza kuwa Fedha wanayopangiwa mwishowe ni ndogo kuweza kukamilisha majukumu yao. Hivyo kwa ujumla natoa rai kuwa ni muhimu kutathimini upya vigezo hivyo eneo jingine ni ELIMU.

Mheshimiwa Spika, katika suala la elimu natoa pongezi kwa mafanikio ya mpango wa MMEM, MMES na jitihada zilizoanzwa za kuboresha Elumu ya Juu na ya Ufundu. Pamoja na pongezi hizi bado mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa watoto, wanachuo wenye ulemavu wnapata elimu inayostahili haiko wazi au hakuna. Kwa msingi huo kundi hili la jamii ya Watanzania litabaki kuwa la nyuma daima katika nyanja zote za maisha. Nalisemea hili kwa vile sikuona cha kuniridhisha katika Hotuba si ya mipango wala fedha kwa maana kwamba sina uhakika kiasi cha fedha zilizotengwa kuhakikisha vifaa vya kujimudu vya kusomea na kujifunzia urekebishaji wa mazingira maalum ya kujifunzia na kadhalika. Natoa rai kujaribu kuwa makini katika kuliwezesha kundi hili la jamii kielimu kwa vile ELIMU ndiyo Mwanga wa maisha duniani hasa dunia hii ya utandawazi.

Mheshimiwa Spika, suala la viwanda, pongezi kwa Serikali katika azma yake ya kuendeleza viwanda vidogo vidogo, vya kati na kadhalika. Lakini naamini wakati umefika wa Serikali kushawishi wawekezaji wa nje na ndani kuwekeza kwenye viwanda vilivyokuwa vinazalisha bidhaa za kuzalisha bidhaa zingine (Viwanda Mama) ili tupunguze kuagiza bidhaa kma hizo nje.

Mheshimiwa Spika, usafirishaji: Katika suala hili Serikali inapaswa kupongezwa kwa vile umeondoa leseni kwa magari makubwa na *pickups* naamini kwa lengo la kuwapunguzia wakulima gharama za kusafirishia mazao yao toka sehemu mpaka kwenye masoko. Pamoja na pongezi hizi nashauri kuwa unafuu huu utolewe kwenye magari ya kusafirisha abiria. Pia hii ni kwa sababu gharama za kugharimia uendeshaji katika sekta ya usafirishaji bado ni kubwa bei ya vipuri, petroli na kadhalika. ni vya bei ya juu, hivyo kuathiri nauli za safari zao.

Katika kijitabu cha Bajeti ukurasa 15 kuhusu Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya Benki kwa ajili ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi ni kwamba bado si rahisi kwa mwananchi kwa kawaida kujua nini hasa vigezo vinavyotumika ili kuweza kufaidika nao. Hivyo natoa rai kuwa ni muhimu sana wananchi waelezwe wazi vigezo hivyo ili kuwarahisishia mchakato mzima wa jinsi hatimaye watakavyofaidika. Nachelea kuamini kuwa wananchi wengi wanajua nini hasa ni *Export Credit Guarantee Scheme*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kudonoa hayo machache naunga mkono hoja hii.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa namna walivyo wasilisha bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha anipe maelezo kwani sija fahamu vizuri hizi pesa ambazo 4.5 ambazo wanapewa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni za vipi, kwani kuuliza si ujinga kuwa kitu huja kifahamu kwani kuwa zinatolewa kwa ajili ya msaada tu kutoka Serikali ya Muungano kwa Serikali ya Zanzibar, la ikiwa kuna Sheria ye yeyote inayotaka kufanya hivyo basi kiasi hicho ni kidogo sana.kwa nini nikasema kuwa ni kidogo, kwa sababu Zanzibar ni nchi na inahitaji fedha nyingi za kujientesha na kipato chake kwa hivi sasa ni kidogo sana. Kwa hivyo, sehemu ya pato la Taifa ni bora likaangaliwa upya ili Zanzibar iongozwe.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii mimi nimefurahishwa na kitu kimoja tu kwenye kuongeza ushuru kwa vitu vya anasa kwani ikiwa unaona hupendi basi acha yaani, kulewa na kuvuta sigara.

Mheshimiwa Spika, mimi kuhusu ubinafsishaji sina wasi wasi isipokuwa ninadukuduku kuhusu kubinafsisha Benki ya *NMB*. Kwa kweli Benki hii ikibinafsishwa itaendelea na kazi zake kama hivi sasa kwani makampuni mengine yakishapewa mashirika huwa hayafikishi huduma mote. Kwanini nikasema hivi kwa sababu hivi sasa katika kisiwa chetu cha Pemba tuna benki moja tu ya Muungano nayo ni hii ya *NMB*. Hatuna *CRDB* wala *NBC* na kadhalika. Kwa hivyo tahadhari yangu na hiki kisije kikapata mgeni akakiondoa. Kwa hivyo wakati wa kubinafsisha hadi mikataba iwe mizuri, na vile vile ninapenda nitowe dukuduku langu kuhusu kubinafsishwa kwa Shirika la Reli.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya Mikoa ya nchi yetu bado haijawa na miundo mbinu ya barabara mizuri, kwa mfano Kigoma sasa mimi wasiwasi wangu ni hili Shirika likaja likapewa mtu na akashindwa kuliendesa vizuri na akawasumbua zaidi wananchi wa mkoa huu ambao wanategemea train kwa safari zao za kwenda Dar es Salaam na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, au Serikali ijitahidi iwatengenezee barabara toka Tabora hadi Kigoma ndio sasa ibinafsisha Shirika hili, vinginevyo nikucheza na maisha ya watu.

MHE. AGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Basil Mramba, Mbunge Waziri wa Fedha kwa hotuba nzuri ambayo ninamini inamsaidia mwananchi mnyonge. Hata hivyo naona kuna hoja ya kutilia mkazo zaidi katika eneo la Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya niliyochangia kwa kauli, ningependa kuongeza kuchangia yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utaratibu na Uoanishaji wa Mipango Mkoo ya Taifa, Wilaya na Vijiji. Nimefarijika sana kwa azma ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji kwamba Wizara yake imeazimia kuboresha taratibu za uratibu wa mipango. Hili ni suala muhimu sana ili kupunguza kero kubwa ya wananchi kuchelewa kupata fedha au vitendea kazi na watumishi kama vile madaktari, walimu na watumishi wengine na hivyo kukwamisha ukamilishaji wa miradi au uzinduzi wa miradi iliyokamilika.

Mheshimiwa Spika, Ushindani na Motisha Kuchochera Maendeleo, nashauri kwamba uanzishwe utaratibu wa kushindanisha kaya kwa kaya, vijiji kwa vijiji, wilaya kwa wilaya, mikoa kwa mikoa na taasisi kwa taasisi au kampuni kwa kampuni kwa kuwaweke malengo ya uzalishaji au utoaji huduma na kuwazawadia wale wanaofanya vizuri. Utaratibu namna hii unatumika nchi nyingi kuhamisha ushindani na maendeleo, kwa mfano Uingereza inatoa '*queens' Award*' kwa wanaviwanda na wafanyabiashara wanaofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, vigezo vya Mgawanyo wa Fedha Maendelo, zaidi ya kutumia idadi ya wananchi katika kufanya mgao wa fedha kwa ajili ya maendeleo viwango vya maendeleo katika maeneo mbalimbali na nafasi (*potential*) ya maendeleo pia viwe mionganini mwa vigezo muhimu katika mchakato wa mgao wa fedha za maendeleo. Aidha vipori vya miradi ambavyo vimekwama kwa sababu zilizo nje ya uwezo wa miradi husika, nayo ifikiriwe kwa mgao.

Mheshimiwa Spika, kodi mpya ya vimeo na sigara, kimsingi naafiki mapendekezo yaliyomo katika mapendekezo ya Bajeti ya 2005/2006. Hata hivyo, nadhani vimeo na sigara kutoka nje vingeweza kuwekewa viwango vikubwa zaidi ili mradi hatuvunji masharti ya *WTO* na mikataba mingine kama vile Protokoli ya soko la Jumuia ya Afrika Mashariki na Mikataba ya nchi kwa nchi *bilateral agreements*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia 100, kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri hawa, Manaibu wao, Makatibu Wakuu na wataalamu wengine wote wanaohusika kwa kazi nzuri na kuwatakia mafanikio mema.

MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kwa masikitiko makubwa natoa mkono wa rambirambi kwa familia ya marehemu Hassan Diria na familia ya Marehemu Abu Kiwanga, Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi, Amina.

Pili, napenda kuwapongeza kwa dhati viongozi wetu wakuu waliochaguliwa kugombea kwa tiketi ya CCM. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, mgombea nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mohamed Shein kuwa mgombea mwenza.

Pia nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa Mgombea Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mawaziri wa Wizara zote mbili yaani Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha pamoja na Manaibu Waziri wa Wizara hizo na watendaji wote walioshiriki kuandaa hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kutoa mchango wangu juu ya hotuba ya bajeti kwa kuanzia ni kuhusu mishahara ya kima cha chini. Kwa kweli hali ya maisha ni ngumu ukilinganisha na kima cha mshahara kinachotolewa hivi sasa, maisha yamepanda sana kiasi ambacho hayakidhi hata kidogo mahitaji ya lazima ukilinganisha na kima cha chini cha mshahar. Hivyo naomba Serikali iwaangalie wananchi wake kwa jicho la huruma kwa kuongeza mshahara angalau kima cha chini kiwe laki moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari ya Zanzibar, kwa kweli bandari ya Zanzibar hivi sasa hairidhishi kwani abiria wanaosafiri hawana sehemu ya kukaa wakati wakisubiri chombo cha kusafiria na vile vile hakuna sehemu maalum ya viongozi wakuu (*V.I.P*) ambayo inejengwa kwa makusudi kwamba viongozi wakae sehemu hiyo wakisubiri chombo cha kusafiria.

Ushauri wangu ni kwamba naomba ijengwe sehemu maalum ya abiria wa kawaida wanaosafiri na pia ijengwe sehemu maalum ya viongozi (*V.I.P*) wanaosafiri kama vile bandari ya Dar es Salaam.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango kwa niaba ya wananchi wa Misungwi. Nianze kumpongeza Waziri, Manaibu Waziri wote wawili, Makatibu Wakuu, Mgonja na Lyimo pia Naibu na Watumishi wote wa Wizara na Idara zote kwa kazi nzuri ya kusimamia mapato na matumizi kwa kipindi chote walichokuwa nacho.

Mheshimiwa Spika, hali halisi inaonekana katika shule zilizoko huko kijijini shule, afya, barabara na huduma zingine zote kwa sasa ni tofauti sana na miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, hotuba zote mbili ni nzuri ikiwa ya mipango nayo inaonyesha wapi tunatoka tuko wapi na tunaeleka wapi hivyo pongezi zimwendee Mheshimiwa Kigoda Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie yafuatayo katika hotuba ya Waziri wa Fedha ukurasa wa 44. (1) Kuhusu kufuta ada za leseni kwa wasafirishaji mbalimbali wa mizigo (magari makubwa).

Mheshimiwa Spika, utozaji wa leseni ya magari mazito ni kati ya vyanzo vine vya mfuko wa barabara vilivyo kisheria namba mbili ya ushuru wa barabara ya mwaka 1998. je, kufuta chanzo hicho hakipingani na Sheria hiyo namba mbili ya 1998?

Mheshimiwa Spika, ni vyema Waziri akaeleza ni jinsi gani atafidia pengo la mfuko wa barabara katika bajeti yake kwani chanzo hicho kilikuwa kinaleta pato la Tshs 190,000,000/= vile vile pesa hizi zinaweza kutengeneza kilometra 190 ambayo ni sawa na bajeti ya H/L moja kwa migao wanayopata.

Mheshimiwa Spika, majibu ya kuridhisha yatafaa kwani badala ya kushangiliawa wenyewe magari makubwa watalia kwa vile barabara zitaendelea kuharibika.

Mheshimiwa Spika, bajeti ni nzuri ombi ni vyema Wizara ya Ujenzi ikaelekezewa nguvu yao kwenye soko bila usumbufu kwani sasa hivi barabara zinazosimamiwa na H/L ni mbovu mno zinahitaji pesa nyingi ili kuondoa umaskini kwa wanakijiji. Tunaipongeza Serikali kwa kazi nzuri za ujenzi wa barabara kuu na zile za mikoa kiasi.

Mheshimiwa Spika, bado ni tatizo kubwa kwa Reli ya kati usumbufu wa pakia pakua pakia ni tatizo wanaloopata wananchi wa kanda ya Ziwa na pia Dar es Salaam ni vyema reli ilekebishwe mizigo ipakiwe mara moja tu.

Mheshimiwa Spika, maji safi na salama bado ni tatizo kubwa sana. Juhudi zifanyike kama jinsi Serikali ilivyoamua kutumia pesa zake kwa mradi wa Ziwa Victoria hadi Kahama na Shinyanga.

MHE. MWANAIDI HASSAN MAKAME: Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukrani zangu za dhati kwa Mawaziri wote wawili, Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa hotuba zao nzuri sana za Bajeti zenye mwelekeo mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, msamaha wa madeni, naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Tanzania kwa kusimamia vizuri madini yanje na kupata masharti mbalimbali ya nchi tajiri duniani mpaka na sisi kuingia katika kupata msamaha kati ya nchi 18 maskini dunia, ahsante sana Serikali ya awamu ya tatu, hongera Mkapa.

Pia naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupa nafasi za upendeleo kwa asilimia thelathini katika nafasi ya maamuzi nchini ya Bunge. Hii imeonyesha tosha mkutano mkuu wa Bejing uliyothaminiwa na Serikali yetu ya awamu ya tatu na utekelezaji wake kama huo kutupatia nafasi hivyo kina mama shukrani zetu waziwazi.

Mheshimiwa Spika, kumalizia UKIMWI, nashauri kwa Semina zinazofanywa kwa kuwaeleimisha juu huko na nashauri sasa semina hizo zifanywe vijijini ambako ndiyo kunakuwa na wananchi wengi zaidi, na wao wapate mafunzo juu ya athari ya maradhi hayo wajue kuwa hiyo dawa, fedha zinazotolewa na wafadhili kwa ajili ya semina nashauri fedha hizo sasa wapewe wagonjwa walioathirika zipate kuwasaidia kwa kupata chakula kilicho bora kinacho shauriwa na madaktari.

Mheshimiwa Spika, ushuru wa forodha, hivi sasa kina mama wengi wanajishughulisha na biashara ndogondogo wanakwenda kuchukua bidhaa Zanzibar, lakini wanapofika bandari ya Dar es Salaam kinamama hawa hupata shida nyingi sana ya kutozwa ushuru mara mbili na omba Serikali iwaangalie kina mama hao, kwa sababu wao wanatafuta kwa kupambana na maisha magumu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):
Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa mchango wangu katika bajeti hii, napenda nami kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Magu, kutoa salamu za pole kwa wananchi wa Kilombero kwa kuondokewa na ndugu yao mpendwa Hayati Abu Kiwanga aliyeitwa mbele ya haki.

Aidha, napenda kutoa pongozi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Mheshimiwa Dr. Mohammed Shein na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuteuliwa kwao kupeperusha bendera ya CCM katika uchaguzi mkuu ujao. Ni matumaini yangu kuwa hii ni timu itakayoipa CCM ushindi mnono mwezi Oktoba mwaka huu, 2005. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Fedha kutolea ufanuzi baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Kwaangw' alitoa hoja kwamba Serikali iongeze kiwango cha mgao wa ushuru wa mafuta (*fuel levy*) kwa Halmashauri za Mikoa kutoka kiwango cha sasa cha 30%.

Mheshimiwa Spika, viwango vya mgao wa mapato ya ushuru wa mafuta kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, umezingatia mgawanyo wa majukumu kati ya ngazi hizi za Serikali. Iwapo kuna mabadiliko yoyote kuhusu mgawanyo wa majukumu kati ya vyombo hivi vya Serikali, Serikali itabidi iangalie upya na kulifanya kazi suala hili na kuleta mapendekezo Bungeni ili kupata ridhaa yake. Hivyo tunaomba tupate muda zaidi kutafakari suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ilitolewa juu ya tozo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye vipuri vya matrekta ya kilimo. Hoja hii imeelezewa na Wabunge kadhaa ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki.

Serikali inatambua umuhimu wa kilimo katika kuchangia pato la Taifa na kuinua hali ya maisha ya wananchi walio wengi vijiji. Kwa mantiki hii, ndio maana imetenga kiasi kikubwa cha fedha katika bajeti yake ya mwaka huu na kutoa vivutio vingi vya kodi na visivyo vya kodi. (*Makofî*)

Serikali imepokea mapendekezo kutoka kwa wadau wa sekta ya kilimo ya kusamehe kodi ya *VAT* kwenye vipuri vya matrekta kwa ajili ya kilimo. Hata hivyo,

pamoja na nia nzuri bado Serikali inaona ugumu uliopo katika kutofautisha vipuri vya matrekta kwa ajili ya kilimo na vyombo vingine vya usafiri visivyo vya kilimo ambavyo vinatumia vipuri vya aina hiyo hiyo. Hivi sasa Serikali kwa kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inalifanyia kazi suala hili ili kuweza kukubaliana utaratibu wa kutofautisha vipuri vya matrekta ya kilimo katika kitabu cha forodha cha Jumuiya. Hivyo tunawaomba Waheshimiwa Wabunge wavute subira.

Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya pamoja na Mheshimiwa Dr. Kamala, walitoa hoja juu ya kupungua kwa viwango vya ushuru wa forodha kwa mafuta ya kula yanayoingizwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 1/1/2005, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeanza kutekeleza itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Community Customs Union Protocol*) ambapo viwango vya ushuru wa forodha kwa bidhaa zote vinakuwa sawa (*Common External Tariff*). Mabadiliko ya viwango hivi hupangwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tangu tumeanza kutekeleza itifaki hiyo, kiwango cha ushuru wa forodha kwa mafuta yaliyosindikwa na kuwa tayari kwa kutumiwa ni 25%. Kiwango hicho kilitumika pia katika sheria yetu ya ushuru wa forodha kabla ya kuanza kutekeleza itifaki hiyo.

Kwa hiyo, kiwango hicho hakijapungua. Kiwango hiki ni kwa mafuta ya aina zote ambayo yanaingizwa nchini yakiwa yamesindikwa.

Mheshimiwa Spika, mafuta ghafi, yaani *crude oil*, ya aina zote yanatozwa ushuru wa forodha wa asilimia sifuri isipokuwa mafuta ghafi yatokanayo na mbegu za alizeti na pamba ambayo yamewekewa ushuru wa forodha wa 10%. Lengo kuu ni kuhamasisha uzalishaji wa mazao haya katika nchi za Afrika Mashariki na kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha mafuta ya alizeti na pamba. Mafuta ghafi yaliyowekewa asilimia sifuri ni yale ambayo katika mchakato wa uzalishaji yanatoa bidhaa nyingine kama zile za kutengenezea sabuni, mafuta ya mgando na kadhalika. Hata hiyo, ningependa ielewewe kuwa hivi sasa hakuna mafuta ghafi yanayoagizwa toka nje.

Mheshimiwa Mwakipesile alitoa hoja kwamba Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) iondolewe kwenye vipuri vya meli kwa mantiki iliyotumika kuondoa kodi hiyo kwenye vipuli vya treni.

Mheshimiwa Spika, mfumo mzuri kabisa wa Kodi ya Ongezeko la Thamani ni ule ambao bidhaa na huduma zote hutozwa kodi hiyo. Hata hivyo, kwa kuzingatia sababu za kiuchumi, kijamii na kiutawala, misamaha ya *VAT* hutolewa kwa baadhi ya bidhaa. Mashirika yetu ya reli yamekuwa katika hali mbaya sana kiuchumi na Serikali imeona kuwa moja ya nija ya kuyakomboa ni kuyapatia unaafuu maalum wa *VAT* kwenye ununuzi wa vipuri vyake. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, usafiri wa reli na meli ni tofauti katika nchi yetu hasa ikizingatiwa kuwa tuna reli mbili tu za *TAZARA* na *TRC* ambapo kwenye usafiri wa majini ziko meli nyingi na vyombo vingine vingi vya usafiri na usafirishaji. Hivyo sio

rahisi kusimamia msamaha wa namna hii kwa usafirishaji wa majini ili kudhibiti uwezekano wa kuvuja kwa mapato ya Serikali. Tunahitaji kufanya utafiti kwanza kabla ya kuchukua hatua hiyo kwa vyombo nya majini. Waheshimiwa Mussa Lupatu na Abdula Suleiman Lutavi walitoa hoja kuwa matokeo ya misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye pembejeo za kilimo na vipuri nya treni yamfikie mlengwa na sio kuwaongezea faida wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaposamehe kodi inakuwa imedhamiria kuwa misamaha hiyo iwanufaishe walengwa. Kwa vile Serikali ilishajitoa katika shughuli za kibiashara, matokeo ya msamaha wa kodi kwa bei kwa mlaji hutegemea nguvu ya soko. Kwa kawaida bei ya bidhaa ni majumuisho ya gharama za uzalishaji na uagizaji, faida pamoja na kodi. Hivyo, kimsingi misamaha ya kodi hutegemewa kuleta unafuu kwenye bei ya bidhaa husika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kuna uwezekano kuwa wafanyabiashara wasio waaminifu wanatumia unafuu wa kodi kujinufaisha wenyewe kwa kujipatia faida kubwa. Serikali pamoja na wadau wote tuna majukumu ya kuhakikisha kuwa misamaha hii inaleta unafuu kwa wale wanaostahili. Serikali kwa upande wake itaendelea kuweka mazingira mazuri ikiwa ni pamoja na kuongeza ushindani kwenye soko. Wadau wote, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, tunawajibika kushirikiana na Serikali kuwafichua wale ambao wanatumia unafuu tunaotoa kwa kupitia misamaha ya kodi kujinufaisha wao binafsi badala ya kuwafikishia walengwa.

Waheshimiwa Hamad Rashid, Eliachim Simpasa; Edson Halinga na Dr. Amani Kabourou wametoa hoja kwamba Serikali imekuwa na huruma sana kutoza kodi kwa sekta ya madini, ambayo ni sawasawa na kutoa zaka.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge dhidi ya kodi ndogo tunayotoa kwenye sekta ya madini ni ya muda mrefu sasa. Serikali imeanza kulifanyia kazi suala hili kwa kuteua wakaguzi waliopewa jukumu la kupitia shughuli za makampuni makubwa ya madini na kuleta mapendekezo Serikalini. Wakaguzi hao yaani *M/s Alex Stewart Assayer's Government Corporation* walianza kazi June, 2003 na tayari wamekamilisha ripoti ya awali ya ukaguzi kwa baadhi ya makampuni. Wakaguzi hao wanaendelea na ukaguzi wa makampuni yaliyobaki na zoezi hili likikamilika, Serikali itafanya uchambuzi wa mapendekezo yote na kuleta Bungeni mapendekezo ya kuboresha mfumo unaotumika hivi sasa.

Mbali na ripoti ya wakaguzi hao, Serikali imepitia upya suala la misamaha ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) na kubaini kuwa hakuna ulazima wa misamaha hii kuendelea kuwepo kwa kuwa tayari mfumo wa *VAT* unaruhusu kujirejeshea kodi wanayolipa kwenye manunuzi yao pindi wanapowasilisha *return* zao za *VAT*.

Aidha, Serikali iliunda Kamati Maalum yaani *Mineral Policy Review Committee* ili kuangalia jinsi Serikali inavyoweza kuboresha usimamizi katika eneo hili. Taarifa ya Kamati hii imekamilika na Serikali inayafanya uchambuzi mapendekezo yaliyomo katika ripoti kwa lengo la kuyatekeleza.

Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mbunge wa Mvomero, alitoa hoja kwamba Serikali iweke *flow meters* Tanga, Mwanza na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufunga *flow meters* katika *Jetty* ya Dar es Salaam mapato ya Serikali yameongezeka kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, kulijitokeza mapungufu madogo madogo ambayo baadhi yameshashughulikiwa na mengine bado yanashughulikiwa. Kama hatua za mwanzo, Serikali imeamua kuanza na Dar es Salaam ambako ndio mafuta mengi hupitia. Hata hivyo, lengo ni kufunga mita hizo katika bandari zote ambako mafuta huteremshwa zikiwemo zile za Mtwara, Tanga na Mwanza. Tayari zabuni zimeshatangazwa kwa ajili ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja pia kwamba Serikali isimamie kikamilifu mafuta ya ndege (*JET A-1*) ili yasihuishwe na mafuta ya taa. Kuhusu usimamizi wa *JET A-1* ni kweli kwamba mafuta hayo hutumika kama mafuta ya taa. Serikali inatambua ukweli huo na hata hivyo kutokana na unyeti na taratibu za Kimataifa za kuhifadhi mafuta hayo, hadi sasa ni kampuni mbili tu zinajihuisha na uingizaji na usambazaji wa mafuta ya ndege. Ili kuhakikisha kuwa msamaha huo unatolewa kwa walengwa tu Mamlaka ya Mapato Tanzania imeweka taratibu madhubuti za kusimamia kampuni hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, vile vile ilitolewa hoja kwamba Serikali isitishe vibali vya sukari. Kuhusu vibali vya sukari, Serikali kupitia Bodi ya Sukari ina utaratibu wa kutathmini uzalishaji wa sukari nchini na kutoa vibali wakati wa upungufu ili kukidhi mahitaji ya walaji. Hata hivyo, ili kutoathiri uzalishaji wa sukari katika viwanda vyetu vya ndani, Serikali huweka muda maalum wa kuileta sukari hiyo hapa nchini. Muda huo huzingatia pia muhula wa uzalishaji wa viwanda vya ndani. Wizara ya Kilimo na Chakula itaelezea zaidi suala hili wakati ikiwasilisha bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, pia ilitolewa hoja kwamba Serikali iweke mikakati mipy ya kufutilia *VAT*. Kuhusu mikakati mipy ya kuboresha mapato yatokanayo na Kodi ya Ongezeko la Thamani, Mamlaka ya Mapato ya Tanzania ilianzisha zoezi maalum linalojulikana kama ‘operesheni kashikashi’ kwa lengo la kuwakamata wafanyabiashara sugu ambao wanauzu bidhaa bila kutoa stakabadhi na ankara za kodi. Zoezi hili lilianza mwezi Oktoba mwaka jana na kati ya wafanyabiashara 826 ambao tayari wameshatembelewa, wafanyabiashara walionaswa Mkoa wa Dar es Salaam tu ni 91 na kulpishwa adhabu ama faini ya Sh.25.9mil kwa kosa hilo. Kwa kuwa zoezi hili limekuza sana uwajibikaji wa hiari kwa walipa kodi, *TRA* itaendelea kulitekeleza. Kwa hiyo ‘operesheni kashikashi’ itaendelea ili kuwatia kashikashi ambao wanafanya vitendo hivi.

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya Serikali ya kuongeza kiwango cha usajili kutoka Sh.20mil hadi Sh.40mil yalikuwa na lengo la kuhakikisha kuwa kunakuwa na ufanisi katika ufuutilaji *VAT* na hatua hii imepelekea kupungua kwa wafanyabiashara waliosajiliwa na kuongezeka uwezo wa Mamlaka ya Mapato katika kusimamia Kodi hii ya Ongezeko la Thamani. Pia *TRA* itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake waliopangiwa kufanya ukaguzi wa nyaraka na kumbukumbu za biashara kwa lengo la

kuhakikisha kuwa wana ujuzi wa kutosha kukabiliana na wafanyabiashara wanaokwepa *VAT* pamoja na kodi nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ieleweke kuwa ushirikiano na wananchi hasa kwenye suala la kuwafichua wafanyabiashara wasiota za kodi na wale wanaotoa bei mbili mbili yaani bei yenyé *VAT* na bei isiyo na *VAT* ni muhimu sana. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuwahamasisha wananchi wao katika kufichua wafanyabiashara wa aina hiyo.

Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda alitoa hoja kwamba utaratibu wa kiforodha wa kutoa mizigo *long room* na bandarini. Mamlaka ya Mapato imekuwa ikichukua hatua kadhaa ili kuboresha na kuimarisha usimamizi wa forodha ili kuboresha huduma za uondoshaji mizigo Bandarini zikiwemo zile zitolewazo *long room*. Hatua hizo ni pamoja na kuwa na majadiliano na vyombo vingine kama Mamlaka ya Bandari, Kitengo cha Makontena kwa nia ya kurahisisha taratibu. Majadiliano haya yameonyesha kuwa na mafanikio mazuri.

Aidha, kwa upande wa urahisishaji wa nyaraka na taratibu, tumeanza kutumia mtandao wa *computer* badala ya utaratibu wa zamani ambapo wakala walihitajika kufika *long room* kushughulikia kadhaa yake *physically*. Programu hii mpya ya *computer* inayoitwa *ASYCUDA++* itaendana pamoja na mradi wa *direct trade input*. Katika utekelezaji wa haya. Mlipa kodi atawasilisha kadhaa au nyaraka zake kwenye ofisi ya mkandarasi wa *direct trade input* ambaye ataziingiza kwenye mfumo wa *ASYCUDA++*. Mfumo huu pia unatoa nafasi kwa walipa kodi wenye *computer* kufungiwa sehemu ya mfumo huu *ASYCUDA++* ambayo itawezesha walipa kodi hao kuingiza kadhaa zao wakiwa kwenye ofisi zao na kuziwalisha moja kwa moja idara ya forodha kwa njia ya mtandao (*Electronic Transfer*). Faida ya mfumo huu ni pamoja na kuharakisha kutoa mizigo, kupunguza mlundikano wa walipa kodi kwenye ofisi za forodha, kulipia kodi zote kupitia benki bila kuhitajika kwenda ofisi za forodha na kuruhusiwa kuchukua mizigo bila kupitia ofisi za forodha.

Aidha, hisia na mtazamo wa kuwepo mianya ya rushwa pia itazibitiwa. Utaratibu huu umeanza kutumika kwa majoribio tarehe 13/6/2005 katika kituo cha uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam na utafuatiwa na *long room*, Zanzibar na vituo vingine vya forodha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, msingi wa utaratibu huu ni uaminifu wa wakala na mwagizaji kuwa mzuri, walipa kodi wanatakiwa kuwa wakweli katika kutoa taarifa wanazozipeleka Idara ya Forodha. Hii itarahisisha na kuharakisha taratibu zote za utoaji wa mizigo. Aidha, wakala na waagizaji wanatakiwa wajitokeze haraka mara wanaposhauriwa kuwa mizigo yao imeshaachiliwa.

Mheshimiwa Faustine Rwilomba alitoa hoja pia kwamba utaratibu wa misahama ya kodi wa *treasury voucher* unachukua muda mrefu. Serikali iliweka utaratibu wa hundi za Hazina (*treasury vouchers*) ili kudhibiti misamaha iliyokuwa inatolewa kwa mashirika ya dini, mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na watumishi wa umma. Utaratibu huu

umeonyesha mafanikio makubwa. Hivi sasa, Serikali inalipia misamaha hiyo na kiwango cha fedha inayotumika kimepungua baada ya kuweka utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu uliopo sasa, kadhia zote huwasilishwa na waagizaji na kushughulikiwa na Idara ya Forodha baada ya mizigo kuwasili. Hii inahusisha pia ukaguzi wa mizigo hiyo mathalani magari. Ili kuthibitisha usahihi wa nambari za *chassis* na injini kabla ya kukokotoa kodi inayostahili kulipwa. Baada ya kukokotoa kodi hiyo, ankara hutayarishwa kwenda Hazina kwa ajili ya kuandikiwa hundi. Utaratibu uliowekwa hauchukui zaidi ya siku saba toka kutayarisha ankara hadi hundi kupokelewa *TRA* sawa na muda uliowekwa na Mamlaka ya Bandari kabla ya kuanza kutoza gharama za kutunza mizigo (*storage charges*).

Kwa mantiki hiyo, *TRA* inatakiwa kutumia siku mbili kukamilisha kadhia na kuziwasilisha Hazina kwa ajili ya kuandikiwa hundi. Pia Hazina inatakiwa kutumia siku mbili kuandika hundi na siku zilizobakia kukamilisha utaratibu wa kutoa bidhaa bandarini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha utaratibu uliowekwa ili kupunguza muda wa kutoa hundi za Hazina chini ya siku saba za sasa. Hata hivyo, walipa kodi wanaotumia utaratibu huu wanatakiwa walete taarifa sahihi na kukamilisha taratibu nyingine na vyombo vingine kabla ya kuleta kadhia Idara ya Forodha. Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi alitoa hoja kwamba ili kuwezesha wananchi watumie umeme, hasa maeneo ambayo hayana umeme wa *TANESCO*, Serikali iondoe kodi kwenye *generator* za *diesel* na vifaa vinavyotumia nguvu ya jua ili wananchi waweze kuvitumia kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, *generator* za umeme zinatambuliwa kuwa ni bidhaa za mtaji, yaani *capital goods* na zina msamaha wa ushuru wa forodha. Pia wanunuzi wa *generator* hizo hawalipi Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kuwa ni bidhaa za mtaji.

Mheshimiwa Spika, vifaa vya nguvu ya jua navyo vina msamaha wa *VAT* kwa mujibu wa kipengele cha 22 cha jedwali la pili la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1997 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria ndogo Na.5 ya mwaka 2005. Pia wananchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamekubaliana kuondoa ushuru wa vifaa vya nguvu ya jua isipokuwa betri ambazo hutumika kwa matumizi mengine kama vile kwenye magari. Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa kinachowasababisha wananchi kushindwa kununua vifaa hivyo sio kodi ila ni bei zinazopangwa na wauzaji.

Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza alitoa hoja ya kupunguza kodi kwenye mitungi ya gesi na magari ya kusambazia gesi. Kiwango cha ushuru wa forodha kwa mitungi ya gesi inayoagizwa kutoka nje ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ni 25%. Katika nchi za Afrika Mashariki bidhaa hiyo huzalishwa nchini Kenya. Kutokana na makubaliano ya utekelezaji wa itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki bidhaa hii hutozwa ushuru wa kiwango cha 5% tu ambapo kiwango hicho kitapungua mpaka kiwango cha asilimia sifuri katika kipindi cha miaka mitano

ijayo kama bidhaa hizo zitaagizwa kutoka nchi wanachama wa Jumuiya hiyo. Ili kufanikisha malengo ya kuundwa kwa itifaki ya Umoja huo, tunawashauri walipa kodi wetu kuagiza bidhaa hizi kutoka nchi jirani ya Kenya ambapo zitatozwa ushuru kwa kiwango cha 5% tu.

Mheshimiwa Spika, magari yanayotumika kusambazaia gesi hayana tofauti na magari yale yanayotumika kwa huduma nyingine kama vile ubeabajji wa mafuta ya petroli, *cement*, maji machafu na kadhalika. Kwa hiyo, sio rahisi kusamehe kodi kwenye magari hayo kwani kufanya hivyo kunaweza kutoa mwanya kwa wale ambao hawastahili kunufaika na msamaha huo. Hata hivyo bidhaa ya gesi imesamehewa ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa. Mheshimiwa Mntangi pia alitoa hoja kwamba ili kupunguza kasi ya upandaji wa bei za mafuta na petroli, kuna umuhimu wa kuoanisha viwango vya kodi kwa nchi zote za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, bei za mafuta ya petroli zinatofautiana kwa nchi zote za Afrika Mashariki. Hali hii imechangiwa na viwango tofauti vya kodi za ndani kwa kila nchi. Kwa mfano, kiwango cha kodi ya *VAT* kwa Tanzania ni 20% na 18% kwa Uganda. Vile vile kiwango cha ushuru wa bidhaa yaani *excise duty* vinatofautiana kwa kila nchi. Kwa hali hiyo, ni dhahiri kwamba tofauti hiyo ya viwango vya kodi za ndani itakuwa kichocheo cha kutofautiana kwa bei ya mafuta ya petroli. Kwa kuwa suala hili linahusu nchi tatu, mikakati inafanywa ili kuwasilishwa kwenye Sekretarieti ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kupatiwa muafaka.

Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini alitoa hoja kwamba Serikali ifute kodi ya mafuta kwa mashirika ya reli ili kuyawezesha kuimarishe kwa reli husika yaani *TAZARA* na *TRC*. Kodi ya mafuta hutozwa kwenye mafuta ya dizeli na petroli kwa madhumuni ya kutengeneza na kutunza barabara zetu ili kuzifanya ziwe za kudumu na kutumika kwa vipindi vyote vya mwaka.

Aidha, kodi hii imekuwa ikilipwa na magari yote ya kigeni yanayoingia nchini kwa madhumuni hayo hayo. Ni matumaini yetu kwamba barabara nzuri zitarahisisha usafirishaji wa bidhaa na watu hivyo kuwa kichocheo muhimu kwa ukuaji wa uchumi wetu. Chanzo hiki cha mapato kimekuwa kikichangia sehemu kubwa sana ya mapato yetu ya ndani katika ujenzi na uimarishejaji wa barabara zetu hapa nchini.

Aidha, usafiri wa barabara haushindani na reli bado unasaidia usafiri wa reli. Abiria na bidhaa hutegemea usafiri wa njia zote mbili kukamilisha safari. Hata hivyo Serikali inatambua mchango wa mashirika ya reli katika kukuza uchumi. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imefuta kodi ya *VAT* kwenye vipuri vyote vya treni katika mashirika haya. Pamoja na msamaha huo wa *VAT*, mashirika ya reli hayalipi ushuru wa forodha kwenye treni, mabehewa na vipuri vya aina zote kwa ajili ya treni na mabehewa hayo.

Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge wa Mwanza Vijiji, ametoa hoja kwamba Serikali imeondoa kodi kwenye *computer* lakini haijaondoa kodi kwenye *computer accessories* na *components*. Ili kuhamasisha matumizi ya teknolojia hii muhimu, Serikali

imeondoa kodi kwenye *computer* na *accessories* zake na sio *computer* peke yake. (*Makofi*)

Napenda kusitiza kuwa msamaha huo unahu su *computer* zenyewe, *outmatic data process machines* na *accessories* zake na sio mitambo mingine inayotumia mifumo ya *computer* yaani *computerized machines*.

Mheshimiwa Profesa Mbawala, Mbunge wa Namtumbo alitoa hoja kwamba Serikali ifikirie upya suala la kutoza kodi kwenye mafuta ya diesel kwa mabasi, matrektu na malori. Kodi ya ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya *diesel* hutozwa kwa sababu kuu mbili muhimu. Moja ni kufidia madhara yake kwenye mazingira na nyingine kuongeza mapato ya Serikali. Kwa misingi ya madhara yanayosababishwa kwenye mazingira kutokana na matumizi ya mafuta ya *diesel* bidhaa hii imekuwa ikitozwa ushuru wa bidhaa kama bidhaa za kimapokeo.

Mheshimiwa Spika, mafuta ya *diesel* huchangia zaidi ya 40% kwa mapato yote ya ushuru wa bidhaa utokanayo na mafuta. Kuondoa ushuru huu, kutasababisha pengo kubwa katika bajeti ya Serikali.

Hata hivyo, Serikali inatambua umuhimu wa mafuta ya *diesel* kama *input* muhimu ya uzalishaji. Kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali haijapandisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwa mafuta ya *petrol* na *diesel* kuanzia mwaka wa fedha 2000/2001 hata pale ambapo Serikali ilibadilisha viwango vya bidhaa nyingine ili kuendana na kasi ya mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mbunge wa Dole, alitoa hoja kwamba viwango vya kodi ya biashara kwa Zanzibar ni vema viangaliwe upya. Viwango vya kodi za biashara vinavyotumika Zanzibar hususan kwa kodi ya mapato na forodha hutumika pia bara. Kwa kuwa kodi hizi ni za muungano sio vizuri kuwa na sheria....

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, nilianza nimechelewa, sijui kama utanipa dakika chache zaidi ili nimalizie?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, hiyo ni kengele ya kwanza tu, endelea na mchango wako umalizie.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Ahaa, ya kwanza. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nh'unga alitoa hoja kwamba viwango vya kodi vya biashara kwa Zanzibar ni vyema viangaliwe upya. Viwango vya kodi za biashara vinavyotumika Zanzibar hususan kwa kodi ya mapato na forodha hutumika pia Bara.

Kwa kuwa kodi hizi ni za Muungano sio vizuri kuwa na sheria mbili tofauti ndani ya nchi moja.

Aidha, kwa upande wa Ushuru wa Forodha viwango vinavyotumika ni vile tulivyokubaliana katika Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki vitumike katika nchi zote tatu na kwa Afrika Mashariki. Sasa ni eneo moja la forodha. Kwa hiyo, itakuwa ni vigumu kwa Zanzibar kuwa na viwango tofauti vya ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Shirika la Meli za Maziwa linatumia fedha nyingi kununua vipuri na *VAT*, inakuwa ni mzigo mkubwa kwa Shirika hilo. Mashirika ya Meli hufanya biashara za kusafirisha abiria pamoja na mizigo. Mashirika hayo yamesajiliwa katika mfumo wa *VAT*. Kwa kuwa mauzo yanatokana na usafirishaji wa mizigo kwa Mashirika hayo, yanazidi kiwango cha usajili wa *VAT*. Kwa kuwa Mashirika hayo yamesajiliwa kwenye *VAT* hurejeshewa sehemu ya *VAT* iliyolipwa kwenye manunuvi ikiwa ni pamoja na yale ya vipuri. Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kwamba, *VAT* sio mzigo kwa Mashirika ya Meli.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba marejesho ya fedha za *VAT* ambazo wakulima wa kahawa hulipa katika vifungashio, magunia, gharama za kukoboa, kusafirisha na utunzaji wa kahawa kwenye maghala, Vyama vya Ushirika vinavyopeleka mazao ya biashara ikiwa ni pamoja na kahawa nje ya nchi vimesajiliwa *VAT* na hupewa marejesho ya fedha za *VAT* zilizotumika kwenye manunuvi ya bidhaa na huduma.

Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Mamlaka ya Mapato Tanzania imerejesha jumla ya Shilingi milioni 109.3 kwenye Vyama vya Ushirika vya Kagera, Kilimanjaro, Karagwe na Nyanza. Serikali inasisitiza kwamba kwa sababu za kiutawala, haiwezi kufanya marejesho kwa mkulima mmoja mmoja. Ni vyema wakulima wakajiunga na Vyama vya Ushirika ili waweze kunufaika na marejesho hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei kubwa ya bati na sementi, imejitokeza hoja kuwa baadhi ya bidhaa nchini zimeendelea kuwa na bei kubwa na mzigo kwa wananchi wa kawaida. Bidhaa zilizoongelewa ni pamoja na mabati na saruji. Napenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali imeshajitoa katika kupanga bei ya bidhaa mbalimbali na kwamba bei hizo sasa zinaongozwa na nguvu ya soko. Chini ya utaratibu huu, mzalishaji hupanga bei ambazo zitafidia gharama zake za uzalishaji ikiwa ni pamoja na kodi. Serikali haijapandisha kodi katika bati na saruji kwa zaidi ya miaka miwili sasa. Hivyo, bei zilizopo zinatokana na gharama nydingine za uzalishaji za bidhaa hizo na sio kodi inayotozwa na Serikali.

Serikali pia inatambua kuwa, hivi sasa inabidi mabati yasafirishwe kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma kwa njia ya barabara na hivyo kuongeza gharama na kusababisha kupanda kwa bei za bidhaa hiyo. Hata hivyo, kwa kutambua tatizo hilo, Serikali hivi sasa inafanya mkakati wa kukarabati reli hiyo na kurejesha hali ya usafirishaji wa bidhaa kama hizi kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inahusu bajeti kuwa tegemezi. Misaada na mikopo ya nje ni asilimia arobaini na moja ya bajeti yote mwaka 2004/2005 na 2005/2006. Mchango mkubwa wa ushirika wetu unatokana na mambo matatu:-

- (a) Mahitaji yetu makubwa ya kugharamia mipango ya kuondoa umaskini.
- (b) Dhamira ya Jumuiya ya Kimataifa kusaidia nchi maskini kupambana na umaskini kama alivyofafanua mgeni wetu tuliyekuwanaye hapa Bungeni juzi, Mr. Camdessus katika hotuba yake.
- (c) Washirika wetu kuridhika na mipango yetu ya kujiendeza.

Mheshimiwa Spika, chaguo lililo mbele yetu ni kama kuahirisha mipango yetu ya kuondoa umaskini mpaka tutakapoweza kujigharamia wenyewe au tukubali misaada ya washirika wetu na kuitumia vizuri kujenga uwezo wetu. Tumechagua kupokea misaada hiyo ili kuharakisha juhudzi za kukuza uchumi na kuondoa umaskini kwa mikakati endelevu.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya matumizi ya misaada vinapangwa na kusimamiwa na sisi wenyewe japo kwa kushauriana na washirika wetu wa maendeleo chini ya Mpango wa *Tanzania Assistants Strategy*. Mikopo ni ya masharti nafuu tu ndio tunayochukua na ndio tunao uwezo wa kuilipa.

Mheshimiwa Spika, pia ilitolewa hoja juu ya tofauti kati ya riba za kuweka na kukopa Benki kwamba ni kubwa. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Njelu Kasaka. Ni kweli kwamba kuna tofauti kubwa kati ya riba inayolipwa kwa amana na riba za mikopo inayotolewa na mabenki ingawa imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, tofauti kati ya riba za amana na riba za mikopo imepungua kutoka zaidi ya asilimia 14 mwezi Aprili, 2001 hadi kufikia chini ya asilimia 10 Mwezi Aprili, 2005. Ni vyema ikaeleweka kwamba ukubwa wa pengo hili unatokana na matatizo ya kimsingi katika uchumi wetu. Matatizo haya ni pamoja na miundombinu hafifu ambayo huongeza gharama za uendeshaji wa shughuli za kibenki, matatizo yanayoifanya ardhi isitumike kama dhamana ya mikopo, kwa mfano matatizo katika usajili wa nyaraka za mikopo, yaani *registration of title deeds*, matatizo katika utoaji wa *Court Injunctions* na kadhalika.

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Endelea umalizie *presentation* yako.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, ahsante. Vile vile kuna udhaifu katika kurejesha mikopo kwa baadhi ya wakopaji. Mambo haya yote husababisha riba za mikopo kuwa juu sana kuliko riba za amana.

Hata hivyo, Serikali ikishirikiana na Benki Kuu itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kibashara ili kuziwezesha Benki zetu kutoa riba zinazowiana na viwango vyatya riba vinavyotokana na soko huria.

Kulikuwa na hoja kwamba kwa nini Shilingi inaporomoka? Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Selelii, Mbunge wa Nzega. Katika kipindi cha miaka mitatu ya hivi karibuni thamani ya Shilingi ikilinganishwa na ile ya Dola za Kimarekani imekuwa ikipungua kwa asilimia ya wastani wa sita kwa mwaka. Kiasi ambacho ni cha kawaida katika hali ya uchumi wa Tanzania ikilinganishwa na uchumi wa nchi tunazofanyanazo biashara.

Hata hivyo, ikilinganishwa na thamani ya Shilingi ya Tanzania na ile ya Kenya utagundua kuwa Shilingi yetu imeimarika kwa asilimia 2.6 katika mwaka 2004 dhidi ya Shilingi ya Kenya kutoka Shilingi za Tanzania 13.97 kwa Shilingi za Kenya mwezi Desemba, 2003 hadi Shilingi 13.61 kwa Shilingi ya Kenya mwezi Desemba mwaka 2004. Kutokana na takwimu hizi, ni dhahiri kuwa thamani ya Shilingi imekuwa imara jambo ambalo linadhihirisha udhibiti wa sera za uchumi zinazosimamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja na Mheshimiwa Mwakipesile kwamba kiasi cha akiba ya fedha za kigeni na mchanganuo wake ueleweke. Jibu lake ni kwamba, akiba ya fedha za kigeni ni jumla ya fedha zote za kigeni zinazobadilishika, yaani *convertible foreign assets* zinazotunzwa na Benki Kuu kwa niaba ya Serikali. Benki Kuu hupata fedha hizi kwa njia mbili:-

- (a) Kununua kutoka soko la fedha za kigeni nchini.
- (b) Kununua sehemu ya misaada na mikopo ya Serikali kutoka nje.

Fedha zilizonunuliwa au kuuzwa na Benki Kuu katika soko la fedha za kigeni zipo na zikihitajika tutazitoa. Kuna jedwali ningeweza kulisoma, lakini litachukua muda na muda wenyewe umekwisha.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwa nini Benki hazikopeshi kwa kiwango cha kuridhisha. Hii ilikuwa ni hoja ya Mheshimiwa Kasaka, Mbunge wa Lupa. Ni kweli kwamba mikopo inayotolewa na mabenki ya biashara nchini bado ni ya kiwango cha chini ikilinganishwa na matarajio ya wadau wa mikopo nchini. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni mikopo ya mabenki imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa kufuatia hatua mbalimbali zinazozidi kuchukuliwa na Serikali kuboresha mazingira ya utendaji katika sekta binafsi ikiwemo sekta ya fedha na mabenki.

Kwa mfano, mikopo ya mabenki kwa sekta binafsi iliongezeka kwa wastani wa asilimia 39 katika kipindi cha miaka mitatu iliopita. Kwa mwaka unaoishia Juni, mwaka jana peke yake mikopo ya sekta binafsi iliongezeka kwa asilimia 47 kufikia Shilingi bilioni 966. Kiwango hiki ni sawasawa na asilimia 86 ya jumla ya mikopo yote nchini. Wakati huo kiasi cha mikopo kwa Serikali kutoka sekta ya mabenki imepungua kutoka asilimia 30 mwezi Juni, 2002 hadi kufikia asilimia 14 mwezi Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana kwa kunisikiliza na napenda kwa niaba ya Serikali, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote walioipongeza *TRA* kwa kazi nzuri inayoifanya. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Honorable Members, before I call on the other Deputy Minister for Finance to make his contribution, I would like to recognize and welcome the presence in the gallery of the British Minister for Africa, the Honourable Lord David Tracemans. He is accompanied by his Private Secretary Mr. Baraty Joshi, the British High Commissioner to Tanzania and other Members of the British High Commission.

They have visiting Tanzania on a variety of missions, the main mission being Lord Tracemans address to Members of Parliament this afternoon, and thereafter he is traveling to Zanzibar immediately after his address to Members of Parliament. He will spend the whole of tomorrow in Zanzibar, meeting with the President of Zanzibar and other Leaders in Zanzibar, including the Secretary General of the Civic United Front (CUF). Most welcome Lord Tracemans. (Applause)

Sasa namwita Naibu Waziri wa Fedha mwingine, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, naye atoe mchango wake na muda ni huo huo wa nusu saa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, nami napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi, kutoa pole kwa ndugu zetu wa Jimbo la Kilombero kwa kufiwa na Mbunge wao kipenzi Mheshimiwa Abu Kiwanga. Naungana na wenzangu kuomba roho ya Marehemu iwekwe mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa wanachama wa Chama cha Mapinduzi walioteuliwa kupeperusha bendera ya Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba mwaka huu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje. Pia, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuwa mgombea mwenza na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kugombea Urais wa Zanzibar. Ni matumaini yetu kuwa Chama chetu kitapata ushindi wa kishindo katika uchaguzi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili hotuba ya bajeti kwa mwaka 2005/2006 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa miradi, hoja ambayo imeletwa na Mheshimiwa Njelu Kasaka - Mbunge wa Lupa, Mheshimiwa Mwakipesile - Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Mrope - Mbunge wa Masasi na Mheshimiwa Profesa Mbilinyi - Mbunge wa Peramiho. Waliishauri Wizara ya Fedha ikagine miradi inayotekelizwa na Serikali nchini. Napenda kulifahamisha Bunge hili Tukufu kwamba, Wizara ya Fedha ina utaratibu wa kukagua miradi kila mwaka wa fedha. Ukaguzi unaofanywa na Wizara yangu umegawanyika katika maeneo mawili muhimu.

Katika eneo la kwanza, Wizara hulinganisha hali ya utekelezaji wa mradi na ratiba ya utekelezaji, yaani *action plan* kwa mradi huo. Ukaguzi wa aina hii huwezesha Wizara ya Fedha kufahamu kama miradi inatekelezwa kulingana na ratiba na fedha zilizoidhinishwa au la. Pia, katika hatua hii miradi hukaguliwa sehemu inapotekelezwa ili kulinganisha taarifa za utekelezaji zilizowasilishwa na Wizara za Kisekta na hali halisi ya utekelezaji kwenye eneo la mradi.

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya pili ya ukaguzi wa miradi, Wizara ya Fedha imeunda Kitengo Maalum cha *Technical Audit*. Kazi kubwa ya Kitengo hiki ni kuhakikisha kwamba Serikali inapata thamani kwa fedha zilizotumika (*value for money or expenditure tracking*). Kitengo kina wataalam wenyewe uwezo wa kufanya kazi hii kwa ufanisi. Hata hivyo, Wizara ya Fedha inachukua hatua za kuimarishe kitengo hiki kwa kushirikiana na wadau wengine ili kazi ya ukaguzi wa miradi ifanyike kwa ufanisi na kwa miradi minge zaidi kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/05, Wizara ya Fedha ilikagua miradi katika Mikoa ya Rukwa, Tabora, Shinyanga, Morogoro, Mtwara, Lindi, Kagera, Manyara, Arusha, Dodoma, Tanga na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu mikopo ya nyumba ambayo Waheshimiwa wengi walichangia katika hili. Wizara imeanza kutoa huduma katika jambo hili ingawa kwa kiwango kidogo kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 16 wa hotuba ya bajeti ya Waziri wa Fedha. Lengo ni kuboresha mazingira ya kisera na kisheria ili mabenki yaliyopo yatoe mikopo ya ujenzi na kuwezesha uanzishaji wa vyombo vipyta vya kutoa mikopo ya sekta binafsi. Uchambuzi wa awali umeonyesha kwamba, mambo muhimu ni:-

Kwanza, taratibu za usajili wa miliki ya ardhi na kubadilisha miliki hizo na pili uwezo wa Mahakama kumaliza mashauri ya ardhi kwa haraka. Lakini bado ufumbuzi wa masuala haya unashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja hasa kutoka kwa Mheshimiwa Mwanne Mcemba, kuhusu Vituo vya Afya na Zahanati zilizojengwa kwa nguvu ya wananchi kushindwa kutoa huduma kwa kukosa wafanyakazi na vitendea kazi. Ujenzi wa Vituo vya Afya na Zahanati kwa nguvu za wananchi hutokana na Sera ya Serikali ya kuwataka wananchi washiriki katika mipango ya maendeleo yao. Utekelezaji wa miradi hii unahuisha wananchi, Halmashauri na Serikali katika ngazi ya Wilaya, Mikoa na hatimaye Taifa. Miradi hii inapokamilika, Serikali huwajibika kuandaa utaratibu wa kujumuisha katika mfumo wa Serikali ili wananchi waanze kupata huduma kutoana na miradi yao. Miradi ya Zahanati na Vituo vya Afya inapokamilika, utaratibu unaotumika ni kama ifuatavyo:-

Kijiji au Wilaya husika kupitia Mganga Mkuu wa Wilaya *DMO* huwasilishwa kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, taarifa ya Zahanati au Vituo vya Afya vilivyokamilika. Pili, Mkoa husika huwasilisha mahitaji ya madawa kwa Wizara ya Afya ili mahitaji hayo

yajumuishwe katika bajeti ya mwaka ya Wizara ya Afya. Kwa mfano, kwa mwaka 2004/2005, Vituo vya Afya 36 na Zahanati 526 zimepewa mgao wa masanduku ya dawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, taarifa hii itakuwa katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Afya kwa mwaka 2005/2006. Kwa upande wa mahitaji ya watumishi, Halmashauri za Wilaya kupitia Ofisi ya *DMO* na Mkuu wa Mkoa hutakiwa kupata idhini ya ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Baada ya kupata kibali cha ajira, mahitaji ya watumishi wapya pamoja na gharama za vitendea kazi huletwa Hazina wakati wa kuandaa bajeti ya Serikali ya mwaka. Hata hivyo, matatizo yaliyojitekeza kuhusu suala hili ni pamoja na:-

Kwanza, taarifa za kukamilika kwa miradi hiyo kutofika Wizara ya Afya na pia sehemu kwa wakati. Pili, upungufu wa watumishi wenye taaluma za kufanya kazi katika hospitali na hivyo kusababisha baadhi ya Zahanati na Vituo vya Afya kuwa na watumishi wachache kuliko inavyotakiwa. Tatu, Serikali bado itachukua hatua kurekebisha kasoro hizo. Lakini hata hivyo, Wizara ya Afya kwa mwaka 2005/2006, itafungua Zahanati zaidi ya 500 mpya na Vituo vya Afya zaidi ya 40 na haya yatafafanuliwa kwa upana zaidi na Mheshimiwa Waziri wa Afya wakati atakapotoa hotuba yake ya bajeti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa na hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa Profesa Maghembe kuhusu fedha za wanafunzi wenye sifa ili waendelee hata wamalize Elimu ya Vyuo Vikuu. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, bajeti ya mwaka 2005/2006, Serikali imechukua hatua madhubuti ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wengi zaidi wenye sifa za kuijunga na Elimu ya Juu wanapata nafasi za kuijunga na Vyuo hivyo. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuongeza bajeti ya matumizi ya kawaida ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kutoka Shilingi bilioni 70.9 mwaka 2004/2005 hadi Shilingi bilioni 111.1 mwaka huu wa 2005/2006. Hili ni ongezeko la asilimia 56. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo, fedha za ndani, Serikali imeongeza bajeti ya Wizara hiyo kutoka Sh.1,300,000,000/= mwaka 2004/2005 hadi Sh.10,401,000,000/= ikiwa ni ongezeko la asilimia 700. Naamini kuwa ongezeko hili la fedha litakwenda sambamba na ongezeko la idadi ya wanafunzi kuijunga na Vyuo Vikuu. Serikali itaendelea kuongeza bajeti hii mwaka hadi mwaka kwa kutimiza lengo hilo hilo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ambayo ililetwa na Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, Mbunge wa Mlandege kwamba bajeti ya mwaka 2005/2006 imetenga fedha kwa ajili ya uamuvi wa kuongeza idadi ya wanafunzi katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Je, Serikali itasaidiae wanafunzi walioko Dekondari huko Zanzibar ili idadi iongezeke kuingia Vyuo vya Elimu ya Juu kwa sababu Zanzibar haina mpango wa MMES?

Pamoja na kuwa jukumu la kuimarisha Elimu ya Sekondari huko Zanzibar si la Serikali ya Muungano, Serikali zote mbili kupitia Wizara ya Fedha zimekuwa zikishirikiana kuboresha Sekta ya Elimu huko Zanzibar. Kwa mfano, katika utekelezaji

wa Zanzibar *Poverty Reduction Plan*, Wizara ya Fedha imefanikisha upatikanaji wa fedha kutoka *USAID*, *SIDA*, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na *BADEA* kutekeleza miradi na *program* mbalimbali ya Sekta ya Elimu kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Yussuf Juma Kombo alikuwa na hoja kwamba kwa kuzingatia mambo ya Muungano itakuwa vizuri wakati tunavyopata misaada kutoka nje tukae pamoja na tupange nini tupeleke wapi. Serikali ya Muungano na ile ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekuwa zikichukua hatua mbalimbali za kufufua na kuimarishe uchumi kwa lengo la kutokomeza umaskini ikiwa ni pamoja na kuandaan mipango na mikakati ya kuleta maendeleo, kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Mipango ya mikakati hii ndio inayoongoza juhudhi zote za nchi ikiwemo mahitaji na matumizi ya rasilimali za ndani na nje katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar kuna Mpango wa Zanzibar wa Kupunguza Umaskini (*Zanzibar Poverty Reduction Plan –ZPRP*) na kwa upande wa Bara kuna Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Mipango na mikakati hii inaonyesha mahitaji ya rasilimali zinazohitajika katika utekelezaji wake. Kutokana na rasilimali za ndani kutotosheleza mahitaji haya misaada na mikopo huchangia ili kutekeleza kwa kikamilifu mipango hii. Hivyo, kukaa pamoja na kuangalia maeneo ya kuelekeza pindi tupatapo mahitaji na utekelezaji wa mikakati niliyokwishaezea hapo juu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanapaswa kushiriki kikamilifu wakati wa uandaaji wa mipango na mikakati ya maendeleo ya nchi kwani ndio mwongozo wa ugawaji wa fedha zote za ndani ya nchi na kwa hili Serikali ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuititia Wizara ya Fedha huwa tunashirikiana kikamilifu katika kuhakikisha kwamba rasilimali hizi au yale yote ambayo yamewekwa katika mikakati hii yanatekelezwa kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja juu ya hatua ya kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya muda wa kati na mrefu. Hoja hii ililetwa na Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Mtangi, Mheshimiwa Bendera na Mheshimiwa Rhoda Kahatano. Hatua zinachukuliwa chini ya mpango wa Awamu ya Pili ya mageuzi katika Sekta ya Fedha, yaani *Second Generation Financial Sector Reforms* na hatua hizi ni pamoja na kwanza kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo, Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya Maendeleo, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kukopesha kuititia mabenki ili kuwezesha mabenki kutoa mikopo ya muda mrefu, Mfuko wa Ukopeshaji wa Vifaa ambaa nitauelezea hapo baadaye kwa urefu na mabenki kutoa mikopo ya nyumba yaani *Housing Finance*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Maendeleo, tayari Serikali imefanya uchambuzi na kuridhika kwamba *TIB* irekebishwe na kuwa Benki ya Maendeleo. Pili, utekelezaji utajumuisha kuiongezea *TIB* mtaji na tatu, mashauriano na wadau wote yamekamilika tayari kwa uamuzi wa mwisho wa Serikali ambaa utapatikana baada ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu Mfuko wa Dhamana kwa Mikopo ya Maendeleo (*Development Financial Grant Facility*). Uchambuzi kuhusu kanuni na taratibu za Mfuko huu zimeshakamilisha, Mfuko huu utasimamiwa na Benki Kuu kwa kuanzia. Mfuko utadhamini mabenki kwa ahadi ya asilimia 50 yatakapotoa mikopo na Mfuko utaanza kazi katika mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Ukodishaji wa Rasilimali kama yalivyo maelezo ya hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Ibara ya 18, ukurasa wa 19 mkakati unashirikisha Serikali ya Tanzania, Serikali ya Switzerland na *International Finance Corporation (IFC)*. *IFC* imeanza kwa mpango uliozinduliwa mwezi Mei, mwaka huu 2005. Tumeajiri mtaalam mshauri wa kutafiti vizingiti vya sheria na kisera vile vya kushamiri kwa biashara ya kukopesha vifaa. Unaposema ukodishaji wa rasilimali za kibiasara, una maana gani?

Huu ni mfumo mbadala wa ukopeshaji ambapo mkopeshwaji hupatiwa rasilimali badala ya fedha tasilimu. Ukopeshaji huo unahusu Mkataba kati ya mkopeshaji na mkopeshwaji ambapo rasilimali husika inakodishwa kwa mkopeshwaji ili itumike kwa kipindi na kwa malipo maalum ambayo pande hizo mbili zinakubaliana. Hakutakuwa na haja ya dhamana au *collateral*. *Collateral* yako ni ile mali uliyokodishwa ambapo hapo utakapomaliza malipo yake, mali ile baadaye inakuwa yako mwenyewe.

Kwa hiyo, huu ndiyo mfumo rahisi kabisa wa wakulima wadogo wadogo, wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati na una kiwango cha kukopa mpaka kiasi cha thamani ya Shilingi milioni 200 ya ile rasilimali utakayotaka kuitumia. Inaanzia hata katika mzinga wa nyuki hata unaweza kufika pengine trekta au kitu fulani kingine chochote kile, lakini ilimradi ukamilishe yale masharti yaliyowekwa na hii *liasing system* ambayo inaendeshwa na rasilimali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo zaidi mnaweza kufika pale ghorofa ya nne ya Jumba la Milambo Ofisi ya *IFC* watakupa maelezo kamili na wahusika na wapeperushi kuhusu mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa na hoja kuhusu vyanzo vya mapato kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Pia, napenda kutoa ufanuzi kuhusu vyanzo vya mapato kwa miradi ya maendeleo. Kwa kawaida miradi ya maendeleo inagharamiwa kwa fedha kutoka nje na fedha kutokana na vyanzo vya kodi na visivyo vya kodi. Kwa mwaka huu wa fedha, fedha za ndani kwa miradi ya maendeleo ni Shilingi bilioni 370, zinatokana na mapato ya kodi ya Shilingi bilioni 255 na mikopo isiyo ya Mabenki ya Shilingi bilioni 115. Kwa hiyo, mapato haya yote ya Shilingi bilioni 370 ni sawa na asilimia 18 ya mapato yote ya ndani ya Shilingi trilioni mbili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TIB* kama nilivyoelezea hapo awali azma ya Serikali ya kuimarisha Benki ya Rasilimali (*TIB*), ili iwe Benki ya Maendeleo bado iko pale pale. Serikali itahakikisha inaimarisha Benki hii kwa kuongeza mtaji ili kuwezesha kutoa mikopo ya maendeleo ya muda wa kati na muda mrefu kwa ajili ya uwezekaji katika miradi mikubwa na midogo ya maendeleo kiuchumi. Hata hii itasaidia katika kuziba

pengo lililopo hivi sasa la upatikanaji wa mikopo bila urasimu na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji uchumi na kuondoa umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba pamoja na kuondolewa kwa kodi kwa mishahara ya kima cha chini hivi karibuni, mishahara hiyo ingepandishwa kufikia Sh.80,000/. Mishahara ya Watumishi wa Serikali imekuwa ikiboresha na Serikali, mara kwa mara kulingana na upatikanaji wa fedha. Kama ilivyokuwa kwa mwaka 2004/2005 mishahara kwa Watumishi wa Serikali kwa mwaka 2005/2006 inategemewa kurekebishwa pia. Ni matumaini yangu kuwa Wizara inayohusika itazingatia ushauri wa Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, kuhusu suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Tanzania imefanikiwa kwa kiasi gani malengo ya *millennium* 2005 na hatua zipi zitumike hasa baada ya kusamehewa madeni yake kama ilivyotangazwa hivi karibuni. Azma ya Serikali ni kutekeleza malengo ya *millennia* baada ya mwaka 2015 bado iko pale pale. Mpango wa MKUKUTA ulioanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2005/2006 una lengo la kuongeza kasi zaidi ya kufikia malengo ya *millennia* kwa kuhusisha sekta zote. Aidha, mgao wa rasilimali nao umezingatia MKUKUTA. Ikumbukwe hapa kuwa, fedha zinazoelekezwa katika kutekeleza MKUKUTA zimetokana na mapato ya ndani. Mapato kutoka nje ikiwa ni pamoja na misamaha ya deni, hivyo uamuvi wa hivi karibuni wa nchi tajiri sana duniani pamoja na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa utaiongezea zaidi uwezo Serikali na kuelekeza fedha katika maeneo muhimu chini ya MKUKUTA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya Wabunge wengi sana, kuhusu Bajeti ya Sekta ya Kilimo kwamba ni ndogo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imekuwa ikitoa kipaumbele kinachostahili kwa Sekta ya Kilimo na itaendelea kufanya hivyo hasa ikizingatiwa mchango mkubwa wa sekta hiyo. Sio tu katika kulipatia Taifa fedha za kigeni, bali pia kutoa ajira kwa wananchi walio wengi. Nikumbushe tu kwamba, Sekta ya Kilimo ni moja ya sekta chache zilizopewa kipaumbele katika mpango wa kupunguza umaskini ambao unamalizika mwishoni mwa mwezi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unaweza ukaona kwamba Bajeti ya Sekta ya Kilimo ni ndogo kama utaangalia Bajeti ya fungu 43 Wizara ya Kilimo na Chakula pekee. Lakini ukitaka kupata Bajeti sahihi ya Sekta ya Kilimo, inabidi pia uchambue Bajeti za mafungu yafuatayo ambayo yana fedha kwa ajili ya Sekta ya Kilimo nayo ni:-

- (i) Wizara ya Ushirika na Masoko;
- (ii) Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo;
- (iii) Wizara ya Ujenzi barabara Vijijini ambazo husaidia Sekta ya Kilimo;
- (iv) Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mikoa; na
- (v) Halmashauri za Miji na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo pia hunufaika na mifuko mbalimbali ambayo inadhaminiwa na Serikali ikiwemo pamoja na *export guarantee scheme*.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu matumizi ya kawaida kwamba yametengewa fedha nyingi kuliko matumizi ya maendeleo. Waheshimiwa Wabunge, wengi vile vile walichangia hoja hii. Uchambuzi wa kina wa matumizi ya kawaida unaonyesha kwamba kama uwezo wa Serikali ni mdogo, basi siyo jambo baya kuwa na Bajeti kubwa ya matumizi ya kawaida. Ikumbukwe kwamba matumizi ya kawaida ni pamoja na deni la Taifa, ambalo ni lazima lihudumiwe ipasavyo. Matumizi ya kawaida pia ni pamoja na mishahara ya Watumishi wa Serikali ambayo Waheshimiwa Wabunge, watakubaliana nami kwamba bado ni midogo ikilinganishwa na gharama za maisha. Kwa hiyo, ni busara kuongeza sehemu hii ya matumizi ya kawaida. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la muhimu zaidi ni kuzingatia ukweli kwamba Bajeti ya kawaida hutumika kuhudumia miradi ya maendeleo iliyokamilika. Serikali inapokamilisha ujenzi wa madarasa, basi ni lazima iwepo Bajeti ya kutosha ya kawaida ili kulipa mishahara ya Walimu, kununulia vitabu, chakula cha wanafunzi na kadhalika kama wengi wenu Waheshimiwa Wabunge mlivyoshauri iongezwe.

Hivyo hivyo, tunapokamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya, basi lazima matumizi ya kawaida yagharamie ununuvi wa madawa. Kama vile Mheshimiwa Mchemba alivyoleta malalamiko yake ya Zahanati 21 ambazo sasa zinataka kufunguliwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, izingatiwe pia kuwa katika Sekta ya Kilimo kwa mfano fedha za kupambana na wadudu au ndege waharibifu hutengwa katika Bajeti ya matumizi ya kawaida. Serikali itaendelea kutenga fedha zaidi kwa Bajeti ya maendeleo kwa kuzingatia mapato ya Serikali, uwezo wa kutekeleza Miradi ya Maendeleo na uwezo wa kuhudumia miradi hiyo pindi inapokamilika. Serikali imeendelea kutenga fedha zaidi kwa ajili ya Bajeti ya maendeleo kama ifuatavyo:-

Bajeti imeongezeka kutoka Sh.803,420,000,000/= mwaka 2003/2004 hadi Sh.1,091,591,000,000/= mwaka 2004/2005 ongezeko la zaidi ya asilimia 35.8. Pia, Bajeti hiyo imeongezeka na kufikia Sh.1,385,183,000,000/= kwa mwaka huu fedha 2005/2006 na hili ni ongezeko la asilimia 26.9.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kunisikiliza na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mtoa Hoja ya kwanza, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, ye ye amenikabidhi nakala ya mchango wake kwa maandishi. Sasa nitawaruhusu wahudumu wagawe nakala hizi kwa Waheshimiwa Wabunge ili wawze kwenda sambamba na Mheshimiwa Waziri wakati anasoma mchango wake. (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia maoni mbalimbali yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba zetu mbili. Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji na ile Wizara ya Fedha. Wapo waliochangia kwa kauli na wapo waliochangia kwa maandishi. Nina hakika kwamba mchango wote uliotoka kwa

Waheshimiwa Wabunge, utathaminiwa na Serikali ya sasa na vile vile Serikali ya Awamu ya Nne ambayo bila shaka yoyote ile itaongozwa na CCM. (*Makofi*)

Hoja zilizotokea ni nyingi sana na nina hakika kama nitazijibu zote, muda hautatosha kwa sababu Wabunge waliochangia ni 84 na ukichukua wastani wa hoja tatu kila Mbunge ni hoja nyingi sana. Kwa hiyo, nilichofanya tumetoa kabrasha ambalo lina hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge na hapa nitakuwa nikigusia sehemu ambazo nadhani ni muhimu zilizojitokeza katika kuchangia hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijaendelea naomba nianze kuwatambua Wabunge wote waliochangia hapa Bungeni kwa kuzungumza. Kwanza ni Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Suleiman A. Sadiq, Mheshimiwa Abdula S. Lutavi, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa John Mwakipesile na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Dr. Amani W. Kabourou, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Athumanji Janguo, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Talala Mbise na Mheshimiwa Philip Marmo (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mheshimiwa Kidawa Saleh, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa George Mlawa na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Juma N'hunga, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Hashim Sagaf, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu na Mheshimiwa Abdisalam Khatibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Khalifa

Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Juma S. N'hunga, Mheshimiwa Mwanaidi Makame, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na mwisho Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana Manaibu Mawaziri wa Fedha ambao wamechangia maeneo ambayo tunaweza kusema ni mtambuka yanagusa maeneo yote mawili kwa maana ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Waziri wa Fedha na wataalam wake wote kwa ushirikiano mzuri tuliokuwa nao katika kipindi cha miaka mitano kilichokwisha. Uhusiano wetu mzuri kati ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji ndiyo umetuffikisha hapa pamoja na kutegemea uongozi wa pamoja wa Serikali nzima ya Chama cha Mapinduzi. Aidha, tunamshukuru sana Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kazi kubwa, nzuri na ya kutukuka kwa mchango wake mkubwa katika Taifa hili kwa kukuza uchumi. Ametuongoza vizuri, anasimamia vizuri *reforms*, anaiweka Tanzania katika sura ya Dunia, madeni yamesamehewa chini ya *HIPC* na sasa *World Bank*, *ADB* na *IMF* imetufutia madeni kutupa afueni ya kuhudumia deni la Taifa. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa mchango wake mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu na mipango yetu imetuonyesha kwamba uchumi wetu unaendelea vizuri, maana yake inabidi tukazane na *reforms* za kiuchumi, za kijamii, za kisera, za kisiasa na hata za kisheria. Tukiendelea na *reforms* hizi maana yake ni kwamba mafanikio yaliyopatikana hivi sasa katika uchumi wetu tutayalinda. Tumeona kwamba vigezo vyote vya uchumi kwa jumla vinaendelea vizuri. Pato la Taifa linakua, sasa kwa asilimia 6.7, mfumko wa bei tunaudhibiti vizuri, ukusanyaji wa mapato unaendelea vizuri, vile vile hata utegemezi wa Bajeti yetu unapungua.

Mwaka 1995 utegemezi wa Bajeti yetu ulikuwa asilimia takribani 60 na zaidi lakini sasa hivi tumefikia asilimia 41. Kwa kweli hii ni dalili nzuri. Wananchi waliokuwa wanaishi chini ya mstari wa umaskini (*poverty line*) walikuwa ni asilimia 38 mwaka 1991 na hivi wanafikia asilimia kama 35. Wenzetu wa Malaysia watu wanaoishi *below poverty line* ni asilimia tatu. Kwa hiyo, tuna kazi kubwa. (*Makofi*)

Kama tulivyokubaliana hapa Bungeni kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge, karibu wote inabidi tufanye kazi kubwa ya kutekeleza mikakati tuliyokwishaipanga pamoja na MKUKUTA. Nadhani tukishirikiana na Serikali na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na wananchi kwa ujumla mafanikio yatapatikana. Tahadhari ambayo lazima tuwe nayo ni kwamba hatuwezi kuitegemea sana Serikali kuzalisha mali kwa sababu Serikali yenyewe vile vile ni *cost centre*, kuna gharama kubwa sana za kuendesha Serikali.

Kwa hiyo, badala yake sisi Watanzania wote hatuna budi kufanya kazi kwa bidii na maarifa na kwa nidhamu kubwa ili tujiletii maendeleo yetu pamoja na kukuza uchumi wa nchi. Nadhani kazi kubwa ya Serikali itakuwa ni uwezeshaji wa wananchi kama

tulivyochangia hapa Bungeni ili tuibue fursa za kiuchumi zilizopo pamoja na kudumisha utawala bora wa kisheria, amani, usalama na utulivu, jukumu ambalo Serikali ya CCM imelimudu ipasavyo kama Waheshimiwa Wabunge wote walivyosema katika kuchangia Bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunazo changamoto. Kwanza bado tuna changamoto kubwa ya kukuza uchumi kwa kutumia kikamilifu rasilimali tulizonazo, huu ndiyo ujumbe uliojitokeza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Matumizi ya tija na ufanisi wa rasilimali hizi yatatokana na kufanya kazi kwetu kwa bidii, nidhamu na ufanisi kwa kila mmoja wetu. Hili ni muhimu sana linawagusa wakulima, wafanyakazi, sekta binafsi, karibu kila kitengo pamoja na Serikali yenyewe. (*Makofi*)

Pili, inabidi tuondokane na dhana ya kufikiria kuwa sisi si maskini kwa vile tunazo rasilimali. Wakati mwingine tunaweza tukazungumza tukisema rasilimali nyingi tunazo, utajiri tunao, lakini hizi rasilimali tulizonazo ndizo zile wataalam kama *De Sotto wanaziita* (*dead capital*), rasilimali mfu. Rasilimali tulizonazo ni lazima tuzibadilishe ziwe fedha au utajiri ili tuzitumie. Bila ya kufanya hivyo, tutakuwa tunapiga kelele bila faida. Tutakuwa tunashabikia *dead capital* ambayo haitatusaidia. (*Makofi*)

Tatu, ipo haja ya makusudi kuendeleza utaratibu wetu tuliokwishauanza wa kuhamishia mafanikio yetu ya uchumi mkuu, uchumi wa jumla ili iwafikie wananchi Vijijini na Mijini, mwananchi mmoja mmoja hasa tukizingatia kuwa tumejitahidi sana kuanza kushambulia umaskini usiyo wa kipato.

Mheshimiwa Spika, jitihada zilizofanyika kwenye uchumi mkuu na kuboresha huduma za jamii hususan Shule, maji, afya na baadhi ya miundombinu, ni utaratibu mmojawapo ambapo uchumi wetu unajaribu kusaidia wananchi mmoja mmoja lakini katika kupunguza umaskini usiyo wa kipato. Tumeondoa kodi zenye kero nyingi na hata katika hotuba yetu ya Bajeti, vivutio vingi vimetolewa katika Sekta ya Kilimo. Yote hii ni kuonyesha jitihada ya Serikali za kumpunguzia mwananchi mzigo kwa maana ya kupunguza umaskini usio wa kipato. (*Makofi*)

Lakini kazi kubwa tuliyonayo mbele yetu ni ile ya kuhakikisha kuwa uchumi unahamia katika umiliki wa wananchi walio wengi. Hili ni eneo ambalo limegusiwa na Wabunge wengi, pamoja na lile la kuona kwamba je, Mtanzania mmoja mmoja anafaidikaje na kukua kwa uchumi huu.

Tulitakiwa tuandae *roadmap* ya kuelezea tutafikaje katika umilikishaji wa uchumi wetu kwa Watanzania ifikapo mwaka 2025. Nadhani Serikali imeshaanza taratibu hizo. Tumezindua Sera ya Uwezeshaji ambayo itawalenga wananchi walio wengi. Tunao mkakati wa kurasimisha rasilimali na biashara Tanzania ambao Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Mama Anne Makinda na aliutolea maeleo jana, nia yake ya kusaidia wananchi wa kipato cha chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunao mkakati wa kuharakisha maendeleo ya Tanzania hii yote ikifanya kazi kwa kusaidiana na mkakati wa kupunguza umaskini. Mikakati yote hii

tukiiangalia kwa karibu na msukumo wake, kwa kweli inalenga kuhakikisha kwamba Watanzania wanaelekea katika kumiliki uchumi. Lakini vile vile pamoja na mikakati tunazo sera kadhaa ambazo nyingi zimepitishwa na Bunge lako Tukufu. Kuna sera za kuendeleza biashara kubwa, za kati na ndogo; kuna sera za mikopo midogo na vyote hivi tukivifatilia kwa vizuri zaidi vinalenga katika kupunguza umaskini wa kipato kwa wananchi wetu. Kazi kubwa ni kufanya kazi kwa bidii kwa juhud, kwa nidhamu kuhakikisha kwamba mipango hii mizuri na mikakati hii mizuri tunayojiwekea tunaitekeleza kwa tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sisi sote Wabunge, tunakubali kwamba hii mikakati si miujiza ambayo itafanya kazi yenye wakati sisi tunasubiri. Mikakati hii itahitaji sisi wenyewe tujitume kwa kufanya kazi kwa bidii na nidhamu kubwa ili tuweze kufanikisha. Mikakati hii inahitaji tufanye kazi kwa bidii, inahitaji tuguse maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge, wameyataja, kama uboreshaji wa elimu, Elimu ya Ufund Stadi na Elimu za Ufund, ku-*organize* vikundi mbalimbali, kuona kwamba muda mwangi unatumika katika kujituma kufanya kazi.

Sisi tunaelewa kwamba hapa duniani nchi inayoongozwa kwa *suicide* ni Japan, lakini Wajapani wana-*commit suicide* (wanajiu) sio kwa sababu nyingine yoyote ile, lakini ni kwa sababu ya kushindwa kazi. Mjapani anaposhindwa kazi kwa nidhamu ya hali ya juu yeye anajitoa uhai wake. Tunataka tuingie katika utaratibu wa kujua kazi, lazima tuifanye kwa juhud kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo kwa kweli nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, wote ambalo tunatakiwa tulifanyie kazi kwa nguvu sana ni Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo kwa kweli ni lazima tuifanyie kazi kubwa sana. Mimi nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha ameeliteza ni vipi tutaweza kuichanganua Bajeti na kujua kwamba Sekta ya Kilimo, imepata fedha kiasi gani. Ukichukua Sekta ya Kilimo yenye bila ya kuchukua zile Sekta ambazo zinainsidia Kilimo, tunaweza tukafikiria kwamba kilimo kimetengewa fedha ndogo. (*Makof*)

Lakini kwa kilimo kimepewa umuhimu, sasa kazi kubwa kama Waheshimiwa Wabunge wengi walivyosema, ni jinsi ya kutekeleza taratibu ambazo tumejiwekea katika sekta hizi. Lakini nina hakika kwamba tukijitahidi sana katika Sekta ya Kilimo pamoja na miradi ya umwagiliaji maji, tunaweza kuongeza pato letu la Taifa kwa kiwango kikubwa sana. Hata kile kiwango tunachokitoa cha asilimia 10 kwamba uchumi wetu ukue asilimia 10 na tunaupa muda mrefu, tukifanya kazi hiyo kwa bidii kiwango hicho tunaweza kukikuta kwa muda mfupi sana kama walivyofanya wenzetu wa Msumbiji. Lakini tunatakiwa kwa kweli tufanye kazi kwa bidii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo la Sekta ya Uvuvi. Sekta ya Uvuvi na Utalii ni lazima nazo tuziangalie kwa karibu. Mtando wa zana za kilimo, pembejeo, masoko na barabara hasa Vijijini havina budi kuimarishwa. Hii ni michango kwa kweli imetolewa karibu na Waheshimiwa Wabunge wengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ambalo tutakuwa tunalisahau lakini lazima tulifanyie kazi na limejitokeza katika uchangiaji wa Bajeti yetu ni uboreshaji wa miundombinu. Hili ni eneo litakalopunguza kwanza gharama za uzalishaji; pili, gharama za biashara na tatu kuondoa gharama za uchumi na ughali wa maisha hasa kwa wananchi wa kawaida. Bado tunahitaji kuwa na msimamo na mwelekeo mzuri wa kuona tunaboresha barabara zetu za Vijijini ili kuwahakikishia wakulima wanaweza kutoa mazao na kwenda kuyaiza na kuboresha usafiri.

Katika eneo hili, Waheshimiwa Wabunge wote tunakubali kwamba Halmashauri za Wilaya zinatengewa fedha za kutosha. La msingi kama alivyosema Mheshimiwa Mwakipesile, ni sisi Wabunge vile vile kuona kwamba fedha zile zinatumika kwa utaratibu gani na zinatoa matokeo gani katika kuboresha na kupunguza gharama za wakulima wadogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pili, gharama za umeme na maji, hizi ni lazima tuzifanyie kazi. Inabidi tuzifanyie kazi kwa maana iko haja ya kupunguza ada zinazotozwa kwa umeme na maji. Tulifanya utafiti fulani mwaka 1998 kwa Kiwanda cha Urafiki, ilionekana kwamba kwa kupunguza asilimia 20 au 30 ya gharama za umeme kiwanda kile kinaweza kuzalisha maradufu. (*Makofî*)

Sasa haya ni maeneo ambayo Serikali itabidi tuyaangalie, tuone ni jinsi gani nishati hizi zinaweza kusaidia katika kupunguza gharama za umeme. Tuna hakika kwamba kukamilika kwa mradi wa Songo Songo na mradi wa *Mnazi Bay* kutasaidia sana sisi kuijweka sawa kama Serikali kupunguza gharama za uendeshaji katika miradi yetu. Gharama za mawasiliano na uchukuzi tuendelee kuzifanyia kazi na kuzipunguza.

Mheshimiwa Spika, vile vile niseme kwamba kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, Tanzania hatuwezi kukaa kimya na kujifanya mabadiliko ya uchumi yanayoendelea duniani hayatuhusu wala hayatugusi. Tutakuwa tunajirudisha nyuma. Ni lazima tuendelee kuimarisha marekebisho yote tuliyokwishayafanya *Economic Reforms, Legal Reforms, Marketing Reforms, Social Reforms* zote ni lazima kuzifanyia kazi bila ya kuchoka.

Pale ambapo bado viwo vikwazo ni lazima tuviondoe. Sasa hivi tumekubaliana kwamba Sekta binafsi lazima tuipe umuhimu mkubwa katika jitihada za kujenga mazingira mazuri ya uchumi, mimi nafikiri hapa ndipo mahali ambapo kwa maana ya Sekta binafsi na tukizungumzia Sekta binafsi inawahuisha hata wakulima wetu Vijijini wanaofanya kazi mashambani. Kwa sababu watu wengine wanafikiri tukizungumzia Sekta ya binafsi ni wale wawekezaji wageni tu, hapana hata mkulima Kijijini ni mwekezaji.

Sasa tujiulize ni sheria gani ambazo zinakwamisha Sekta binafsi na kuleta hasara badala ya faida katika uchumi wetu? Haya ndiyo yanayofanyika katika bajeti zetu za kupunguza baadhi ya kero zinazowapata wakulima wetu na wananchi wetu kwa ujumla. Lazima tujiulize ni kodi zipi ambazo zinakera Sekta binafsi na hivyo kukwamisha Sekta hiyo kuendeleza shughuli zake za kuzalisha mali?

Tatu, tujiulize ni urasimu upi unaokwaza Sekta binafsi katika kutekeleza shughuli zake? Ni urasimu gani wa kiserikali ambao unaifanya Sekta binafsi hususan wakulima wasindeleze kazi zao? Mwishoe moja ya eneo ambalo linasumbua sana Sekta binafsi ni suala la rushwa. Tunahitaji bado tuendelee kupambana na suala hili la rushwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi sisi wenyewe tu mashahidi. Sisi Tanzania miaka kumi hivi au kumi na tano iliyopita tulikuwa sawasawa na nchi kama Korea ya Kusini, tulikuwa sawasawa na nchi kama Malaysia, Singapore, Indonesia. Lakini sasa hivi hata katika nyanja za mazungumzo tukisema kwamba sisi Watanzania wenzetu ni nchi kama hizo kwa kweli tunajidanganya tu. Wale sasa siyo wenzetu ingawaje nchi hizo zilikuwa kama sisi katika miaka ya 60 – 70 wenzetu wamepiga hatua kubwa sana. Siri moja waliyofanya wenzetu ni msukumo katika uwekezaji *Investment drive*.

Wenzetu wamejithadi sana katika suala la uwekezaji. Sisi tulikwenda Uchina tukazungumza na viongozi wa uchumi wale Wachina tukawauliza, ni nini siri ya maendeleo yenu? Wale Wachina wakatuambia unajua zamani tulikuwa tunasema kwamba lazima tufungue milango kwa wawekezaji wa nje. Sasa tukuhakikishie Mheshimiwa Waziri sisi China tumefungua milango, tumefungua madirisha na inawekezana hata kuta sasa tukazivunja ili kukaribisha wawekezaji kutoka nje. (*Makofî*)

Sasa hili kwa kweli wenzetu limewafikisha mbali sana. Sasa hili linahitaji kwanza *political will*, inataka sisi wanasiasa; Je, kisiasa hilo tunalipa miadi gani *political will*. Lakini la pili linataka tubadilishe fikra zetu na mtazamo wetu. Wenzetu wanasema *change of altitude and right mind set*. Ni lazima kuwe na miadi ya uongozi, mabadiliko ya mtazamo wa wanasiasa, mabadiliko ya Watendaji Serikalini na hamasa ya jumla kwa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, sisi tumekaa chini ya mfumo funga karibu miaka 30, 35, 40. Inawezekana kabisa fikra zetu sisi tunapowaona Wawekezaji tunatanguliza suala la udhibiti, kwa sababu tumezoea kudhibiti. Sasa *altitude* hii tunaomba kwamba tuibadilishe tuone kwamba Wawekezaji kutoka nje na ndani tunawapa umuhimu mkubwa katika kuuendeleza uchumi wetu. Lakini yote haya yatazingatia mahusiano ya faida kwa wote na siyo yale ya kumnyonya mwengine.

Ndiyo maana tunasema tunachohitaji ni *win, win situation, siyo beggar by neighbour*. Tunataka tufanye *partnership* kama walivyozungumzia wenzetu wa Kamisheni ya Afrika, *partnership* ambayo inaleta faida kwa wote. Tunatakiwa tukaribishe mitaji katika maeneo ya usindikaji, barabara, uvuvi, kilimo, teknolojia ya habari na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie eneo la ubinafsishaji ambalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Zoezi la ubinafsishaji hivi sasa linagusa maeneo muhimu. Miundombinu inayotoa huduma moja kwa moja kwa wananchi au Umma *public utilities*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawahakikishia Waheshimiwa Wabunge na inawahakikishia wananchi wa Tanzania kwa ujumla wao kwamba utaratibu wa kubinafsisha Mashirika haya hayatauzwa. Haya Mashirika kwa kweli hayatauzwa, bali yatakodishwa. Uzoefu duniani umetufundisha hata katika nchi zilizoendelea Australia, walibinafsisha reli, wakauza imewashinda. Uingereza wamebinafsisha reli kwa kuuza imeshindwa. Sasa kwa kweli napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba hilo eneo sasa hivi tutalifanya kwa makini sana ili tusije tukaharibu uchumi wetu au tukaangamiza uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge hili la Serikali ya Awamu ya Tatu, kwanza limekuwa ni *innovative Parliament*. Wabunge wamekuwa *innovative*, Wabunge wamekuwa wabunifu na ndiyo maana tumefika hapa tulipo. (*Makofi*)

Hii siyo kazi ya Serikali peke yake. Ni kazi ya Serikali pamoja na Waheshimiwa Wabunge tumeleta Miswada hapa, tunaleta sera hapa, tunazichangia, tunafikia muafaka, tunakwenda kutekeleza. Kwa hiyo, awamu hii Bunge limekuwa bunifu, lakini vile vile awamu hii ipata Serikali bunifu. Kwa sababu yote yaliyotolewa hapa, yamekwenda kutekelezwa na leo tunazungumzia ukuaji wa uchumi wetu.

Tunazungumzia kuimariika kwa huduma za afya, kuimariika kwa huduma za jamii, lakini tunasema kwamba maendeleo siyo tukio kama alivyosema Mheshimiwa Milton Makongoro, maendeleo ni mchakato, ni *process*, maana kama maendeleo yangekuwa ni tukio la sasa hivi tu nadhani tungefika mbali sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina hakika tukiendeleza nidhamu katika kutekeleza mipango yetu katika matumizi yetu ya fedha, katika ukusanyaji wa mapato, katika kufungua na kuibua fursa za ajira na mapato, kufanya kazi kwa bidii, kujituma, kudumisha amani na usalama, kama ilivyo sasa hivi, tutapiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nchi yetu kufutiwa deni lote na *World Bank, IMF* na *ADB* haina maana tena kwamba hatuna deni la kulipa. Hili inabidi tulitafsiri kwa vizuri sana na lile deni ambalo tunesamehewa maana yake ni kwamba hazipo raslimali tayari hivi sasa ambazo zilikuwa zinatakiwa kulipa deni hilo. Raslimali hizo zilikuwa lazima tuzitafute katika kujenga uchumi wetu. Kwa hiyo, pamoja na kupata afueni hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri wa Fedha atalielezea vizuri zaidi.

Lakini tunasema tu uamuzi wa *G8* unatuongezea uwezo wa kumudu deni letu *that sustainability* wa kulipa yale madeni ambayo hayajafutwa nje ya *World Bank, IMF* na *ADB*. Kwa hiyo, bado kazi tunayo kama tulivyosamehewa *HIPIC* fedha zilipatikana tumejenga mashule. Sasa kama tunavyosamehewa na *World Bank, IMF* na *ADB* ina maana fedha zile ambazo tungelipia lazima tuzitafute sasa ndiyo hizo ziende kwenye miundombinu, huduma za afya na jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama walivyochangia Waheshimiwa wengi, tunasema tutatoa kipaumbele kwenye kilimo, tutaendeleza jitihada ya kuuza nje pamoja na usindikaji na tutaendeleza miundombinu hasa barabara Vijijini. Mikakati tuliyojiwekea kama

MKUKUTA, kama MKURABITA vinahitaji nidhamu kubwa sana katika utekelezaji wake na kwa sababu MKUKUTA ni mkakati unaogusa sasa hivi sekta zote, umezingatia vile vile urekebishaji wa *investment disparities* zinazotokea hapa nchini kwetu.

Kama kawaida ya Serikali ya CCM nina uhakika kuwa afueni ya madeni tulioipata na utaratibu huu ambao tunaufuatalia sasa hivi utatufikisha mahali pazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu imefaidika na michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge. Hoja zote zilizotolewa hapa tumezijibu. Makabrasha tumeshayasambaza kama tunavyofanya siku zote. Nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa mwongozo wako mzuri hapa Bungeni, umetuongoza vyema na kwa busara sana. (*Makofi*)

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, tumeshirikiana vizuri katika kipindi hiki cha miaka mitano ambayo Bunge hili linafikia mwisho hasa nilipopewa dhamana na Chama changu na Serikali yangu kwenye eneo la Mipango ya nchi na Ubinafsishaji, Mmenisaidia sana, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Ahsante yangu ni kuwaombeeni kila la kheri na fanaka mrudi tena hapa Bungeni. Ndiyo ahsante yangu. Nami mniombee kwani nitagombea tena Jimbo la Handeni. (*Makofi/Kicheko*)

Mwisho, nawashukuru sana Wanahandeni kwa fursa waliyonipa ya kuwatumikia. Nami naahidi kuendelea kuwatumikia kwa tija na ufanisi kwa nafasi waliyonikabidhi tokea mwaka 1995. Nitajitahidi sana. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mwisho kabisa, Waheshimiwa Wabunge, mmechangia vizuri sana bajeti hii, mmetoa mawazo ya msingi na kama kawaida mawazo yote yanayotoka kwa Waheshimiwa Wabunge Serikali inayapokea, inayathamini na ndiyo maana tumefikia hapa. Mimi nawaombeni tena tupitishe bajeti hii ili twende tukaendeleze mbele utekelezaji wa Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi kwa maslahi ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Aidha, tupitishe Bajeti hii tukatekeleze tena MKUKUTA, MKURABITA na mipango mingine tuliojiwekea. Mimi nina hakika Bunge lingine lijalo wale watakaokuwepo katika Bunge hilo wataona maendeleo makubwa. Sasa tumefikia katika eneo la uchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokwishaeza, hiyo ndiyo inatufikisha mwisho wa kipindi hiki cha asubuhi. Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 05.41 Asubuhi Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Kikao kilichoanza asubuhi kinaendelea. Sasa namwita mtoa hoja ya Bajeti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ahitimishe hoja yake.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi tena ya kufafanua baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ambao ni 28 na kwa maandishi ambao ni 25.

Wabunge hao ni Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mheshimiwa Abdulla Lutavi, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Faustine Rwiomba, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa William Kusila na Mheshimiwa Athuman Janguo. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Profesa Talala Mbise, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Rished Abdallah, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi walikuwa Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu tena,

Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi na Mheshimiwa Ireneus Ngwatura.

Waheshimiwa wengine ni Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Mwaka Abraham Ramadhani, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo na Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir. (*Makofî*)

Nawashukuru sana Waheshimiwa hawa wote niliowataja, nasikitika kama nimesahau mtu anisamehe sana. Niseme kwamba kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, asubuhi, hawa ni wengi na siwezi kumjibu mmoja, mmoja. Lakini natumaini kwamba mchanganyiko wa hoja za Manaibu Waziri wangu leo asubuhi na hizi nitakazotoa hapa kwa ujumla wake zitasaidia kutoa mwanga kwa waliokuwa wengi.

Mheshimiwa Spika, niseme kwanza kwamba kuna watu ambao wana wasiwasi, wana madukuduku. Kadri nilivyoelewa walikuwa watatu Mheshimiwa Leonard Derefa, alikuwa na dukuduku juu ya masuala ya umwagiliaji, Mheshimiwa Philip Marmo, juu ya tatizo la Wahzabe na Mheshimiwa Omar Kwaangw', juu ya tatizo la barabara ndani ya Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Wizara ya Fedha siyo Wizara tendaji kwa maana kwamba mambo mengi yaliyozungumzwa hapa ni jukumu la Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha kazi yake kubwa ni kutafuta mitaji, kutafuta fedha za kuendeshea Serikali na kulipa madeni na kugharamia Serikali kwa ujumla ndio kazi yetu kubwa na kusimamia uchumi katika maeneo yale yanayohusu fedha, mabenki na kadhalika.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa hao wayafikishe madukuduku yao kwa undani zaidi kwa Wizara husika lakini kijuu juu kwa sababu Wizara nayo inauelewa wa mambo mengi kijuu juu kwa sababu hatutoi fedha bila kujua ni kwa ajili gani na kwa sababu hiyo mambo fulani huwa tunayafahamu ili tuone kama yanastahili kupewa fedha ama hapana. Kwa sababu hiyo niseme kijuu juu kwa matumaini kwamba Waheshimiwa wahusika wataonana na Mawaziri husika, kuzungumza kwa undani zaidi na mimi naweza nikaahidi ushirikiano wangu kama kawaida. Kwa sababu Wizara ya Fedha kazi yake ni kushirikiana. (*Makofî*)

Hili la umwagiliaji nitalieleza baadaye, kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Leonard Derefa, naomba asubiri nitakapomwaga *material* hapa juu ya umwagiliaji labda yanaweza yakamsaidia. Kwa ndugu yangu Mheshimiwa Philip Marmo, ni kweli wengi tunafahamu kuna Watanzania yeye mwenyewe ametuambia ni kaya 500 wanaoitwa Wahadzabe katika eneo lake katika Jimbo lake nadhani la uchaguzi na tunajua kwamba wako nyuma kimaendeleo.

Mimi ningemwomba Mheshimiwa Philip Marmo, akishirikiana na Halmashauri yake wajenge hoja ndani ya Halmashauri, ndani ya Mkoa ili kama tatizo ni kubwa kiasi kile Taifa liweze kuona kwa mapendekezo kutoka Mkoani ni kitu gani kifanywe kuwawezesha wananchi hawa kufanana na wananchi wengine.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema tu ni kwamba nilibahatika kutembelea China na kule nilikuta wana mpango wa kusaidia watu waliokuwa wakiishi kwenye mahandaki na ambao sasa wanaishi kama sisi. Kwa hiyo, inawezekana China wamefanya na Tanzania inaweza ikafanya lakini lazima hoja ijengwe. Hili la barabara naelewa pia kwamba Mheshimiwa Rais alipounda Mkoa wa Manyara alitamka kwamba Wilaya za Mkoa ule zingeunganishwa kwa barabara za kuaminika ili Mkoa ule uwe ni kitu kimoja. Kwa sababu Wilaya zile zimenyofolewa kutoka uliokuwa Mkoa wa Arusha. Hilo la kwanza, kwa hiyo, kuna barabara za kuunganisha Wilaya za Manyara, hasa Kiteto na Simanjiro na Wilaya nyingine na ninaelewa kwamba kuna mpango ambao Mkoa umeandaa.

Kwa hiyo, ninachoweza kusema tu ni kwamba kwa barabara hizo za ndani sisi Hazina tumezipokea na kwa kiasi tumeweza kutoa fedha za kugharamia sehemu ya barabara hizo. Tatizo hapa ninavyolielewa ni kwamba fedha zilizotolewa hazitoshelezi, labda mimi nafikiri kwamba hiyo ni ngazi ya Mkoa, lakini ukienda kwenye zile Wilaya ambazo zimeanzishwa wakati huo huo, Mvomero kwa mfano, Kilolo, juzi liliulizwa swali hapa la barabara za Kilolo, nadhani Mheshimiwa Venance Mwamoto, aliuliza swali hapa na akajibiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi. Nafikiri inawezekana ikajengwa hoja ya kusema kwamba Mkoa na Wilaya hizi mpya zihudumiwe kwa utaratiabu maalum Kibajeti. (*Makofi*)

Kama hoja hiyo ingejengwa na Wizara husika ya TAMISEMI, nafikiri sisi Hazina tuko tayari kusikiliza na kutoa ushirikiano wetu, ni lazima ijengwe hoja. Swali langu ni kwamba Waheshimiwa Wabunge watashirikiana na wenzao huko kwenye Wilaya hizo na Mkoa kufanya mambo hayo. Nafahamu kwa mfano Wilaya ya Mvomero, liko daraja pale ambalo limezuia kabisa maendeleo ya kilimo na ufugaji katika Wilaya ile na gharama yake ni kubwa siyo gharama unayoweza kuibajeti Kimkoa au Kiwilaya. Kwa hiyo, mambo kama hayo yaje mahali ili tuyaaangalie na tuone jinsi ya kuibua Wilaya hizo na shughuli za kiuchumi za Wilaya zenyewe.

Lakini kwa Mheshimiwa Omar Kwaangw', nitaeleza baadaye nitakapozungumzia juu ya barabara hizo. Kuna kazi ambayo sisi kama Hazina tumekuwa tukiifanya na tumeendelea kuifanya na nitaeleza baadaye, kwa hiyo nionavyo mimi tatizo labda liko ndani ya Mkoa siyo kuzunguka Mkoa, siyo kuunganisha Mkoa na Mkoa mwagine. Mkoa wa Manyara umeunganishwa vizuri na Arusha utaunganishwa vizuri na Dodoma, utaunganishwa vizuri na Iringa, utaunganishwa vizuri na Singida, kwa hiyo, hii nitaeleza baadaye. Nimetanguliza haya kwa sababu niliwasikiliza vizuri, niko tayari kuendelea kusikiliza au Waziri wa Fedha yuko tayari kuendelea kusikiliza kwa sababu *Hansard* itakuwepo.

La pili linahusu pensheni za Afrika Mashariki, waliokuwa watumishi wa Afrika ya Mashariki. Niseme kwamba Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ilipovunjika aliteuliwa msuluishi Victor Umbritch, Mswisi ambaye sasa ni marehemu. Ambaye alitoa mapendekezo, nayo yakakubalika na Serikali hizi zote tatu za Afrika ya Mashariki, namna ya kugawana mali zilizokuwa za Afrika ya Mashariki na namna ya kugharamia mambo mengine yaliyotokana na Jumuiya hiyo. Kwa upande wa watumishi wa Tanzania iliambiwa kiasi ambacho watumishi wangelipwa wakati ule na Uganda ilipewa na Kenya walipewa, wakapewa na tarehe ya kulipa yaani hii taarifa ni ya mwaka 1989. Tanzania tulipewa fedha kutoka *Crown Agents* yaani kwa ajili ya kulipa hawa kutoka Uingereza *Pound Sterling* milioni 9,189,410.54. Mwaka 1987, fedha hizi ziliingia Tanzania zikawekwa kwenye *account* ndani ya Benki Kuu (*BOT*).

Waziri wa Fedha wa wakati ule akaagiza Benki Kuu kwamba fedha zitafsiriwe kwa shilingi na ziwekwe kwa shilingi, kwa sababu malipo ya mishahara yanafanywa na marupurupu na pensheni Tanzania inafanya kwa shilingi siyo kwa *Pound Sterling*, sarafu yetu sisi ni shilingi, ikafanyika. Baadhi wakalipwa, baadhi hawakulipwa kwa sababu mbili, moja wengine walajiriwa upya na Mashirika yaliyoundwa kutokana na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mfano Shirika la Posta, Shirika la Ndege, Shirika la Bandari. Mashirika yale yaliyoundwa upya na wengi wa watumishi wale walichukuliwa na Mashirika hayo na wakapewa masharti mapya ya kazi ikiwemo sharti la kulipwa sehemu yao ya hayo malipo yaliyotoka *Crown Agents* siku watakapostaafu. Lakini Umbritch akasema kama Serikali itachelewa kulipa iko asilimia fulani ambayo itabidi ilipe kama *interest* kwa fedha hizo zilizotoka *Crown Agents* wakati wa kulipwa ukicheleweshwa 7% *interest* iliwekwa na ikakubalika kwa kuchelewesha kulipa wafanyakazi hawa.

Hao amba wameshalipwa ni zaidi ya shilingi 17 bilioni, lakini kuna wengine amba wanlipwa hata sasa hivi Mashirika yaliyo kwa mfano chini ya lililokuwa Shirika la Posta na Simu, leo ni *Simu 2000*, ni *TTCL* ni *CELTEL*, ni Shirika la Posta, hayo watu wanaendelea kulipwa hata sasa hivi tunavyozungumza. Kuna wengine waliokuja kujitokeza mmoja mmoja wakasema mimi siwezi kusubiri nilipeni niende zangu, wamelipwa na rekodi zipo. Wengine wakasema hapana sisi tunataka kwenda Mahakamani tudai kwa sababu Serikali inaonekana inatudhulumu. Wakaenda Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, siku walipokwenda Mahakamani kwa mujibu wa sheria kesi likishaenda Mahakamani Utawala lazima usimame. Hii kila Mwanasheria anajua kwamba kesi iliyoko Mahakamani hulifanyii tena jambo lolote lile mpaka liamliwe. Kesi ile imekaa Mahakamani zaidi ya miaka 10, Serikali ya Tanzania yenye Serikali hii ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa tukikaa hapa Dodoma tarehe kama hizi mwaka 2004, maana wakati ule tukizungumza kulipa mkupuo, hata watu amba hawakuwa na haki ya kutudai, tumeenda kuwatafuta na kuwalipa upya. Tunalipa walimu, tunalipa wadai wengi wa ndani, tukasema liko tatizo la watu hawa amba kwa kusubiri kesi wataendelea kusota.

Kwa hiyo, tuwaite wale, tuwaambie tuzungumze, tuwalipe. Ni sisi, wao hawakuwa wanazungumza tena habari ya kulipwa, hii unasikia hawa walipwe ni sisi

Serikali tuliibua tena jambo hilo ndio sasa kila mtu anasema walipwe, kama hatukuliibua hakuna mtu angezungumza kulipwa, walikuwa Mahakamani. Kwa hiyo, tunastahili makofi kwanza kwa kuibua hili jambo. (*Makofi*)

Kwa kusema hii ni Serikali ya kistaarabu na watu wake ni watu wazuri tu, wastaarabu na wengine wanazidi kuzeeka basi tutafute namna tuwalipe wakaja. Mimi binafsi nikawaambia ondoeni kesi Mahakamani ndio utaratiabu wa kisheria ili tuzungumze uraiani. Tukifika mahali tusipolewana mtarudi Mahakamani, lakini angalau tutakuwa tumezungumza. Hawa walikuwa wanadai shilingi bilioni 500, Mahakamani waliende kudai Serikali iwalipe shilingi bilioni 510 ndio kesi iliyoko Mahakamani na mpaka leo kimekuwa *suspended* kwa maana hiyo wakaondoa, tukaunda Kamati mbili, ya kwao na ya Serikali. Wamezungumza muda mrefu, wakafika mahali wakakubaliana Kamati ya Serikali na Kamati ya Watumishi hao waliokwenda Mahakamani wakakubaliana.

Mheshimiwa Spika, yalikuweko masuala zaidi ya 10 waliojadili, masuala 12 ambayo wamekubaliana na mengine manne ambayo hawakukubaliana. Kati ya masuala yote 12 walikubaliana na kwa bahati nzuri kati ya hayo ni pensheni yenye, ni akiba ya wafanyakazi, *severance allowance*, kiinua mgongo, malipo ya malimbikizo, riba, ni mambo 12. Walikubaliana yakabaki manne tu, na hayo manne ni yapi ambayo hatukukubaliana yaani ile Kamati ya Serikali hawakukubaliana na Kamati ya Wadai.

Moja ni gharama za kesi wanataka Serikali iwalipe gharama za kesi mpaka hapo walipoenda kuondoa, wanataka Serikali iwalipe usumbufu kitu wanaita *damages*, wanataka Serikali iwalipe pensheni ya nyongeza yaani pensheni kutokana na ofisi zao kufutwa, kitu wanachoita *Abolition of Office*, kwamba nilipe kwa sababu mimi nilikuwa kazini wewe ukavunja lile Shirika. Lakini Serikali ya Tanzania haikuvunja Shirika la Afrika ya Mashariki ni nchi tatu zilivunja. Hawa wanasema nyie mlivunja lile Shirika lililokuwa linatujiri tulipeni fidia kwa kuvunja Shirika. Kisheria kuna jambo linaloitwa *Abolition of Office*, lakini sio kwenye hili. Hii kwa kweli ungeweza ukasema ni dharura, kwenye Sheria wanaita ni *force majeur* wao wanasema *Abolition Office*. Mimi hapa ni *bush lawyer* sikusomea Sheria nakwambieni linaitwa *force majeur*. (*Kicheko*)

Hiyo wala sikuhitaji Mheshimiwa Andrew Chenge anieleze hilo, *force major* ni sawa sawa na tukio la kivita, ni sawasawa na mafuriko, ni sawasawa na tetemeko la ardhi *force major*. (*Kicheko/Makofi*)

Halafu baada ya yote haya sasa wanataka walipwe kiinua mgongo yaani *gratuity asilimia* 70 ya mishahara yao ya mwezi kwa kipindi chote. Uwalipe kiinua mgongo asilimia 70 ya mishahara yao ya mwezi kwa kipindi chote, toka mwaka huo wa 1987. Sasa Waheshimiwa Wabunge nyie hapa kila siku mnanigombeza tunza hela ya Serikali. Angalia, mimi nilivaa miwani nikaangalia vizuri sana nikaona hii haifai. (*Kicheko/Makofi*)

Lakini nikasema kwa sababu zile zile mlizokuwa mnasema hapa Waheshimiwa Wabunge nikasema lakini watu wamesubiri muda mrefu tukubaliane nao kwa sababu *issue* kubwa hapa ni pensheni. Walikuwa wanadai hasa kiinua mgongo na mengine haya

ambayo ni mazuri tu 12 tumekubaliana ni manne yenyе maneno, sisi haya yenyе maneno tuyaweke kando yanaweza yakarudi hata Mahakamani tena. Kwa sababu hayana madhara makubwa, lakini mtu ataanza kupokea hela leo atakula na huku akisubiri, kwa hiyo, nikasema niko tayari kuwalipa, wakasema hapana.

Siku moja nimetoka Rukwa niko Ofisini hivi naangalia angalia mambo ya wiki iliyopita nikaona watu wamekuja wengi kabisa, wengi wanaelekea Ikulu, nikauliza watawala wangu kuna nini pale nje? Hata mzee sisi hatufahamu. Basi kumbe ni rundo kubwa la watu limekuja pale nikaona *FFU* wameingia pale, mimi nilishtuka sana maana Ofisi yangu haina dirisha la kurukia ili nitoke nje. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, nikaona watu wananyakuliwa pale wanapelekwa polisi, sikuelewa ni kitu gani kabisa. Lakini nikaona waandishi wa habari nikawaita, nikawauliza kuna nini? Wakanambia unadaiwa hela hapa bwana Waziri wa Fedha, nikawaeleza waandishi wa habari historia yangu mimi nilivyoijua. Baadaye nikajifunza kwamba Polisi wenyewe waliona kuna watu wakadhani watu hao walikuwa wanakwenda Ikulu. Ndio wakawashughulikia, mimi sikuita Polisi, wanasema Basil Mramba aliita Polisi, mimi wala sikuwa na habari yoyote kabisa.

Kwa hiyo, mara baada ya hapo zikaanza kuja barua za kusema lile kundi tulilokuwa tunazungumza nao limesambaratika, kumetokea mapinduzi ya ndani kwa ndani, wale watu hawaelawani tena na barua ya kusema usizungumze na wao tena ni wahuni sisi tumeachana nao. Kwa hiyo, bwana Waziri endelea na wewe tuge chochote unachoweza kutupa muda si muda ikaja barua nydingine inasema hapana lile kundi limerudiana, muda si muda ikaja barua nydingine ikasema hapana wamechagua viongozi wapya muda si muda lile kundi likasambaratika.

Lakini Mungu amebariki yule Mwanasheria wao bado yupo, ni *advocate*, kwa hiyo, mimi nikasema tuzungumze na huyu *advocate* kwa sababu ni mwakilishi wao halali kabisa ndio alikuwa Mahakamani, tuzungumze na *advocate* kwa hayo yaliyobaki. Lakini kwa sababu limeshatoka hadharani haya mambo yalikuwa bado yako kiofisi tu kwa sababu yalishatoka hadharani ikabidi sasa Rais afafanue kule Songea wakati wa *May Day*.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri walio hapa watathibitisha, juzi tarehe 8 Juni, 2005 Rais mwenyewe wakati tukijadili hii Bajeti alifafanua kwa Mawaziri alisema nini Songea? Na ninanukuu alisema; “Kuna madai ya shilingi 400 milioni hayo 400 sasa ni ile 500 ilikuja kuteremka ikafika 400 kwa yale tuliyokubaliana. Zile bilioni 500 za awali zilizokuwa Mahakamani zilikuja kukokotolewa zikafika 400 bilioni kwa yale mambo 12 ambayo tulikubaliana. Hawezi akasema hivi Mawaziri kwa sababu vyombo vyaya habari vimesema nilivyojema na vingine havikusema nataka nyie Mawaziri mfahamu, sikusema kwamba nalipa shilingi 400 bilioni, kule Songea sikusema hivyo *point number one*.

Point number two, nimesema nitalipa chochote ninachoweza kulipa kabla sijaondoka madarakani na. Ni 50 bilioni ndio tunayoweza kwenye Bajeti hii na ndio hiyo unayoiona kwenye Bajeti 50 bilioni.

Mheshimiwa Spika, ya tatu, tutaendelea kuzungumza na hawa wafanyakazi mpaka hapo tutakapofika mahali tuelewane kabisa au tusielewane kabisa ndio itaamuliwa tena mambo yatakuwa namna gani. Kwa hiyo, kwenye Bajeti hii nimeweka shilingi 50 bilioni na sikuweka kwa kukisia, iko mantiki ukichukua *formula* ya Umbritch, ukachukua na misingi ya Kibenki mimi nilikupa fedha mwaka 1987 leo ni shilingi ngapi? Kama nilikupa shilingi 100 mwaka 1987 leo ni shilingi ngapi? Halafu tukasema kama wewe Serikali ingekuwa ni hela yako na umeshaipeleka huko ukakopesha watu wakaifanyia biashara leo ingekuletea shilingi ngapi yaani faida yake? Tukatumia elimu ya Kibenki na Kihazina tukafika mahali panapokaribia karibia 50 kwa sababu kama nilivyosema wanaodai sio wote wale, jumla ya wafanyakazi waliotoka kwenye hili Jumuiya walikuwa 28,831.

Mheshimiwa Spika, wanaodai sio 28,000 wala 20,000 wala 10,000 ni wale waliopo, lakini wapo kwenye Mashirika ambako hivi leo wanalipwa pensheni na wataendelea kulipwa pensheni na watalipwa mafao yao yote ndani ya Mashirika hayo wanayofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hao waliobaki ambao wameelea unaweza ukasema wameelea ndio hao wa 50 bilioni, maana yake watu wanazungumza kana kwamba kuna Serikali hapa imekaa tu inacheke cheka na huku watu wanakufa.

Mheshimiwa Spika, tutalipa, tutalipa na endapo katika utafiti kutajitokeza waliokufa basi warithi wao watalipwa. Hii Serikali inawezaje ikamrusha mwananchi wake? Serikali imrushe mwananchi? Si ingemrusha Mwingereza aliyetoka hapa sasa hivi. Maana yule hana kura wala hana lolote, yule sana sana anaweza akatuletea mabomu hapa akatubomu, thubutu ataanza wapi? Hakuna. Lakini sisi ni wastaarabu, tunalipa madeni ya nje na tunalipa madeni ya ndani na kwenye kila bajeti tunatenga na tunalipa mpaka fidia mpaka *interest*, siyo kwamba mtu anakuwa na kielfu chake kimoja ndiyo leo kinatembea tembea tunakuja kulipa kielfu, hapana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukokotoaji uliofanywa utakuta kuna watu watakula mamilioni hapa. Kuna watu watakula mamilioni, kuna mwingine atapata milioni 90, mwingine milioni 40, mamilioni yatavuliwa hapa mengi tu, kwa hiyo, kila wanapozungumza wanajicheleweshea wao mamilioni. (*Kicheko*)

Sisi tuko tayari kulipa lakini waache kufanya jambo hili kama ni la mzaha. Kuna watu hapa wana mamilioni mengi sana, mimi niliona nikasema loh! Namna hii hata kazi hii ningeacha, nizichukue fedha hizi. Kwa hiyo, zipo Mheshimiwa.

Kwa kifupi ningetaka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali ina nia ya kweli ya kulipa madeni haya, tumekwisha yakokotoa, tunayajua kabisa hata kwa majina na kiasi.

Mimi nitakupeni mfano lakini hamtajua ni nani. Kuna mtu hapa anaitwa Nguma, huyu atalipwa shilingi 91,000,000/=, kuna mtu hapa anaitwa Mkajude au Mkajunde sina uhakika huyu atalipwa 16,000,000=/. Kwa hayo kumi na mawili tumekubalina licha ya hayo mengine, kuna atakayelipwa 45 milioni, 41, 6,11,41,36,29,27,53. Wako na hela ipo, na majina pia yapo na hesabu pia ipo, kwa hiyo, naomba tumalize maneno haya nikafanya kazi tuwalipe hawa jamaa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, na kwa kweli naomba tulimalizie hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa raslimali kimkoa tulishaeleza, nilieleza kwenye hotuba yangu na nimeeleza tena. Kwa kweli tumeanza kutumia ile *formula* na ile *formula* imeonyesha tofauti. Nafikiri ni Mheshimiwa Athuman Janguo alieleza vizuri sana alipokuwa anachangia kwamba kweli kuna tofauti, sekta hizi za elimu, afya, kilimo, barabara, maji vijiji tumeanza kugawa fedha kwa kutumia *formula* ambayo inasaidia siyo kama ilivyokuwa huko nyuma na hili ni lenu. Hili siyo langu ni lenu ninyi, mlinipa kazi nikaifanya nikaweka *formula*, ipeni nafasi *formula* hii ifanye kazi kwa sababu hatuwezi kuwa na *formula* mwaka huu na mwaka ujao tunabadilisha, tunaweka mwaka kesho kutwa mwaka mtondo goo tunabadilisha itakuwa nchi inayumba yumba, haina wasomi. Sisi hapa tunesoma, tumeona *formula* inafanya kazi. (*Kicheko/Makofi*)

Lakini kwa kutambua pia hoja zinazojitokeza hapa toka miaka miwili iliyopita kuna Mbunge mmoja alisema ni kweli nilifanya kikao na Wabunge, baadhi ya Wabunge wa Mikoa ya Singida, Shinyanga, Kigoma na Rukwa hawa wa Ukanda wa Magharibi wanajiita wa Ukanda wa Magharibi, nikazungumza nao. Mnasema mikoa yenu iko nyuma sasa tufanyaje? Tulikubaliana na baadaye nikaithibitisha kwa maandishi kwa Wabunge waliowakilisha Mikoa hiyo kwamba kwenye mikoa hii ukiweza kushughulikia barabara na maji yaani kwa ujumla miundombinu na maji utakuwa umefanya jambo kubwa kabisa.

Mimi nikawaambia nitafanya zaidi, nitafanya zaidi lakini tuanze hapo, nikarudi lakini Mtwara, Lindi, nikarudi eneo hili la Ruvuma, hii *Mtwara Corridor* nikarudi, Ruvuma hii nikarudi, mambo ni yale yale. Sasa tukakubaliana na nikawathibitishia kwa maandishi Wabunge wale wako hapa kwamba sasa tukubaliane kwamba tufanye kazi hii, mimi nitaingia kazini na ninyi ingieni kazini huko kwenu.

Matokeo ni nini. Sasa naanza na lile la barabara. Matokeo ni nini, barabara za *Mtwara Corridor* mimi mwenyewe hapa niliondoka hapa mwezi Februari wakati Bunge linakutana hapa mimi niliondoka na wengi hawakujua nimekwenda wapi. Nilikwenda kutafuta hela zenu za barabara hizo, nimefika Khartoum na Tunis na Rome kufuatilia hela za mikoa hii. Nikapata nini? Khartoum, *BADEA* wameahidi kugharimia kilometra 200 za barabara inayotoka Mtwara kuelekea *Mbamba Bay* kilometra 200. (*Kicheko/Makofi*)

Ya pili, watanitafutia matajiri wengine *Kuwait Fund* na *funds* nyingine waungane nao mkono ili barabara hii ipate wafadhili kama watatu, wanne, watano, ili waimalizie Mtwara - *Mbamba Bay*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pale pale nilifikia maelewano juu ya uwanja wa ndege wa Songwe - Mjini Mbeya, palepale, kule Khartoum . Nilipokwenda *African Development Bank (ADB)*, kule Tunisia *African Development Bank*, nilikwenda kuhimiza na kusaini fedha za ziada hazikuwa kwenye bajeti wala haziko kwenye bajeti za ziada zitakazosimamiwa na Wizara ya Kilimo kwa ajili ya mikoa ya Kanda. Kagera, Mara, Mwanza, Shinyanga, Kigoma, mikoa hiyo itapata fedha kutoka *African Development Bank*, za ziada kwa ajili ya maendeleo yao ya vijijini yaani *TASAF* mara tano. Ni fedha nyingi sikuenda kutafuta hela ndogo, nilikwenda kutafuta fedha nyingi. (*Makofi/ Kicheko*)

Hizi za *Lake Zone* shilingi bilioni 80, bilioni 80. Kwa hiyo, huku ukiona fedha za *TASAF* sahau kwanza hizo na zile nyingine huko za Halmashauri sahau na zinazokuja kule kuititia Wizara mbalimbali sahau. Ongeza na zinazokuja kwa barabara za vijijini kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu sahau, ongeza nyingine 80 bilioni kwa wote hao wanaozunguka Ziwa Victoria. Shida yangu sasa siyo hiyo, shida yangu ni ile aliyo sema Mbunge wa Kyela, kwamba zikisha kwenda huko zitakuwa salama? Zikishaenda huko fedha nyingi namna hii haijawahi kutokea hii ni sawa sawa na nzige na siyo senene, ni nzige, nyingi kama nzige. (*Kicheko*)

Halafu kana kwamba hilo halitoshi kwa Mtwara na Lindi nikarudi. Nikaenda *OPEC*, maana hawa walikuwa wanalamikia mambo yao vivyo hivyo yanafanana na haya tulikuwa nyuma ooh! Sisi tulikuwa *front line*, sasa mnatufanyaje? Mtwara nikatafuta *OPEC* shilingi nyingine bilioni 11 kwa ajili ya Mtwara na Lindi. Sahau *TASAF*, na hizo nyingine, hii ni *over and above, billion 11* kutoka *OPEC*. Shida yangu ni hiyo hiyo *capacity*, kule zitakuwa salama?

Sasa niambieni huo Mkoa ulioongezewa kiasi hicho, *over and above* hii hela iliyoko kwenye bajeti hii ni mkoa upi? Lakini mimi nimefurahi kwa sababu nimejibu hoja za Wabunge, nimejibu hoja zenu Wabunge na wa mikoa hii mngepiga makofi hapa jumba lingeunguruma nimewasaidia sana. Maana fedha hizi zitakwenda kwenye afya, kilimo, elimu, barabara za vijijini mambo yaleyale ya *TASAF*. (*Makofi*)

Halafu nikarudi hapa kuunganisha sasa mkoa wa Arusha na Dodoma na Iringa. Mwaka jana mimi mwenyewe nilikwenda na Maafisa wangu, Washington tukasaini pesa pale Washington, tukasaini *Word Bank* yaani Benki ya Dunia, *Nordic Fund*, tumesaini fedha pale za kushughulikia barababara ya Makuyuni - Dodoma, halafu tukaja kusaini fedha nyingine ya *Central Corridor*, Dodoma - Iringa. Barabara hizo zinafanyiwa utafiti, *design, feasibility study* ije ikawe ya lami kutoka Makuyuni - Dodoma kuititia Kondoa mpaka Iringa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *NORDC Fund*, Benki ya Dunia, *ADB*, nikarudi huko kutafuta fedha sasa za kuunganisha Tunduma, Sumbawanga, Kigoma kuelekea Mkoa wa Kagera.

Tumeanza mwaka huu wa fedha barabara ya Tunduma, Sumbawanga inafanyiwa maandiko ya mwisho tayari kutengenezwa kwa kiwango cha lami mwaka huu hela imetengwa. (*Makofi*)

Hata mkiniambia niwasomeeni hii fedha naifahamu. Haina haja ni nyingi *Euro* bilioni ngapi, *Euro*, *Euro* na dola ni nyingi na kwa mara ya kwanza toka Samora Machel na Mwalimu Julius Nyerere, mwaka huu linajengwa lile Daraja la Umoja kuunganisha Mtwara na Mozambique tena linajengwa mwaka huu wa fedha hiyo tayari iko kwenye bajeti litajengwa mwaka huu wa fedha na Tanzania sisi ndiyo tunaongoza ujenzi huo. Mozambique tumewaambia tulieni sisi tutajenga ninyi mkapige makofi kazi ikiisha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa kuna maneno nimesikia hapa ya kuunganisha Mkoa wa Ruvuma na Msumbiji. Jenga hoja. Jenga hoja ya kitaalam haya mambo ni ya utalaam, *economic feasibility* ndiyo jenga hoja, nadhani mlimsikia yule Mwingereza hapa akisema na yule Camdessus wiki ilyopita dunia hii hela mingi, hela mingi lakini uwe safi, uvae vizuri, uwe safi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuwa safi maana yake uachane na ufisadi, uwe na Serikali bora, ushughulikie mambo ya *macro economic parameters* ziwe safi, ujulikane wewe una misimamo unaoelekea wapi siyo mtu unakwenda kwenye mizunguko kama ng'ombe aliye kwenye boma. Huwezi kupata fedha hizi, hii ndiyo ile nilisema kwamba tunakopesheka na tunahesabu ni akina nani watukopeshe na nini na kwa sababu gani na wapi.

Mheshimiwa Spika, haya mambo ndiyo niliyoyaeleza kwenye ile hotuba, ni haya sasa mnayaona *practically*. Maana maneno siyo kitu, hoja ulizeni Wabunge wa maeneo hayo wanajua ninachozungumza .

Kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Omar Kwaangw' zile kubwa kubwa mimi tayari nimeshazitafutia fedha, zile ndogo jenga hoja upya sasa tukae labda tafuta namna tukae tuzungumze za kule ndani tufanye nini. Maana unakuwa na mkoa ambao wilaya moja inatazama kule na nyingine inatazama kule na Mkuu wa Mkoa yupo katikati haifai. Si ndiyo hiyo?

Kwa hiyo, hili la umeme. Hili la umeme maana yake ni miundombinu pamoja na umeme. Limejibiwa swalii hapa juzi na Naibu Waziri wa Nishati na Madini juu ya umeme kuanzia Makambako kuelekea Songea, Mbanga kuelekea Ludewa. Yote ile ya Ludewa tena ni ziada ile mimi nimeitafutia hela za ziada 450 milioni. Uongo Mheshimiwa? Angalia Mheshimiwa anavyofurahi sasa hivi mambo yake poa kabisa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, maneno hayo ya umeme kwa mkoa wa Iringa kuelekea Ruvuma ni utendaji tu umebakii, lakini yalitokana na maneno hapa. Ninyi hapa mlinifumbua macho nikahangaika na sasa pale Mtwara kuna ile gesi ambayo itatoka tu wakati wowote kuanzia sasa hii itashughulikia Mtwara kuelekea Lindi.

Lakini kwa taarifa yenu Mheshimiwa Edger Maokola-Majogo, ni shahidi mimi ndiyo siku moja nikiwa hapa wale wazungu walikuja wakasema Bwana mkubwa wewe ndiye Bwana Fedha, tuendelee ama tusiendelee? Nikaketi nao hapo na akina Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi na Mheshimiwa Philip Magani tukawasuka wale watu wa Canada, wengine walikuwa hawaelewii tunazungumza nini, lakini mimi nikawaambia mimi nawahakikishieni niko nanyi saa 24. Gesi inatoka pale *Mnazi Bay* wakati wowote kuanzia sasa. Kuna gesi imechomwa pale wiki mbili haiishi, wamewasha gesi pale wiki mbili inawaka tu haiishi ni nyingi, ni nyingi sana. (*Makofî*)

Sasa hivi mpango uliopo Sweden hao hao waliokubali ku-*finance* huo mradi unaokwenda wa umeme kuelekea Kusini *proper*, hao hao sasa wanashughulikia kuunganisha mikoa ya Tabora na Kigoma. Tumeshawapata Sweden ili kusudi Kigoma itokane na hali sasa hivi ambayo kwa kweli hairidhishi kiumeme na papo hapo tunataka kuunganisha Tabora na Kigoma kwa barabara, hii ni kazi tunashughulikia sasa hivi. (*Makofî*)

Nazungumza habari za Wizara ya Fedha na siyo Basil Mramba. Wizara ya Fedha. Halafu juzi juzi hivi tumesaini mkataba, namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa kuunganisha Rwanda na Tanzania kwa reli kutoka Isaka kwenda huko Rwanda. Tayari hiyo tumeshasaini na hela inatoka *feasibility study* tayari inafanywa tayari, halafu kwenye yale makubaliano yetu na Rwanda kuna mpango mwagine wa kuunganisha kwa umeme mikoa hiyo ya Magharibi mpaka Kigoma mpaka Tabora kwa kutumia maporomoko ya Rusumo na vile vile kuna uwezekano wa kuunganisha hii barabara ya Dodoma - Isaka mpaka Rusumo kwa lami. Kwa hiyo, umeme, barabara, reli, itaenda tena eneo hilo la wakulima wanaozunguka Ziwa.

Nimemsikiliza kwa makini sana yule Mheshimiwa Mbunge wa Pangani akizungumza juu ya barabara ya kutoka Dar es Salaam kupitia Bagamoyo kwenda Pangani mpaka Mombasa. Hiyo ni *point*, nchi tutaichora chora na juzi nilisikia nakushukuru Mheshimiwa John Malecela niliona barua yako ulimwandikia Waziri wa Mipango juu ya barabara kuambaa ambaa na Ziwa Tanganyika kutokana na Kamati ya Ulinzi. Ile barua kwa bahati tumeshaizungumza na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, ni ya kuifanya kazi mara moja maana ina *point*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nchi hii itakwenda kwa kasi, kwa kasi mpya. Hili la usimamizi, usimamizi wa matumizi niseme tu nimekwishatoa agizo jana kuanza mara moja mkisha idhinisha hii bajeti. Katibu Mkuu wangu na watalaam wengine wanakaa na watalaam wa kodi wanakaa tuzungumze namna ya kufuatilia shilingi kutoka Hazina mpaka kijiji fulani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, zamani kulikuwa na kitu kilichokuwa kinaitwa *Budget Supervision, Budget Supervision Unit*, wale mliokaa Serikalini. Hili ni suala la kurejea upya, tuangalie kama hatuwezi kuirejesha ili tusimamie vizuri zaidi fedha, lakini hata kabla ya hapo wiki iliyopita nilisaini amri ya Serikali ya Wizara ya Fedha, lakini ni ya nchi nimesaini kanuni itakayotoa adhabu na tozo yaani *Penalties and Surcharges*, inaitwa *Penalties and Surcharges Regulations* kwa mtumishi yejote wa Serikali atakayekiuka

taratibu za fedha na kanuni hizo zimeanza kazi mara moja kuanzia wiki iliyopita ziko tayari. Tulisahau kupiga watu faini na kuwatoza na kuwawekea kashikashi. Hii *regulation* itaanza kufanya kazi pindi tukiandaa jambo kuhusiana na hili lililozungumzwa hapa na ninyi Waheshimiwa Wabunge kwamba tuweke utaratibu mpya wa kufuatilia fedha na kupata *Value For Money*.

Mheshimiwa Spika, nina *unit* pale inaitwa *Technical Audit Unit* ile nayo inahitaji iimarishe zaidi, labda iimarishe na ipanuliwe ni kati ya mambo nimewaambia wataalam wangu wayashughulikie kabla ya Oktoba ili niweze kuhakikisha yanakwenda sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora, Tanzania pamoja na matatizo yetu yote tuna Utawala Bora, nafikiri Mheshimiwa Rais wetu sisi Mawaziri huwa siku nyingine anatuasa, anasema ninyi Mawaziri msikae kae hapa kwa woga woga hivi yale mazuri mnayofanya semenii, maana tulikuwa tumekaa kaa kiungwana ungwana katika mambo haya hakuna uungwana ungwana.

Mheshimiwa Spika, kuna kusema ukweli na mimi nakuambia sisi tulikuwa tunanyanyaswa nyanyaswa kidogo hapa. Mambo ya Utawala Bora nakwambieni kwamba Benki ya Dunia kufuatia utafiti uliofanyika kati ya kipindi cha mwaka wa 1996 mpaka 2004 ambapo Tanzania ni mionganoni mwa nchi tano za Afrika zilizoonyesha mafanikio ya kuridhisha katika eneo la Utawala Bora, hawa ni benki ya dunia.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora ni mambo kama haya, Bunge hapa lenye watu wazuri, wanauliza maswali hata kama mgeni kama yule wa leo kwa kiingereza kizuri, kwa sababu kuuliza ni jambo moja lakini kiingereza je, kilikuwaje? Kilikuwa kizuri. Wapo hapa watu wanaosema mambo ya kielimu kabisa wanasukuma mambo ndiyo haya ninayoeleza hapa na haya yote ni yale magoli yenu niliyoeleza kwenye *speech*. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi ni kati ya nchi zenyetane Utawala Bora, ina Bunge, Mahakama zinazofanya kazi hata kama zina matatizo, polisi na Serikali inayofanya kazi. Sijui kama Waheshimiwa Wabunge wanajua kwamba kuna nchi hapa Afrika ambazo Serikali ipo pale Makao Makuu tu. Ndani kwenye vijiji hakuna hata Mwenyekiti wa Kijiji sana sana ni mchawi mkuu wa kijiji, hakuna mtu zaidi. Mtawala wa pale ni yule mtu mwenye uchawi anatisha tisha watu pale basi ndiye mtawala, hakuna. Hapa sisi tuna Serikali mpaka ya kijiji, mpaka ya kitongoji. Nchi hii ina utawala jamani tuseme tu vizuri na wala tusione aibu kwa hiyo, sisi tumesifiwa. (*Kicheko*)

Halafu hii nchi, ni mionganoni mwa nchi tatu Barani Afrika zinazoonyesha mafanikio ya kuridhisha katika vita dhidi ya rushwa. Yupo na Waziri mzima, yupo Waziri mzima kazi yake ni hiyo tu saa 24, yuko ndani ya Tanzania, huyo ni Mheshimiwa Wilson Masilingi. Kwa hiyo, tuna utawala Bora na haya ndiyo tunayovuna sasa unaona wanatusema vizuri ndiyo tunayovuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, asilima 4.5 mapato ya Zanzibar, chimbuko la asilimia 4.5 ilikuwa huko nyuma namna ya kugawana faida kutokana na Benki Kuu kwa makubaliano mionganoni mwetu. Sisi, SMT na SMZ tukafikia hiyo *formula* ya 4.5. Kitu ambacho watu wameshindwa kufahamu vizuri ni kwamba asilimia 4.5 inakua jinsi makusanyo yanavyozidi kuongezeka na asilimia 4 inazidi kuongezeka. Kwa mfano, mwaka 2002/2003 Bajeti ya Zanzibar kwa *formula* hiyo walipata shilingi milioni 7,000 yaani bilioni 7.3. Mwaka uliopita bilioni 11.9, mwaka huu bilioni 15.5. Wanazidi kupata tu, wanazidi kupata, hata hivyo Tume ya Mheshimiwa William Shellukindo hivi tunavyozungumza iko kazini kuangalia kama *formula* hii itatosha au kama haitoshi basi iweje, kwa hiyo, hilo linakuja. Kwa Zanzibar wale waliokuwa na wasiwasi juu ya Bandari ya Zanzibar, Bandari ya Zanzibar itajengwa, itajengwa. Kulikuwepo kigugumizi kidogo lakini kimekwisha lakini tarehe 30 Juni, 2005 tutasaini mikataba na mara baada ya hapo tunasaini mkataba mwingine na mambo yanakwenda kama yalivyopangwa, msiwe na wasiwasi. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kumalizika*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri usijali kengele ya Katibu, wewe endelea mpaka utakaposikia kengele yangu mimi nasema hivi. (*Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, sawa sawa. Kuhusu hii misamaha ya madeni hili tangazo la juzi, yule Waziri alijaribu kueleza hapa, lakini leo niseme tu kwamba sisi kama nchi bado tunajaribu kuelewa maana yake kwetu ni nini na yako mambo mawili ambayo hayakusemwa, moja ni lazima haya matangazo ya juzi Jumapili yaridhiwena yaidhinishwe na Wakuu wa Nchi hizi za G8 wanaokutana tarehe 6 na 7 Julai, 2005 huko Scotland, Greenangles wanaita. Ya pili ni lazima bodi za benki hizo, benki ya dunia, *IMF*, *ADB*, bodi za benki hizo nazo ziidhinishe maana benki hizo hazikukupesha G8 zimetukopesha sisi. Sasa sisi si lazima twende tuseme tumepata mfadhili anayetaka kufanya hivi na hivi? Kuna hoja ya kujenga. Kwa hiyo, mpaka hapo tutakopofikia ngazi hiyo ndiyo tunaweza tukasema kwa ujumla maana yake ni nini.

*Mheshimiwa Spika, lakini nieleze tu kwa kifupi kwamba kama haya yote yakienda vizuri tunafikiri kwamba hakutakuwepo na tofauti ya matumizi ya fedha hizi na tulivyokuwa tunatumia zile za misamaha ya huko nyuma kutokana na maamuzi ya nchi za kundi la Paris (*Paris Club*). Kwa hiyo, tutatumbukia tu kwenye MKUKUTA, kulingana na watakavyosema wao kwa sababu wengi wa hawa wanataka fedha hizi ziende kwenye elimu, kama wengi wenu walivyopendekeza kwenye afya, kwenye maji, kwenye maeneo yale ambayo yanasadid a sana maendeleo vijijini. Sisi hatuna mgogoro na hayo ni suala tu sasa la kuja kuelewana nao mbele ya safari. Wako watu ambao wamekuwa wakiibeza beza hii bajeti. Kuna waliosema bajeti hii haikumsaidia maskini mimi nimeshangaa sana kati ya mshangao wangu mkubwa. Bajeti hii kama nilivyoeleza nusu ya bajeti hii imekwenda kusaidia maskini moja kwa moja, lakini haina maana kwamba ilitakiwa itumbukizwe fedha kwenye mifuko ya watu. Hakuna bajeti ya namna hiyo, eti ikusaidie ukiwa maskini kwa jina Mramba vema, Mwando sya vema, Lukuvi X, siyo hivyo, kwa sababu bajeti ya Serikali kama nilivyo kuwa nawaambia watu wengine juzi siyo sawa na Father Christmas. Hii siyo Father Christmas anayesema kaeni hapo*

huyu *pencil*, huyu peremende, huyu soda. Bajeti ya Serikali ni chombo kama tulivyoelezwa hapa siku moja ni chombo cha kuendeleza nchi, kiuchumi na kijamii, ni chombo. Kwa hiyo, suala la kujuliza ni je, chombo hiki maana kila mwaka tunaoa hiki chombo ili kiwe kizuri zaidi. Je, mwaka huu tumekidhi haja hiyo? Mimi nasema ndiyo kwa sababu asilimia hamsini ya bajeti hii imekwenda kwenye eneo la MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA wote ni *pro-poor*, MKUKUTA wote ule ni habari ya kukuza uchumi na kupambana na umaskini wote ule. *TASAF*, *MMEM*, *MMES* Wizara yote ya Kilimo, Wizara ya Ujenzi kila barabara inapofunguliwa inafunguliwa kwa ajili ya maskini kwa sababu ingawa maskini hana gari lakini mazao yake lazima yasafirishwe kwa lori, dawa zake lazima zitoke mahali ziende kwenye kijiji chake. Mtoto wake akitaka kwenda Chuo Kikuu lazima apitie kwenye barabara aende Dar es Salaam au Mwanza au Iringa. Kwa hiyo, barabara ni ukombozi mkubwa sana, tukitoa aina fulani za kodi, *VAT* kwenye reli kwenye vifaa vya treni, maana yake ni hiyo hiyo. Kwa hiyo, Bajeti hii kwa kweli unaweza ukasema ni Bajeti ya maendeleo vijijini na vijijini ndiko wanakokaa wale maskini. Lakini wengine wanasema, sasa hii kodi ya *PAYE* hii walipandisha kidogo walisema tutoke kwenye mshahara wa shilingi 60,000 twende kwenye shilingi 80,000.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kukueleza ukweli mmoja. Huko kwa watu binafsi hata yale makampuni makubwa yanayolipa, hakuna ahueni kama huku Serikalini na sisi wengine tunajivunia sana kuifanyia Serikali yetu kazi, sio tu kwa sababu sisi ni wazawa na wazalendo, lakini kwa sababu kule maslahi yake ni mazuri. Kuna watu leo hii tunavyozungumza wanakimbia kwenye kampuni za binafsi, wanakuja Serikalini. Wapo, kwa nini wapo, kwa sababu marupurupu ya Serikali ni ya ajabu, linganisha huyu na mtu ambaye ni mfanyabiashara wa kawaida ana duka hapa Dodoma, duka la kawaida tu sio duka kubwa, aliye kwenye ile sekta ambayo hapati pato la zaidi ya shilingi milioni 20 au 30, kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, tuseme mtu anayepata shilingi hata hii 80,000, chukua mtu anayepata pato lake la shilingi 80,000 kwa mwezi hapa Dodoma, mtu wa kawaida ambaye hafanyi kazi Serikalini na huyu wa Serikalini. Tofauti yao ni nini, wote wanapata shilingi 80,000 kwa 80,000, lakini yule wa Serikali ana pensheni, ndiyo hii imetufikisha tunazungumza hapa habari za pensheni. Yule mwenzake hana pensheni, huyu wa Serikalini ana matibabu ya kulipiwa na Serikali kwa asilimia tena. yule wa kule hana matibabu, na hii ndiyo inaeleza kwanini ukienda hapo mlangoni nyiye Wabunge mnajua. Sisi pale tunavamiwa na watu wote hawa wenye shida za kila namna. Hana hela ya kununulia dawa, hana hela ya sijui ya kwenda kudunga sindano ya Malaria, alishapiga moja bado mbili. Ndiyo wanaotungojea sisi Wabunge hapo kwenye geti. Kwa hiyo, yule mtu wa Serikali anaenda tu kwa *DAP*, *DAP* anampeleka. Kuna likizo unaambiwa nenda likizo na mke na watoto wanne sijui sita, kuna posho ukifanya kazi za ziada, hata ukifa Serikali inakuzika, kuna sanda na jeneza, ndiyo ni taratibu za Serikali. Yule mtu mwingine akifa hapa ndiyo tunachanga, tunaunda hata vyama vya kuzikana. Ili tusaidie watu wa namna hii, kwenye miji sasa kumezuka vyama vya kuzikana, kwa sababu Serikali haiko iwazike wale ambaio sio watumishi wa Serikali.

Mheshimimiwa Spika, kwa hiyo, mtumishi wa Serikali kwa kweli hawezi kusema kwamba ile 80,000 ndiyo hiyo hiyo ukilinganisha na yule ambaye sio mtumishi wa Serikali na wala Serikali hii haiwezi kushindana na mtu anayelipa mara kumi kwa sababu hatuwezi. Lakni tunasema ukijumlisha yale yote, hiyo kidogo ya shilingi 80,000 na marupurupu mengine, kwa kweli anajikuta yuko katika hali nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kumetokea hoja nyingi sana juu ya mikopo, na nimefurahi sana kuna baadhi ya Wabunge wamezungumza vizuri sana, ukombozi wetu sisi kama Wabunge na ukombozi wa wapiga kura wetu ambaao ni hawa maskini tunaowazungumzia hapa, uko kwenye kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa, ndiyo mkombozi. *NMB* hata ingefika pale nyumbani kwako kwenye kijiji, mpaka ukapate hapo mkopo si jambo rahisi kwa sababu benki ni benki. Lakini chama chako wewe mwenyewe, nimefurahi sana jana nimesikia Idara ya Magereza imeunda *Magereza SACCOS*, haya ndiyo maneno ninayotaka kusikia, kwenye Wizara kuna *SACCOS*, kwenye Mashirika kuna *SACCOS* kila mahali kuna mfuko wa kuweka na kukopa, huo ndiyo ukombozi na tafadhali tung'ang'anie na mimi nimefurahi sana hapa Dodoma ndiyo wameelewa jambo hili. Labda kwa sababu kuna Naibu Waziri hapa amefanya kazi kubwa ya kuwahamasisha watu, kwenye Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, ukipita kwenye vyama hivi vya Dodoma, vyama vya Mbeya, vyama vya Mikoa kadhaa na kwenye fedha hizi za Kanda ya Ziwa nilizozungumzia, kuna eneo kubwa la kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa, eneo kubwa kabisa, fedha nyingi sana tumetenga. Kwa hiyo, ndugu zangu ndiyo maana nikarekebisha kwenye Hotuba hii yale mambo ya Benki Kata, ya vyama vya kuweka na kukopa. Nikarekebisha ili kusudi sasa vyombo hivyo vidogo vidogo sana viweze kuijandikisha hapo hapo Wilayani na vihudumiwe na watawala hapo hapo Wilayani, ambapo sasa hivi vilikuwa vinakwenda mpaka Dar es Salaam na vingine vinaandikishwa kama Ushirika kwa utaratibu wa Ushirika.

Kwa hiyo, wale ambaao wanataka kuwa ushirika wataendelea kuandikishwa kama ushirika (*SACCOS*), wale ambaao hawataki kuwa ushirika watajiandikisha kama *Associations*, Umoja (*SACAS*), halafu wanajiunga wanakuwa wakubwa zaidi ngazi ya Kata, wanakuwa Benki Kata, wanajiunga Benki Kata nyingi zaidi wanakuwa Benki ya Wilaya, *Community Bank*, Benki Jamii na kule ambako wameanza zimefanikiwa. Nenda Mbinga, Waheshimiwa Wabunge wako hapa, nenda Mbinga, nenda Mufindi, nenda Mwanga, Morogoro ndiyo wanazungumza sasa na mimi niko mbioni, kila mtu mahali pake, tukifanya hivi zitazuka Benki za Wilaya 200, hivi ndani ya miezi sita au mwaka zitazuka.

Mheshimiwa Spika, zile sasa ndizo za kuunganisha na Benki kubwa kama akina *NMB*, watakapokuja na Benki ya Biashara na Benki ya *CRDB*, hizo ndizo zitawaunganisha. Kwa hiyo, yule mkubwa atakopesha yule mdogo zaidi na mdogo zaidi na baadae Waziri wa Fedha akiona inafaa wakati muafaka anaweza akafidia hasa *interest rates* kwenye vikundi hivi ili vikope kwa urahisi zaidi, hili ni jambo la baadaye. Lakini ni jambo linalowezekana, kwa taaluma hiyo linawezekana kabisa. Nimalizie kwa kusema kitu kimoja, wale watu waliokuwa wanasesma hii Bajeti ni ya kisiasa, nawashangaa sana.

Kwa nini isiwe ya kisiasa? Bajeti hii ni chombo cha kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama kinachoitwa Chama cha Mapinduzi, na kwa miaka mitano hiyo iliyopita mimi naweza nikawaambieni hiyo kazi nimeifanya kwa umakini mkubwa, katika Bajeti. (*Makofi*)

Nimeweka mazingira bora vijijini na mijini, maskini na tajiri, nje na ndani, kwa njia ya Bajeti, kila mnapoidhinisha *Finance Bill*, ikawa *Finance Act*, ndiyo mazingira hayo. Tumeshughulikia mambo ya *Micro-economics*, mfumuko wa bei, ujazi wa fedha, mazingira mazuri ya uwekezaji. Haya yamekuja kwa njia za Bajeti, Serikali ina-*propose* ninyi mnaidhinisha, wote sambamba. Bunge na Serikali tumekuwa pande mbili za sarafu moja ya CCM. Lakini kama unavyo jua kila ngoma inawasindikizaji na ngoma nzuri sana inayoitwa mdundiko ndiyo inawasindikizaji wa kila namna. Sasa ndani ya ngoma ya CCM, kuna wasindikizaji. Kwa hiyo, huu ni mdundiko wa CCM ambao kijiji kizima kilijua kuna mdundiko mahali fulani, lakini wasindikizaji walikuwepo. Hao wanaolalamika kwamba Bajeti hii ilikuwa ya kisiasa ndiyo wale waliingia kwenye mdundiko bila kujua ile ngoma ilikuwa hasa ya nani. Wakaenda nayo miaka mitano mpaka wakajikuta wamepotea na mwezi Oktoba mdundiko unaendelea. Sisi tunafanya kazi kisayansi hapa. Haikuwa lazima tutangaze, lakini kila mtu alijua iko ilani na sheria tukatunga za kuhalalisha Bajeti za kuhalalisha ilani na ndivyo itakavyokuwa kwa kasi zaidi, kwa nguvu mpya na ari mpya. (*Makofi/ Kicheko*).

Waheshimiwa Wabunge, mimi nawatakia kila la heri, njia ni nyeupe kabisa tuonane tena hapa Novemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyotolewa na inayohitaji uamuzi ni kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Ndiyo hoja inayohitaji uamuzi. Sasa kwa utaratibu wa kuamua Hoja hii, *Sergeant-At-Arms* atapiga kengele ili kama kuna Mheshimiwa Mbunge yupo nje aweze kuingia ndani halafu Katibu ataita jina moja moja kwajili ya kupiga kura ya kupitisha Bajeti ya Serikali.

(*Hapa Kengele ilipigwa ili Waheshimiwa Wabunge waliopo nje ya Ukumbi waingie ndani ya ukumbi wa Bunge*)

(*Hapa Upigaji wa Kura Kwa Kutaja Majina Ulianaza*)

Mheshimiwa Frederick T. Sumaye	-	Ndiyo
Mheshimiwa William V. Lukuvi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Anna M. Abdallah	-	Ndiyo
Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Zakia H. Meghji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Y. Ng'wandu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Edgar D. Maokola - Majogo	-	Hakuwepo

Mheshimiwa Daniel N. Yona	-	Ndiyo
Mheshimiwa Harith B. Mwapachu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Gideon A. Cheyo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Edward N. Lowassa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Wilson M. Masilingi	-	Ndiyo
Mheshimiwa John P. Magufuli	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Basil P. Mramba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Phillemon M. Sarungi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri	-	Ndiyo
Mheshimiwa Charles N. Keenja	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandomsy	-	Ndiyo
Mheshimiwa Joseph J. Mungai	-	Ndiyo
Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngwilizi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Balozi George C. Kahama	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Asha -Rose M. Migiro	-	Ndiyo
Mheshimiwa Juma A. Ngasongwa	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Andrew J. Chenge	-	Ndiyo
Mheshimiwa Juma J. Akukweti	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Shamim Parkar Khan	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari	-	Ndiyo
Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Pius P. Mbawala	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir	-	Ndiyo
Mheshimiwa Bujiku K. Sakila	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda	-	Ndiyo
Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita	-	Ndiyo
Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. R. Msabaha	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Hussein Alli Mwinyi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha	-	Ndiyo
Mheshimiwa Anthony M. Diallo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Abdulkader A. M. Shareef	-	Ndiyo
Mheshimiwa Rita Louise Mlaki	-	Ndiyo
Mheshimiwa Njelu E. M. Kasaka	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed	-	Hakuwepo
Mheshimiwa William H. Shellukindo	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Dr. William F. Shija	-	Hakuwepo
Mheshimiwa John S. Malecela	-	Ndiyo

Mheshimiwa Eliachim J. Simpara	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Omar S. Kwangw”	-	Ndiyo
Mheshimiwa Anne S. Makinda	-	Ndiyo
Mheshimiwa . Sophia M. Simba	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Mgana I. Msindai	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Henry R.Mgombelo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Isaac M. Cheyo	-	Hapana
Mheshimiwa Thomas Ngawaiya	-	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa	-	Hapana
Mheshimiwa Muttamwega B. Mgaywa	-	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi	-	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mheshimiwa Ali Said Juma	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Dr. Willibrod P. Slaa	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Ali Said Salum	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Adelastela E. Mkilindi	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Grace S. Kiwelu	-	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Shoka Khamis Juma	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa <i>Major</i> Jesse J. Makundi	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Frank G. Magoba	-	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mheshimiwa Bakari Shamis Faki	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Dr. Amani W. A. Kabourou	-	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mheshimiwa Aisha P. Magina	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Teddy Louise Kasella - Bantu	-	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mheshimiwa Freeman A. Mbowa	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah	-	Ndiyo
Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah	-	Ndiyo
Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Bahati Ali Abeid	-	Ndiyo
Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud	-	Ndiyo
Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali	-	Ndiyo
Mheshimiwa Omar Mjaka Ali	-	Ndiyo
Mheshimiwa Salum Omar Ali	-	Hapana
Mheshimiwa Fatma Saidi Ali	-	Ndiyo
Mheshimiwa Khamis Salum Ali	-	Ndiyo
Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally	-	Ndiyo
Mheshimiwa Shaibu Ahmadada Ameir	-	Ndiyo
Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir	-	Ndiyo
Mheshimiwa Rostam Aziz	-	Ndiyo
Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar	-	Ndiyo

Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Joel N. Bendera	-	Ndiyo
Mheshimiwa Lydia T. Boma	-	Ndiyo
Mheshimiwa Zamda S. Bozzen	-	Ndiyo (<i>Makofî</i>)
Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian	-	Ndiyo
Mheshimiwa Robert J. Buzuka	-	Ndiyo
Mheshimiwa Margareth J. Bwana	-	Ndiyo
Mheshimiwa Kisyeri W. Chambiri	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Aaron D. Chiduo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Diana M. Chilolo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Samwel M. Chitalilo	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Anatory K. Choyo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Omar Said Chubi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Paschal C. Degera	-	Ndiyo
Mheshimiwa Leonard N. Derefa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail	-	Ndiyo
Mheshimiwa Abdallah Khamis Feruzi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Dr. Lawrence M. Gama	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Lephy B. Gembe	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jina Khatib Haji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Edson M. Halinga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan	-	Ndiyo
Mheshimiwa Salama Khamis Islam	-	Ndiyo
Mheshimiwa Yahya Kassim Issa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ismail J. R. Iwvatta	-	Ndiyo
Mheshimiwa Yusufu Kombo Juma	-	Ndiyo
Mheshimiwa Peter Kabisa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Charles H. Kagonji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Janet B. Kahama	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Rhoda L. Kahatano	-	Ndiyo
Mheshimiwa Stephen M. Kahumbi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Ally A. Karavina	-	Ndiyo
Mheshimiwa Stephen M. Kazi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalifan	-	Ndiyo
Mheshimiwa Zahor Juma Khamis	-	Ndiyo
Mheshimiwa Sharifa Mbarouk Khamis	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib	-	Ndiyo
Mheshimiwa Juma S. Kidunda	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda	-	Ndiyo

Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Estherina Kilasi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Halima Omar Kimbau	-	Ndiyo
Mheshimiwa Paul P. Kimiti	-	Ndiyo
Mheshimiwa Emmanuel E. Kipole	-	Ndiyo
Mheshimiwa Remidius E. Kissassi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Hassy H. B. Kitine	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Stanley H. Kolimba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Komba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Parseko V. Kone	-	Ndiyo
Mheshimiwa Hadija K. Kusaga	-	Ndiyo
Mheshimiwa William J. Kusila	-	Ndiyo
Mheshimiwa Lekule M. Laizer	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Masumbuko R. M. Lamwai	-	Ndiyo
Mheshimiwa Benedict K. Losurutia	-	Hakuwepo
Mheshimiwa George M. Lubeleje	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Musa A. Lupatu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Abdula S. Lutavi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ernest G. Mabina	-	Ndiyo
Mheshimiwa Philip A. Magani	-	Ndiyo
Mheshimiwa Beatus R. Magayane	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame	-	Ndiyo
Mheshimiwa Danhi B. Makanga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Paul N. Makolo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jackson M. Makwetta	-	Ndiyo
Mheshimiwa Benito W. Malangalila	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Anne K. Malecela	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Philip S. Marmo	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Ibrahimu W. Marwa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Robert K. Mashala	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Janeth E. Mashele	-	Ndiyo (<i>Makofit</i>)
Mheshimiwa Haroub Said Masoud	-	Ndiyo
Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid	-	Ndiyo
Mheshimiwa Halimenshi K. R. Mayonga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Salome J. Mbatia	-	Ndiyo
Mheshimiwa Monica N. Mbega	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Simon M. Mbilinyi	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Talala Bana Mbise	-	Ndiyo
Mheshimiwa Bakari M. Mbonde	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mchande Salim Mchande	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Bernard K. Membe	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki	-	Ndiyo

Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Jenista J. Mhagama	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Juma M. Mikidadi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed H. Missanga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Margareth A. Mkanga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Nimrod E. Mkono	-	Hakuwepo
Mheshimiwa George F. Mlawa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Oscar T. Mloka	-	Ndiyo
Mheshimiwa Raphael N. Mlolwa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed	-	Ndiyo
Mheshimiwa Sumri A. S. Mohamed	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Elisa D. Mollel	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Balozi Getrude I. Mongella	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Alhaji Ahamadi H. Mpeme	-	Ndiyo
Mheshimiwa Benson M. Mpesya	-	Ndiyo
Mheshimiwa Kilontsi M. M. Mpologomyi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Felix C. Mrema	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ruth B. Msafiri	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela	-	Ndiyo
Mheshimiwa Herbet J. Mtangi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte	-	Ndiyo
Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji	-	Hakuwepo
Mheshimiwa James P. Musalika	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Ali Machano Mussa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ali Sheha Mussa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Daimon M. Mwaga	-	Ndiyo
Mheshimiwa John L. Mwakipesile	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Venance M. Mwamoto	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mbaruk Kasim Mwandoro	-	Ndiyo
Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila	-	Ndiyo
Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri	-	Ndiyo
Mheshimiwa Omar Mohamed Mwenda	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Damas P. Nakei	-	Ndiyo
Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala	-	Ndiyo
Mheshimiwa Bernadine O. Ndaboine	-	Ndiyo
Mheshimiwa Richard M. Ndassa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Edward N. Ndeka	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Job Y. Ndugai	-	Ndiyo
Mheshimiwa Asha Ali Ngede	-	<i>Yes (Makofi)</i>

Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru	-	Ndiyo
Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye	-	Ndiyo
Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jumanne Hamisi Nguli	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura	-	Ndiyo
Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Said Juma Nkumba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya	-	Ndiyo
Mheshimiwa Paul E. Ntwina	-	Ndiyo
Mheshimiwa Tembe K. Nyaburi	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Rosemary H. K. Nyerere	-	Ndiyo
Mheshimiwa Charles M. Nyerere	-	Ndiyo
Mheshimiwa Thomas S. Nyimbo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mathew Taki Ole- Timan	-	Ndiyo
Mheshimiwa Omar Juma Omar	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Semindu K. Pawa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mwaka Abraham Ramadhani	-	Ndiyo
Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq	-	Ndiyo
Mheshimiwa Hashim A. Z. Saggaf	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed Ali Said	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh	-	Ndiyo
Mheshimiwa Issa Mohamed Salim	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Lucas L. Selelii	-	Ndiyo
Mheshimiwa Haji Juma Sereweji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame	-	Ndiyo
Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah	-	Ndiyo
Mheshimiwa Leonard M. Shango	-	Ndiyo
Mheshimiwa Henry D. Shekiffu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jacob D. Shibili	-	Ndiyo
Mheshimiwa Iddi M. Simba	-	Ndiyo
Mheshimiwa John E. Singo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud	-	Ndiyo
Mheshimiwa Esha H. Stima	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman	-	Ndiyo
Mheshimiwa Khalid S. Suru	-	Ndiyo
Mheshimiwa Aridi M. Uledi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha	-	Ndiyo
Mheshimiwa Maria D. Watondoha	-	Ndiyo
Mheshimiwa Christopher S. Wegga	-	Ndiyo

Mheshimiwa Martha M. Wejja	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir	-	Ndiyo

SPIKA: Mheshimiwa Murji amerudi sasa. Piga kura yako.

Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji	-	Ndiyo (<i>Makofî</i>)
----------------------------------	---	-------------------------

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati Makatibu wanahesabu kura, ni kwamba Bajeti inatakiwa ipitishwe kwa kura siyo theluthi mbili ya kura, ni *simple majority*, zaidi ya nusu. Sasa, zaidi ya nusu maana yake nini. Tulipochaguliwa mwaka 2000, tulikuwa Wabunge 295. Hapa kati kati Mwenyezi Mungu amechukua Watano, tukabaki 290. Hapo katikati Chama cha UDP kikamfukuza Mbunge wake, tukabaki 289. Hapa katikati Mheshimiwa Eliachim Simpasa akaleta hoja ya kuwasimamisha Wabunge wengine watatu, kwa hiyo, tukabaki 286, ndiyo tuliopo leo, Kikatiba 286, nusu yake ni 143. Lakini tunatakiwa tupate zaidi ya nusu, yaani kura moja zaidi, angalau mmoja zaidi. Kwa hiyo, kama kura za ndiyo zitakuwa 144, basi Bajeti ya Serikali itakuwa imepita. Tusubiri matokeo.

(*Hapa Spika alikabidhiwa matokeo na Katibu wa Bunge*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimekabidhiwa matokeo ya kura tuliozipiga sasa hivi, nayo ni kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, Wabunge waliopiga kura za Hapana au Siyo ni watatu, ambao hawakupiga upande wowote, waliosema *Abstain* ni 11, ambao hawakuwepo Bungeni kwa sababu moja au nyingine ni 53 na kura za Ndiyo ni 219. Sasa natangaza kwamba Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 imepitishwa na Bunge hili. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndio mwisho wa kazi iliyopangwa kwa kikao cha leo. Kwa hiyo, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.39 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 16 Juni, 2005 saa tatu asubuhi*)